**18 MEI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 18 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stergomena Lawrence Tax, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Katibu.

**18 MEI, 2022**

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali yetu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa sasa aulize swali lake.

Na. 216

**Tatizo la Ajira Nchini**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, ni vijana wangapi hawana ajira nchini na Serikali imewaandaaje kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali namba 216 lililoulizwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2021 unaonesha kuwa vijana wa umri wa miaka 15 – 35 ni 17, 712,831 ambapo kati yao, vijana 14,219,191 wana uwezo wa kufanya kazi na vijana 3,493,640 hawana uwezo wa kufanya kazi kutokana na sababu mbalimbali kama vile masomo, ugonjwa na kadhalika. Kati ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi, vijana 12,486,682

sawa na asilimia 87.8 wana ajira na vijana 1,732,509 sawa na asilimia 12.2 hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha vijana wanaandaliwa ipasavyo kushindana katika soko la ajira, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya Serikali imekuwa ikiandaa programu mbalimbali za kuweza kuhakikisha kwamba kunakuwa na mikakati ya kuwapatia vijana fursa za ajira na kuwaandaa kuweza kupata fursa ikiwemo mafunzo mbalimbali kwa maana ya uzoefu kazini, *internship* kwa hitimu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo imekuwa na *scheme* mbalimbali ya kuweza kuwapatia mikopo, mafunzo, ya utarajali na mafunzo ya kilimo cha kisasa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba kupitia mafunzo haya, zaidi ya vijana 84,245 wamenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Elimu pia Wizara ya Kilimo, kuweza kuhakikisha zinatolewa *program* mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikopo, mafunzo na kutengeneza fursa mbalimbali zaa jira kutokana na Wizara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hili tatizo la ajira ni tatizo kubwa sana hapa nchini hivi sasa. Je, kwanini Serikali isifanye *tracer study* na kuandaa *database* ya vijana wote wanaohitimu mafunzo ili kuweza kuwatambua, kuweza kuwafuatilia na kujua namna nzuri ya kuwapatia ajira Serikalini pamoja na sekta binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwanini Serikali isiandae mfumo mzuri wa kuwakopesha hawa vijana, wale wanaotaka kuingia kwenye ujasiriamali hata walau mtaji wa Milioni 20 wa kuanzia na wakajidhamini kwa vyeti vyao vya vyuo?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali yaho Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mweyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na tatizo la ajira lakini kwa sehemu kubwa Serikali imeweza kulifanyia kazi Serikali ya Awamu Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan. Tumekuwa na mikakati mingi ya kuweza kuhakikisha tatizo hili linapungua, mojawapo kwanza amefungua *private sector* kwa kubadilisha sheria pamoja na sera. Sambamba na hilo katika maeneo mengi vijana sasa wameanza kupata ajira kwenye miradi mikuwa ya maendeleo, lakini sambamba na hilo wameendelea kutoa ajira katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili katika kutafuta kanzidata, ni kweli tumekuwa katika kila nafasi ambazo zinatolewa kwa ajili ya ajira majina yale ambayo wamekuwa waombaji tumekuwa tukiyachukua kupitia kitengo cha ajira *TAESA* ili kuweza kupata takwimu sahihi za vijana ambao wamemaliza Vyuo Vikuu. Sambamba na hilo hatuwaachi hivyo, kumekuwa na mafuzo mbalimbali ya kuwapa *internship*, wapo vijana ambao wamepelekwa *TRA* na taasisi nyingine nyingi za Serikali kuweza kupata mafunzo ya uzoefu kazini sambamba na kuanzisha pia utaratibu wa kuwauhisha wale

ambao wamehitimu kwenye vyuo mbalimbali vikiwemo vya *VETA* na *FDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo tumekwishakuanza kufanya, tumemaliza *manpower survey* kuweza kujua, lakini tunaenda kwenye hatua mbili sasa ya kufanya *labour survey* kuweza kujua idadi ya vijana ambao wanaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na mikopo, Serikali hii imekuwa ikitoa mikopo ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan tena kwa upendo mkubwa, ukiangalia hakuna kijana yoyote ambaye hapati mkopo, kumekuwa na *scheme* za utoaji mikopo katika elimu. Kwa mfano, kwa Shule za Msingi, tumekuwa tukitoa elimu bila malipo, lakini akimaliza sekondari anaenda Chuo Kikuu anakutana na bodi ya mikopo ambayo inampa mikopo, akitoa Chuo Kikuu, anapokuja nje anaenda kwenye Halmashauri zetu tunatoa mikopo ya 4:4:2 kwa maana ya asilimia Nne (4) kwa wanawake, asilimia Nne (4) kwa vijana na asilimia Mbili (2) kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo tumekuwa na scheme nyingine za makubaliano na mabenki mbalimbali kuweza kushusha riba na kutoa mikopo ikiwemo benki hizo za kilimo ambazo tayari zimekwishaanza kutoa na yalikuwa ni maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuweza kuhakikisha katika kila Halmashauri wanatenga maeneo maalum ya vijana kwa ajili ya kufanya kilimo na wanapewa mikopo kupitia Benki lakini pia Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge pia Mheshimiwa Luhanga Mpina ambaye ndiye muuliza swali kama mtapitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo, kule kuna mpango wa *building the better tomorrow* ambao unaenda kugusa vijana zaidi ya Milioni Moja katika kuhakikisha wanatengenezewa *scheme* za maeneo ya kilimo kwa

maana ya *block farming* na wajibu wa Wizara ya Kilimo, itakuwa ni kuandaa kwanza maeneo hayo lakini pili kutafuta fecha kwa ajili ya kuwapa vijana hao na kuweka miundombinu na tatu ofisi ya Waziri Mkuu itakuwa wajibu wa kuweza kuratibu shughuli hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa hayo tumeyaona kwa kweli vijana wakae tu mkao wa kula na watoe ushirikiano kwa Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan inawaona na inawaangazia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan hivi juzi, ametoa zaidi ya Shilingi Milioni 10 kila Mkoa kwa ajili ya wamachinga. Kwa hiyo, vijana wengi wako kwenye eneo hilo, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Yahaya Massare na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko dhamira ya Serikali ya kutoa ajira kwa vijana hasa kupitia vitalu nyumba, lakini vitalu nyumba hivi ni ghali sana. Je, Serikali iko tayari sasa kuweka ruzuku katika vitalu nyumba ili vijana wengi waweze kujiajiri kupitia eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Massare, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa na programu ya kutoa elimu kwa ajili ya vijana kujifunza

utengenezaji wa vitalu nyumba na tumekwishakufanya katika Halmashauri zaidi ya 82 na katika hayo maeneo ilikuwa wajibu wa kwanza ni kuhakikisha kwamba elimu inatolewa, lakini pia fedha na gharama zote zinaratibiwa na Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kupitia ofisi ya Waziri Mkuu. Ni kweli kitalu nyumba kimoja kilikuwa kinagharimu zaidi ya karibia shilingi milioni 12, baada ya kuliona hilo na kwa ushauri mzuri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na muuliza swali Mheshimiwa Massare akiwa mjumbe tulitembelea Zanzibar na tuliweza kuona kwamba kuna uwezekano wa kutengeneza vitalu nyumba bila kutumia mabomba ya chuma na kutumia tu vitu vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumekwishakuanza kuwa-*engage* wataalam kuweza kutusaidia zaidi namna gani watashusha gharama na kutafuta wadau wengine ambao watasaidia katika kuweza kuwapa mikopo vijana hawa katika maeneo haya. Kwa kweli eneo hili limeonekana linapokelewa vizuri na vijana, tutahakikisha kwamba kwa ushirikiano na ushauri ambao mnautoa tutaufanyia kazi kila wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali fupi la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo unaeleza ni kama vile uko nje ya Tanzania. Tuna vijana wengi sana wamekosa ajira zaidi ya miaka sita sasa, lakini unasema kule chini kuna nafasi kwenye Halmashauri za wao kupata fedha, ninafahamu kuna ile 4.4.2 kama ulivyosema, lakini mwisho wa siku vijana wengi mfumo unawaacha nje kwa sababu hawana sifa za kupata mikopo hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wako vijana wengi ambao kwa wakati huo na kwa jinsi alivyosema ameshindwa kutueleza takwimu hasa, Serikali tunazo takwimu za vijana hawa, tumeshafanya *Manpower survey*, lakini wale wote wanaofanya *application* ya ajira, Vyuo Vikuu vyote tumekuwa tukipata taarifa za ajira na *demographic population* ya wanafunzi ambao wanamaliza Vyuo Vikuu *at least* kila mwaka. Tunao vijana zaidi ya Laki Mbili wanaoingia kwenye soko la ajira kutoka vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya takwimu nikuambie Mheshimiwa ninazo za kutosha hapa na tutakueleza Serikali inawajali vijana kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunayo mifumo na programu ambazo tunaziandaa, labda programu ya kwanza nikikupa tu kwa faida yako tu Mheshimiwa uweze kujua na mengine nitakushirikisha ili tuwasaidie vijana kwenye eneo ni pamoja na hiyo *internship* ambayo inatusaidie siyo tu katika kuwafanya kupata mafunzo kazini, pia inawasaidia vijana hawa kuweza kuangaliziwa ajira ndani ya nje ya nchi kupitia wakala mbalimbali wa ajira waliosajiliwa na Ofisi Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia tumekuwa tukiendelea kuhakikisha tunatoa mikopo. Kwa hiyo, takwimu zipo, zaidi ya bilioni 150 zimekwishatolewa kwa vijana mbalimbali. Kwa hiyo, kama kuna vijana ambao wapo, labda pengine siyo Watanzania ni Wakenya, utanisaidia ili niweze kuwaingiza hapa na kuweza kuona ni

namna gani tunawasaidia. Kwa hiyo, ninakutaarifu tu kwamba nipo Tanzania na huu ndiyo utaratibu wa Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, Serikali ya takwimu na utekelezaji na Serikali inayowapenda vijana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Patrobas Katambi, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa majibu hayo. Tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

Na. 217

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Makete?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imeitenga shilingi milioni 900 kwa ajili ya kufanya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Hospitali hiyo ili iweze kuwa na miundombinu bora yenye hadhi ya Hospitali ya Wilaya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Makete ni moja kati ya hospitali chakavu sana. Ni hospitali ambayo imetembelewa na Mawaziri tofauti, Mheshimiwa Ummy akiwa TAMISEMI amefika, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Jafo amefika na Kamati ya Bunge ya TAMISEMI imefika wamejionea hali ya Hospitali ya Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipi ni kauli ya Serikali mimi kama Mbunge ningeomba msifanye ukarabati mjenge. Je, ipi ni kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tuna vituo vya afya cha Kitulo, tunayo zahanati ya Nungu, Kisungilo na Unyangogo, hizi zahanati zimekamilika hazina vifaatiba. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaatiba ili huduma zianze kutolewa kwa sababu wananchi wangu wa Makete, wametoa nguvu kazi yao wamejenga zahanati hizi na vituo vya afya lakini vifaatiba hamna. Ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Sanga kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa wananchi wa Jimbo la Makete, nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kumpa ushirikiano ili kuhakikisha wananchi wa Makete wanapata maendeleo ambayo yanatarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete ni kweli ni hospitali chakavu, Mheshimiwa Mbunge ameuliza hapa mara kadhaa Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ikamuahidi kupeleka fedha na sasa tumetenga mwaka ujao wa fedha milioni 900. Hii ni miongoni mwa hospitali 19 ambazo mwaka ujao wa fedha zitakabarabitiwa au kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba tunafanya tathmini na kuona hospitali zile zenye uchakavu mkubwa *beyond repair* tunafanya ujenzi mpya, lakini zile ambazo zinaweza kukarabatika, tutakarabati. Kwa hiyo, kauli ya Serikali ni kwamba kufuatia tathmini ambayo tutaifanya katika hospitali ya Makete tutatoa maelekezo rasmi kwamba Shilingi Milioni 900 inakwenda kujenga ama inakwenda kukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Vituo vya Afya vya Kitulo, Zahanati ya Nungu na nyingine kuhitaji vifaatiba. Katika mwaka wa fedha ujao, Serikali imetenga milioni 450,000 kwa ajili ya vituo vya afya na zahanati katika Jimbo la Makete ili vituo hivi viweze kupata vifaatiba. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shaban Shekilindi nimekuona.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, wananchi wa Kata ya Gale, na Kata ya

Makanya, wamejenga viuo vya afya kwa nguvu zao wenyewe.

Je, ni lini Serikali itatoa milioni 250 kama ilivyokuwa inatoa fedha hizo kwenye vituo vingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mkakati ambao umeendelea kutekelezwa na Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi kwamba Serikali imeendelea kupeleka fedha Milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, tumeendelea kupeleka Milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati na hospitali za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi vituo ambavyo wananchi wameanza ujenzi, Serikali itapeleka fedha ili tuweze kukamilisha ujenzi huo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali lingine la Ofisi ya Rais TAMISEMI, litaulizwa na Mheshismiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti.

Na. 218

**Ujenzi wa barabara za vijijini – Serengeti**

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara Jimbo la Serengeti hasa za vijijini ambazo hutumika kusafirishia mazao?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 971.78 zinazohudumiwa na *TARURA*. Barabara zenye hali nzuri ni kilometa 131.82, wastani kilometa 194.97 na mbaya ni kilometa 644.99. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 barabara zenye urefu wa kilometa 121.24 zilifanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali kwa gharama ya shilingi milioni 965.85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.494 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 152.24 ambazo ujenzi na matengenezo ya kilomita 138.74 za barabara na vivuko 34 yamekamilika. Matengenezo haya yanajumuisha barabara ya Mugumu – Masangula – Kemgesi kilometa 9.0, Kwitete – Mosongo – Wagete kilometa 25, Nyichoka – Maburi kilomita 6.0 na Barabara ya Nyamakobiti – Iselesele kilometa 7.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 2.41 kwa ajili

ya ujenzi na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 72.81 na vivuko vidogo 18.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jeremiah Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi tena. Nishukuru majibu ya Serikali yaliyotolewa kwa swali, lakini niombe kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza jumla ya barabara ambazo zilijengwa 2021/2022 na zitakazojengwa mwaka wa kesho zinaonesha wastani wa kilomita 100 tu kwa mwaka. Sasa basi jumla ya barabara zinazohudumiwa na *TARURA* ni zaidi ya kilomita 900, hii maana yake ni kwamba itatuchukua zaidi ya miaka tisa kujenga barabara zote zilizo chini ya *TARURA* katika Jimbo la Serengeti. Sasa basi Serikali haioni haja ya kutafuta fedha za ziada kwa ajili ya kuongezea Jimbo la Serengeti kwa sababu barabara ni nyingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tarehe 25 Julai, 2021, Naibu Waziri wa TAMISEMI aliwaahidi wananchi wa Serengeti kwamba barabara ya lami inayozunguka soko la Mugumu ingejengwa na kukamilishwa. Mpaka sasa hivi mkandarasi ameshasaini mkataba toka mwanzo wa mwaka huu lakini barabara ile haijengwi. Tunaomba *commitment* ya Serikali ya kujenga barabara ile ya lami ya kuzunguka soko la Mgumu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Msabi kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kuwakilisha ipasavyo wananchi wa Jimbo la Serengeti. Pili, kuhusiana na fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara katika Halmashauri ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeendelea kuongeza fedha ambazo zinakwenda kufanya matengenezo na ujenzi wa barabara vijijini na mijini. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2020/2021, bajeti ya Serikali kupitia *TARURA* ilikuwa bilioni 255, lakini 2021/22 Serikali iliongeza kutoka 255 mpaka bilioni 722, zaidi ya mara tatu ya bajeti. Pia mwaka ujao wa fedha tumeongeza kutoka 722 mpaka bilioni 822 *plus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii yenyewe inaonyesha namna Serikali ambavyo ina *commitment* kubwa ya kuongeza fedha kupitia *TARURA* ili barabara zetu ziendelee kujengwa. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata wao mwaka 2020/2021, bajeti ilikuwa ndogo, lakini imeendelea kuongezeka na tutaendelea kuhakikisha tunaongeza bajeti ili barabara za Serengeti zijengwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na barabara ya lami inayozunguka Soko la Mugumu, naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi na Watendaji wote wa Mamlaka hii ya Barabara *TARURA* kuhakikisha mkandarasi huyu anaanza kazi haraka iwezekanavyo na vinginevyo tutachukua hatua mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha barabara inakamilika mapema. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni, nimekuona.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kata ya Lahoda ndio kata maarufu sana kwa uzalishaji wa ufuta na alizeti kwa Kanda ya Mashariki, lakini

barabara yao ya kutoka Ilasee, Lahoda hadi Handa na kuunganisha na Singida ni mbovu sana. Naomba kujua nini mkakati wa Serikali wa kuboresha barabara hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Jimbo la Chemba na nimhakikishie kwamba Serikali imeweka mkakati mzuri sana kuhakikisha maeneo yote yenye mazao ya kimkakati kama alizeti, ufuta na kata ambazo amezitaja, kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara zile zinajengwa vizuri zinapitika vizuri ili wananchi waweze kusafirisha vizuri mazao yao. Kwa hiyo nitoe maelekezo kwa Meneja wa *TARURA* Chemba, wafanye tathmini ya bajeti iliyopo na kuweka kipaumbele kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa kama haya ili barabara ziweze kupitika vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus nimekuona.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya swali la nyongeza. Barabara ya Chombe, Kaoze ni barabara muhimu sana na mvua za mwaka jana zilipelekea uharibifu mkubwa na ombi maalum lipo tayari Wizarani. Nataka kujua je, ni lini Serikali itaijenga barabara hii ya Chombe, Kaoze ambayo ni muhimu kwa uchumi wa Kata ya Kaoze?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kufuatia mvua barabara zetu nyingi zimeathirika na Serikali imefanya tathmini, lakini wataalam wote Mameneja wa Mikoa na Halmashauri wameelekezwa kuleta maandiko maalum ya mapendekezo, lakini na gharama ya utengenezaji wa barabara hizo. Niwapongeze halmashauri hii wameshaleta andiko hilo, tunalifanyia kazi na mapema iwezekanavyo tutaona uwezekano wa kwenda kufanya matengenezo ili barabara ipitike vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Dkt. Pallangyo, nimekuona.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Changamoto za barabara Arumeru Mashariki zinasababishwa na hali ya kijiografia ambayo sio rafiki wananchi wengi wako milimani. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizi kwa kiwango cha lami au kwa teknolojia nyingine yoyote ambayo itafanya barabara hizi zihimili mafuriko wakati wa mvua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Pallangyo kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa Jimbo la Arumeru Mashariki. Pia nimhakikishie kwamba tunafahamu na tumefanya tathmini ya barabara ambazo ziko milimani katika Jimbo la Arumeru Mashariki na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* tumeweka mpango kazi wa kutenga fedha kulingana na uhitaji. Kuna maeneo yenye milima yenye mvua nyingi na changamoto kadhaa. Kwa hiyo bajeti zetu sasa pamoja na vigezo vingine itazingatia sana hali ya hewa, lakini pia na uhitaji mkubwa wa barabara hizo. Kwa hiyo nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tunalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Festo Dugange kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 219

**Mradi wa *Climate Change* – Chamriho**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa *Climate Change* utawafikia wananchi wa Tarafa ya Chamriho wanaokabiliwa na tatizo la ukame?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* linasimamia utekelezaji wa Mradi uitwao *Bunda Climate Resilience and Adaptation Project* wenye kiasi cha dola za Kimarekani 1,400,000 unaofadhiliwa na *Adaptation Fund*. Mradi huo unatekelezwa Wilayani Bunda katika maeneo ya Kata za Kasuguti, Namhura, Iramba, Neruma, Mahyolo, Igundu na Butimba. Kwa mujibu wa andiko lililoidhinishwa, Tarafa ya Chamriho kwa sasa iko nje ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutafuta fursa mbalimbali za miradi ya Mazingira kwa kushirikiana na Halmashauri ya Bunda ili kukabiliana na changamoto iliyopo katika Tarafa ya Chamriho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa kata zote zilizotajwa hapo saba hazipo hata kata moja ambayo ipo kwenye Tarafa ya Chamriho; na kwa kuwa Tarafa ya Chamriho ina kata ya Nyamanguta, Nyamswa, Kitale, Salama, Bihingo, Mgeta na Unyali. Sasa ni lini Serikali itapeleka mradi huu ambao uko Bunda kwenye hizo kata alizotaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa mradi huu unaelimisha watu juu ya madhara ya *climatic change* Serikali ina mkakati gani sasa wa kupeleka semina mbalimbali

na warsha katika maeneo haya ili kuelimisha watu juu ya tabia nchi inayotokea kwenye maeneo haya?

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi ukiangalia kwenye *paragraph* ya pili imeonesha kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, tunaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kwamba tunakaa na wadau na wafadhili mbalimbali ili kuweza kupata fedha twende tukaendeleze mradi huo katika hiyo Tarafa ya Chamriho. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na Subira, lakini pia kama kuna namna ya kufanya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda watuandikie hilo andiko walilete kwetu Ofisi ya Makamu wa Rais, twende tukalipeleke kwa ajili ya kuliombea fedha ili tukakamilishe mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, miongoni mwa kazi yetu kubwa tunayoifanya katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuhifadhi mazingira ni kuchimba visima maeneo mbalimbali ili kunusuru hali hiyo. Kwa hiyo nimwambie tu kwamba tunakwenda kutafuta fedha ili twende tukachimbe visima ili kuweza angalau kuokoa maeneo hayo huku tukisubiria mradi huo uweze kukamilika. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, una nyongeza? Karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwanza naomba nipongeze majibu mazuri sana ya Naibu Waziri. Hata hivyo, kwa heshima ya Mheshimiwa Boniphace Getere na nikifahamu kwamba ameendelea kuwapambania wananchi wake kwa nguvu kubwa sana. Ofisi yetu itafanya kila liwezekanalo mwanzoni mwa mwaka wa fedha katika eneo hilo tutatengeneza *borehole* moja ya mfano kama kuwafariji wananchi wa Kata ya Chamriho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sambamba na maelekezo yaliyotolewa na Naibu Waziri katika majibu ya awali. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Getere kwamba, tutakwenda kuchimba *borehole* ya haraka sana katika Kata ya Chamriho. Lengo letu ni kuanzia hapo kwanza wakati tukijadili mambo mengine, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Suleiman Jaffo. Nilimwona Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kisiwa cha Mtambwe Mkuu kilichopo katika Jimbo la Mtambwe, Pemba ni kisiwa ambacho kimeathirika sana na tabianchi, maji ya bahari yanaathiri sana makazi ya wananchi wasiopungua 500. Je, ni lini mradi huu wa *climate change* utawafikia watu wa Mtambwe Mkuu ili kunusuru kaya zao?

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumeona hizo athari za kimazingira ambazo zimetokezea katika Kisiwa hicho cha

Mtambwe Mkuu, lakini nimwambie kwamba aendelee kuwa na Subira, tupo kwenye michakato kuhakikisha kwamba maeneo yote ya visiwa ambayo yameathirika kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu, tunaendelea kutengeneza mazingira ili angalau visiwa hivyo viweze kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nitoe wito, visiwa hivi vinakuwa vinapata athari za kimazingira kutokana na shughuli za kibinadamu, watu wanakata miti hasa mikoko, watu wanafanya shughuli za ujenzi lakini na mambo mengine. Kwa hiyo pamoja na kwamba Serikali tunaenda kufanya juhudi ya kukiokoa na kukinusuru kisiwa hiki lakini kwa ushirikiano wa Wabunge na viongozi wengine wa Serikali, tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu ili sasa waone namna na umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwenye maeneo haya hasa maeneo ya visiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamza Khamis, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 220

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Miradi ya Umeme – Mbeya**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Wilaya ya Mbeya waliopisha mradi wa njia kuu ya kusafirisha umeme mkubwa wa Kilovolti 400 watalipwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa wenye msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 616. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme vya Iringa, Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga pamoja na ujenzi wa kilomita nne za njia ya umeme msongo wa kilovoti 400 kwenda kwenye mpaka wa Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini unafanywa na *TANESCO* kwa kushirikiana na Wathamini wateule wa Wilaya za Iringa, Mufindi, Mafinga, Mbarali, Mbeya, Jiji la Mbeya, Mbozi, Tunduma, Momba na Sumbawanga ambapo katika maeneo hayo mradi unapita. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022, majedwali ya fidia ya Halmashauri za Iringa, Mufindi, Mafinga, Momba na Mbarali tayari yameshaidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali na kukabidhiwa *TANESCO* kwa ajili ya kuanza maandalizi ya malipo. Majedwali ya Wilaya za Mbeya, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mbozi, Tunduma na Sumbawanga yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Fidia hizi zinatarajia kuanza kulipwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali na yanatia matumaini kwa wananchi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; mradi huu ulitegemewa kuwapatia umeme wa vijiji wanaopitiwa na mradi huu ikiwemo Vijiji vya Wambishe, Ihango katika Kata ya Ulenje na Vijiji vya Rusungomina katika Kata ya Iwindi na Bonde la Songwe ambako kuna viwanda vikubwa sana vinavyohitaji umeme mkubwa kwa ajili ya kuchakata madini. Sasa je, ni lini hawa wananchi watapatiwa umeme kwa mradi mbadala baada ya kuona huu mradi unasuasua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, vilevile mradi wa *REA III,* awamu ya pili na mradi wa *Densification* umechelewa kwa kiasi kikubwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru hii miradi miwili ambayo ukiangalia mradi wa *densification* umepitwa na wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa kuendelea kufatilia mradi huu mkubwa tunaouita *TAZA* wa kupeleka umeme mkubwa katika maeneo hayo. Nimhakikishie tu kwa kauli ya Serikali kwamba mradi huu hausuisui, lakini ni taratibu za kimanunuzi zinazofanya mradi uonekane unachukua muda. Hata hivyo, kama tulivyosema kwenye jibu la msingi tayari taratibu za kufanya fidia zimekaribia kukamilika na kwenye mwaka wa fedha ujao

tunatarajia kuanza kufanya fidia. Tayari wafadhili wameshapatikana na fedha ipo na ni taratibu za kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa mradi zinazoendelea na zitakapokamilika mradi utaanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kwamba tayari vijiji hivyo alivyovitaja katika maeneo hayo viko katika program ya kupewa umeme na mradi huu. Tunayo program inayoitwa *Land End Connection* ambayo tunawaunganisha watu kwenye maeneo ya miradi mikubwa inapopita kama ambavyo wale wenzetu wanaopitiwa na mradi unaotoka Iringa kupita Dodoma, kupita Arusha kwenda Namanga walivyoona tukifanya kwenye maeneo hayo na huku pia tutafanya hivyo hivyo. Kwa hiyo niwaombe tu wananchi wa maeneo hayo wawe na matumaini na Serikali itawapelekea umeme katika maeneo yao baada ya kukamilisha taratibu za mradi ambao unatarajiwa kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, kuhusiana na *REA* ni kweli *REA* kama alivyosema siku chache zilizopita Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali tulipata changamoto ya mabadiliko ya bei, lakini suala hilo tumelichukua kwa uzito wake kwa kukaa na wakandarasi na kukubaliana bei mpya zenye uhalisia kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hayo, miradi hiyo katika maeneo mbalimbali inaendelea kwa hatua mbalimbali ya uthamini wa maeneo, ya kusimika nguzo, ya kuvuta nyaya kwa wale ambao walishapata vifaa hivyo kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo niwaonye, kuwaasa, kuwaomba, kuwashawishi na kuwashauri wakandarasi wote waendelee na utekeleaji wa miradi hii kwenye maeneo yao kwa sababu mikataba yetu ipo pale pale ili kuweza kufikisha azma yetu ya kukamilisha vijiji vyote vilivyobakia kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Nishati. Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 221

**Mkataba wa Kampuni ya Songas na Serikali**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuingia mikataba mipya isiyo na dosari kwani Mwaka 2024 ndio mwisho wa mkataba wa Songas?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya Songas utaisha muda wake mwezi Julai, 2024. Ili kuhakikisha kwamba Serikali inakuwa na mkataba usiokuwa na dosari, Serikali haitaongeza muda wa mkataba utakaoishia mwezi Julai, 2024. Badada yake, Serikali itajadili mkataba mpya na iwapo pande zote zitakubaliana, mkataba mpya wenye tija kwa Taifa na usiokuwa na dosari utasainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali kupitia *TANESCO* imeunda timu ya kupitia masuala ya msingi ya kuzingatiwa kwenye mkataba mpya kwa ajili ya maslahi kwa Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa kwa dhati ya moyo wangu napenda

kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa nia yake ya kutaka kusitisha Mkataba huu mwaka 2024 ni jambo ambali nimelipigia kelele kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya nyenzo muhimu sana na mahsusi kwa ajili ya kusaidia kutoingia mikataba ambayo haina tija katika Taifa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Tanzania ya *Extractive Industry* ya mwaka 2015 inayotaka mikataba yote ya sekta ya uzidiwaji kuwekwa wazi. Nataka kujua ni kwa nini kumekuwa kuna kusuasua kwa Sheria hii kutekelezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya Songas ulioingiwa mwaka 2004 ni mkataba ambao unanyima fursa ya nchi ya Tanzania kunufaika na rasilimali kikamilifu. Nataka kujua Serikali imejipangaje mwaka 2024 kwenye mkataba mpya kuhakikisha kwamba hawafanyi makosa yaleyale kwenye eneo *ya Investment cost, shareholding structure agreements* na pamoja na eneo la *capacity charges*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jesca Kishoa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapokea pongezi alizozitoa kwa Serikali kwa jitihada ambazo zinafanyika pia ninamshukuru kwa kuuliza maswali ya msingi kabisa yenye ufuatiliaji na tija kwa watu wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali la pili kwamba Serikali imejipangaje. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari imeshaundwa timu ya kuanza kupitia mkataba uliopo

sasa na kubaini ni wapi tuliteleza na kutibu hayo maeneo ambayo tuliteleza ili yasijitokeze tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu zipo nyingi, ipo timu iliyoundwa na *TANESCO* inaendelea na upitiaji, ipo timu iliyoundwa na Wizara inaendelea na upitiaji, ipo timu iliyoundwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na upitiaji. Kama tulivyosema kwenye swali la msingi mkataba unaisha Julai, 2024 na hii ni Mei, 2022, kwa hiyo tuna miaka miwili kufikia muda wenyewe wa kuisha kwa mkataba. Tunayo imani kwamba tutakuwa tumeshajipanga vizuri na kuona ni kitu gani tutakifanya kuhakikisha kwamba mikataba tutakayoingia itatupa tija sisi kama Taifa na kuhakikisha kwamba nia na azma ya kupeleka umeme kwa wananchi inafikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la kwanza la msingi la kwamba uwazi unakuwa *guaranteed* kiasi gani na Serikali. Niseme kama alivyosema kwenye Sheria ya *Transparent Initiative* ya *Extractive Industry* na umoja tuliokuwa taasisi tuliyokuwa nayo ya *TEIT* ambayo inasimamia uwazi na uwajibikaji katika mikataba hii, imekuwa ni shughuli inayoendelea nasi tunaji-*subject* kule kuweka mambo yetu wazi, kuonyesha wachimbaji au wadau katika eneo hilo wamekusanya pesa kiasi gani, wamepata faida kiasi gani, wamelipa kodi kiasi gani, tunaweka wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia Bunge hili Kamati za Kudumu za Bunge zimekuwa zikiitisha mikataba hii, zimekuwa ziikitisha *value for money areas*, zimekuwa zikiitisha Wizara na maeneo mbalimbali kwenda kueleza kwao na kujua namna gani haya mambo yako wazi. Kupitia Bunge hili tunaamini wananchi wote sasa wanakuwa tayari kuona kwamba Serikali inafanya kitu gani kwa uwazi na uwajibikaji kupitia sisi Wabunge ambao tunakuwa kwenye Kamati mbalimbali. Kwa hiyo, niseme hata yeye Mheshimiwa Mbunge yuko na uhuru

kupitia kwenye Kamati kuweza kupata taarifa mbalimbali zilizopo katika maeneo hayo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya swali fupi la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Serikali iko tayari kupitia mkataba tu ambao ameusema Mheshimiwa Jesca Kishoa. Lakini Wizara yenu ina changamoto nyingi tu ya mikataba mbalimbali ambayo inahusaina na umeme na inailetea hasara Taifa hili, ikiwepo ule wa Pangea na Mgodi wa Geita na maeneo mengine. Hamuoni kwamba kuna haja sasa kama Serikali kupitia mikataba yote ili kuona tumekosea wapi huko tunakoenda nchi yetu isipate hasara na iweze kurekebisha sasa hivi, ukiwepo na mkataba wa Bwawa la Mwalimu Nyerere? Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo na maoni yaliyotolewa kwa niaba ya Serikali niseme ninayachukua, tutaendelea kushirikiana Serikalini kwa ajili ya kushauriana namna bora ya kuweza kuwa tunafikia mikataba yenye tija kwa watu wote. Ile ambayo itakuwa imekwisha tutahakikisha tunafanya vizuri zaidi kwa nyakati zilizopo na ambayo inaendelea tutaona namna bora zaidi ya kuifanya iwe na tija kwa watu wote.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Byabato kwa majibu hayo. Tunaendelea sasa na Wizara ya

Mambo ya Nchi Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 222

**Hitaji la gari Kituo cha Polisi Muhange-Kakonko**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari Kituo cha Polisi Muhange Wilayani Kakonko?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mahitaji makubwa ya kibajeti, kwa sasa Serikali haitaweza kuvipatia vituo vyote vidogo vya polisi magari. Hivyo, kituo kidogo cha Polisi cha Muhange ambacho kipo Wilaya ya Kakonko kitaendelea kuhudumiwa na Kituo cha Polisi cha Wilaya ambacho kina magari mawili namba PT 1983 na PT 3631 *Toyota Land Cruiser* kama inavyofanyika kwa vituo vingine vidogo vilivyoko Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kituo cha Muhange kipo mahali ambapo lipo soko la Ujirani Mwema na mara nyingi hutokea uhalifu na kutokana na ukosefu wa gari, Maaskari wa eneo hilo hulazimika kuazima pikipiki kwa Diwani wa eneo hilo. Ni lini sasa Serikali itapeleka japo pikipiki kwenye Kituo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kituo cha Kitanga katika Wilaya ya Kasulu kiko mpakani, eneo hilo linatenganishwa na Mto Malagalasi, ukitoka Kitanga kwenda Malagalasi unavuka Mto Malagalasi. Kwa hiyo naangalia ni jinsi gani kuna umuhimu wa kupeleka gari katika eneo hilo, na eneo hilo, kutoka Kitanga kwenda Kasulu Mjini ni kilomita 150, katika eneo hilo hutokea ujambazi mara nyingi.

Ni lini sasa kwa umuhimu wa eneo hilo Serikali itapeleka gari ili kunusuru maisha ya wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Genzabuke kwa kufuatilia kwa karibu sana masuala ya usalama katika Mkoa wa Kigoma na hususani katika hizo Wilaya alizozirejea Kankonko na Kasulu. Hata hivyo nimjibu tu kwamba tumpongeze Mheshimiwa Diwani kama moja ya wadau aliyetoa vyombo vya usafiri kama pikipiki na kama ambavyo Mkurugenzi wa Wilaya ya Kankonko pia ameahidi kutoa pikipiki ili kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa kwamba Wizara kupitia Jeshi la Polisi itapata magari zaidi ya 300 ifikapo mwezi Septemba na maeneo yenye changamoto kubwa za

kiusalama kama haya ya mipakani yatapewa kipaumbele. Kwa hiyo nimuondoe shaka Mheshimiwa Genzabuke. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Azan nimekuona.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba ina vituo Vinne vya Polisi ambavyo vina gari moja ambalo lilipatikana mwaka 1980. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea gari nyingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu wakati najibu swali la msingi kwamba tunao mpango wa kuimarisha usafiri kwenye maeneo yote ambayo yana changamoto ya usafiri ikiwemo Mkoa wa Kusini Pemba. Kwa hiyo, kulingana na vipaumbele na mahitaji ya magari, magari tutakayoyapata mapema iwezekanavyo yale 78 Mkoa wa Kusini Pemba pia utazingatiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim nimekuona.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Msalala, Halmashauri ya Msalala ina Kituo cha Wilaya na haina gari la Polisi. Kama unavyofahamu kwenye maeneo yetu ya uchimbaji usalama ni hatari sana ukizingatia kwamba kwa sasa kumeanza

kuibuka makundi mbalimbali. Sasa ni lini Serikali itachukua hatua za dharura wakati ikisubiria mpango wa kuleta magari yale mengine, ichukue hatua ya dharura ili kuhakikisha kwamba wanatupatia gari la Polisi tuweze kukabiliana na uhalifu katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua ni kweli kwamba maeneo ya migodi ni maeneo yanayovutia pia matendo ya uhalifu. Kwa hiyo tutakaa na Mheshimiwa Mbunge ili tukae na *RPC* wa Mkoa wa Shinyanga kuona kama pana magari ya ziada basi sehemu ya magari yale yahamishiwe kwenye Wilaya hii ya Kahama ili kuimarisha usafiri kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, maswali ni mengi kweli kama utaridhia Wabunge waje wakufuate wakuulize ili Majimboni mwao wakae salama, tunashukuru. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma Mbunge wa Muheza sasa aulize swali lake.

Na. 223

**Kukamilika kwa miundombinu ya maji – Muheza**

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha matengenezo ya miundombinu ya usambazaji maji katika kata sita za Muheza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma Mbunge wa Jimbo la Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka 2021/2022 inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji katika kata sita za Muheza ambazo ni Mbaramo, Genge, Masuguru, Tanganyika, Majengo na Kwemkabala. Ukarabati huo unahusisha kazi ya kubadilisha bomba kuu lenye urefu wa kilomita Mbili na ukarabati wa bomba la usambazaji maji lenye urefu wa kilomita 14.5. Kazi hii itakamilika mwezi Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imepanga kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika Kata Sita za Mji wa Muheza ikiwa ni pamoja na kusambaza maji katika maeneo ambapo mtandao wa usambazaji maji haujafika kwenye Kata hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamis Mohamed swali la nyongeza.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nashukuru kwa majibu mazuri na ya kutia moyo ya Serikali hasa kuhusiana na bomba la kilomita 14.5 na tarehe yake ya kukamilika. Hili ni moja ya matatizo tu nataka kupata *commitment* ya Serikali kuhusiana na tarehe ya kukamilika kwa mfumo mzima wa usambazaji ukiachilia mbali kilomita 14.5? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama muda utaruhusu naomba kuambatana na aidha Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri kwenda Muheza ili jibu atakalonipa kwenye swali langu la nyongeza akawape wananchi wa Muheza pamoja na kujionea mwenyewe jinsi miundombinu

ya usambazaji wa maji Wilayani Muheza kwenye Kata hizi za Mbaramo, Genge, Masuguru, Tanganyika, Majengo na Kwemkabala vilivyokuwa hoi, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukupongeza sana Mheshimiwa Mbunge jitihada zako za kuweza kushirikiana na Wizara zinafahamika, *commitment* ya Wizara ni kuhakikisha muda ambao usanifu unataka mradi kukamilika tutajitahidi kufanya hivyo hizi kilomita 14.5 kuhakikisha zinakamilika na maji yatoke bombani, wananchi waweze kufurahia fedha ambayo Mheshimiwa Rais ametaka iwafikie. Lengo ni kuwatua akina Mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuambatana ni moja ya taratibu zote mara baada ya Vikao vya Bunge aidha mimi ama Waziri ukinihitaji mimi hakuna neno tutakwenda tukafanye kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati nimekuona.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, katika Mji wa Ilula uliyoko katika Wilaya ya Kilolo unao mradi ambao umeshakamilika kwa muda mrefu lakini changamoto kubwa ni usambazaji wa maji katika vitongoji vyote.

Je, lini Serikali au katika bajeti hii itatoa pesa ili maji yaweze kusambazwa katika Mji wa Ilula?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi Mheshimiwa Kabati ni mfuatiliaji mzuri sana wa miradi ya maji kukamilika. Suala la mradi ambao tayari umekamilika usambazaji unafuata hiyo ndiyo hasa Wizara inashughulika nayo. Sisi tunapenda kusema mradi umekamilika pale maji yanapotoka bombani mwananchi ananufaika. Hivyo kwa mradi kama huu ambao umekamilika usambazaji ndiyo hatua inayofuata kwa mwaka ujao wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Maryprisca kwa majibu hayo na Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali kwa leo umeishia hapo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa matangazo nitaanza na matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii; kwanza kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, ambaye wa kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Anthony Mavunde Naibu wa Kilimo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *Chabuma Amcos* shamba la zabibu lililopo Chinangali Jijini Dodoma ambaye ni Ndugu David Mwaka, hayupo naona.

Wageni wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Subira Mgalu ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Mariam Fundi, hawa wapo karibuni sana Ndugu zetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ambaye ni Askofu wa Kanisa la TCOM Tanzania kutoka Mkoani Geita ambaye ni Askofu Eliud Chrisant, karibu sana Askofu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Catherine Magige kutoka *Dar es Salaam Commercial Bank*, ambao ni Ndugu Fransisca Francis na Ndugu Dalila Issa, karibu sana wageni wetu wa Mheshimiwa Catherine. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 57 wa Mheshimiwa Joseph Mhagama ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jesca Kishoa ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Singida ambao ni Ndugu Winfrida Kishoa ambae ni mama mzazi karibu, Ndugu Happiness Kishoa ni dada yake pia kuna Ndugu Pasaka Mkenda ambae ni kaka yake, karibuni sana wanafamilia wa Mheshimiwa Kishoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Ufuatiliaji wa Bwawa la Mkomazi kutoka Korogwe Vijijini Mkoani Tanga, wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Mnzava ambao pia ni viongozi wa Halmashauri ya Korogwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Sadick Kalaghe, karibu sana wageni wetu kutoka huko Korogwe. *(Makofi)*

Pia tunao wageni sita wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambao ni walimu kutoka Ushetu na Kahama Mkoani Shinyanga, wakiongozwa na Mwalimu Victor Tandise, karibu sana wageni wetu kutoka huko Kahama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo hao ni wageni 60 kutoka *Tanzania Muslim Students and Youth Association* Tawi la Morogoro, karibuni sana wanafunzi kutoka huko kwa ajili ya mafunzo Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 140 na walimu kumi kutoka Shule ya Sekondari Lukundo kutoka Jijini Dodoma, ooh, wanafunzi wako huku hawa, karibu sana wanafunzi kwa ajili ya mafunzo pamoja na walimu nawaona wapo pale, karibu sana kwa ajili ya mafunzo katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo pia kuna tangazo nimeombwa niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa leo tarehe 18 Mei kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote kuhusu masuala ya bima yatakayotolewa na Shirika la Bima la Taifa na masuala ya Diplomasia na Itifaki itakayotolewa na Chuo cha Diplomasia. Semina hii itaanza saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnasisitizwa kuhudhuria semina hiyo muhimu sana.

Katibu tuendelee.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwa Wizara ya Kilimo.

Tunaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa wajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika eneo hili la kilimo pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Anthony Mavunde. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na nzuri sana ambayo imeanza kuonekana. Tunataka kuona sasa kazi hii itoke kwenye zile suti ambazo wameziandaa ielekee kwenye vitendo na uhalisia zaidi ili mwisho wa siku tusifanye tathmini kwa mavazi, bali kwa tija ambayo itaonekana kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaulekeza katika zao la kimkakati la kahawa. Mkoa wa Tanga ni miongoni mwa mikoa takribani 15 ya nchi yetu ambayo inalima kahawa na hususan katika milima ya Usambara kwa maana ya Wilaya za Muheza, Korogwe pamoja na Lushoto. Zao hili kwa muda mrefu Serikali imekuwa haitoi motisha kwa wakulima kiasi kwamba zao hili sasa linakwenda kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka, hata jana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela alikuwa anaongelea zao la tangawizi, na hali ya hewa ya Same na Lushoto zinafanana kwa asilimia kubwa, lakini watu wamehama kutoka kilimo cha kahawa kwenda kilimo cha tangawizi kwa sababu ya changamoto mbalimbali zikiwemo huduma hafifu za ugani, uchakavu au umri mkubwa wa mibuna, upatikanaji wa pembejeo; madawa na mbolea na matumizi ya mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye mbegu bora ndiko ambako nataka niweke msisitizo. Ni kwamba Bodi ya Kahawa *(TCB)* ifanye kazi ya ziada kuhakikisha kwamba kunakuwa na miche mingi ya kahawa hasa katika mikoa hii ambayo nimeitaja hapo awali. Mkoa wa Kagera ndiyo unaoongoza kwa uzalishaji wa kahawa hapa nchini ambapo wanazalisha takribani kwa mwaka tani za kutosha tu, ambazo kwa ujumla wa tani zote nchi nzima, wao wanachangia asilimia 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa unaofuata ni Mkoa wa Mbeya, Kigoma na Songwe nako kahawa inazalishwa. Yapo maeneo ambayo wanazalisha kwenye baadhi ya wilaya ikiwemo Ruvuma ambako ni Mbinga pamoja na Nyasa, pia Mkoa wa Arusha, Mara, Njombe, Iringa, Manyara, Katavi, Morogoro na Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo langu hapa ni kuishauri Serikali kwamba sasa tuweke ruzuku katika zao hili la kahawa. Tunaona kabisa kwamba zao la kahawa kwa ripoti za mwaka 2021 tumeuza nje takribani dola milioni 142. Ni kiasi kikubwa sana ukilinganisha na pesa ambayo tumeuza kwenye tumbaku ambapo tumbaku ina ruzuku, lakini kahawa haina ruzuku. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba tukiongeza uzalishaji katika kahawa, hata hili pato litaongezeka kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetazama hapa kwenye takwimu, nchi ya Ethiopia ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa kahawa, inazalisha takribani tani 457,000. Yenyewe tangu mwaka 1959 mpaka tunavyozungumza sasa, haijawahi kupunguza uzalishaji. Kadri mwaka unavyoongezeka ndivyo na uzalishaji unavyoongezeka, maana yake wao walilichukuwa hili kama ni zao mahususi, zao la kimkakati ambalo linaibeba nchi ya Ethiopia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla nawaomba sana kwamba pamoja na mazao mengine yote ya kimkakati tunayoyajadili, tuweke nguvu ya ziada katika zao hili la kahawa ambalo sasa linaelekea kupotea. Matarajio yetu ni kuzalisha wastani wa tani laki moja kwa mwaka, lakini mpaka sasa hivi tumefika tani 68,000 tu. Hizi ni chache sana kwa ukubwa wa nchi yetu ukilinganisha na nchi jirani ambazo kahawa inalimwa lakini siyo kwa ardhi kubwa kama ambayo tunayo hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa, tofauti na mazao mengine ya kimkakati, ukishapanda una uwezo wa kukaa miaka 30 mpaka 40 kutegemea na aina ya kahawa. Kwa mfano, Arabika, kubadilisha mti uliochoka unahitaji miaka 50 mpaka miaka 60. Hata hii ambayo sasa hivi tunaendelea kuvuna huko, ni kahawa ambayo imeanza kulimwa na wakoloni na baadaye ikalimwa na babu zetu. Sasa sisi kama kizaki kipya tunatakiwa tupeleke mbegu, tuanzishe vitalu vya miche ya kahawa katika maeneo yote niliyoyataja ili sasa tuongeze uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya Robusta, mche unaweza kukaa hadi miaka 40, ndiyo unakwenda kuzeeka kiasi cha kupunguza uzalishaji. Kwa hiyo, naomba sana katika eneo hili tufanye maboresho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la uzalishaji, nikitoa tu mfano wa eneo la uzalishaji wa kimkakati ambalo tumejifunza katika Wilaya ya Mbinga kule Ruvuma; kupitia ushirika wa *MBICUFARM* tumejifunza jambo kubwa sana. Kahawa yote tunaiona inakobolewa katika mashine ambazo ziko chini ya Vyama Vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, tukitaka kwenda kujifunza ushirika wa ukweli, ni vizuri tukaenda kujifunza kwenye Chama cha Matengo kule

ambacho sasa hivi kinaitwa *MBICUFARM*. Wanafanya kazi nzuri sana na tumeiona kahawa yote ikiwa kwenye maghala imehifadhiwa. Hapa ndipo tunapopata somo kwamba haya maghala na yenyewe tukiyawekea takwimu yanaweza yakasaidia hata kuvutia wateja kutoka nje kwa sababu watakuwa na uhakika kwamba akifika mahali fulani kwenye ghala namba fulani anaweza akapata tani za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana na nitoe rai kwamba tuige mifano mizuri ya wenzetu kama hawa ambao tumezikuta tani takribani 15,000 ziko kwenye maghala na tayari mnunuzi amepatikana kutoka nje ya nchi. Halmashauri haikamatani na wafanyabiashara kwenye mageti, hela yote inapatikana kupitia mfumo sahihi wa stakabadhi. Halmashauri inachukua mrabaha wake, Vyama Vya Ushirika vinachukuwa mrabaha, *AMCOS* zinachukua kilicho chao; na tumeona *AMCOS* zikitoa *CSR* hata kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *AMCOS* moja inaitwa Kimuli, imeweza kutoa makalavati kwa *TARURA* ili waweze kuboresha miundombinu ya barabara. Sasa hii ni dhana pekee unayoweza kuipata kupitia ushirika nje ya ushirika itakuwa ni kukimbizana na wachuuzi wadogo hawa ambao baadaye pia wanasaidia kutorosha mazao hata kwenda nje ya nchi na mwisho wa siku inaonekana *turnover* ya nchi ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ni hili ambalo limezungumzwa kuhusu leseni za maghala. Tumejifunza jambo kwenye maghala haya ya mafuta kwamba baada ya kupata mfumuko huu wa mtikisiko wa soko la mafuta duniani, kila wakati Wizara ya Nishati ilikuwa inatoa takwimu za mafuta yaliyoko katika maghala ya mafuta. Ningetamani kuona jambo hili nalo likitokea katika kila aina ya bidhaa ambayo tunayo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litawezekana tu kama tutakuwa na takwimu sahihi na ghala lilipo na linahifadhi kitu gani? Maana yake hapa tunachotafuta ni takwimu siyo jambo lingine. Mambo ya ubora na mambo mengine yatasimamiwa na idara zinazohusika, lakini angalau kujua kwamba nchi yetu ina sukari kiasi gani? Nchi yetu ina ngano kiasi gani? Nchi yetu ina mafuta ya kupikia kiasi gani? Hili linahitaji takwimu na sehemu sahihi ambayo tunaweza tukafanya hili, ni kupitia wakala wa maghala nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi. Kabla sijaendelea kuna wageni wengine nimeletewa hapa. Wageni wanne wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni wapigakura wake kutoka Tarime Mkoa wa Mara wakiongozwa na Ndugu Charles Mgana, wale kule wapo juu. Karibuni sana katika Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majina ya wachangiaji kuwa mengi asubuhi hii, kila mmoja atapata fursa ya dakika tano. Naomba sana kila mtu aende kwenye hoja ya msingi ambayo anaona ni muhimu kwake kuisema kabla ya nyingine zote. Dakika tano na italia kengele moja tu. Naomba tujikite kwenye *point* muhimu sana kwa sababu wachangiaji ni wengi sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Ditopile, halafu Mheshimiwa Tumaini Magesa na Mheshimiwa Daniel Sillo wajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika nchi yetu kwa kweli kilimo kinafanyika sana, na ndiyo maana kwenye takwimu za Serikali tunaelezwa kwamba kilimo ndiyo ambayo imeajiri asilimia kubwa ya

Watanzania. Cha kushangaza, miaka yote pamoja na jitihada kubwa za Serikali yetu, lakini mkulima anakutana na Serikali baada ya kuvuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilimo ni mfumo wa mambo yafuatayo: Kilimo ni utafiti na utaalam *(expertise),* kilimo ni sayansi teknolojia na mitambo, kilimo ni udongo ama ardhi, kilimo ni mbegu, kilimo ni maji kwa maana ya mvua ama umwagiliaji, kilimo ni urutubisho, kilimo ni madawa, kilimo ni miundombinu ya uvunaji, kilimo ni miundombinu ya uhifadhi na mwisho kabisa, kilimo ni soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mtitiriko ukikosea jambo moja tu, tayari umeshaondoa tija kwenye kilimo. Nasi kama Wabunge kila siku tunapiga makelele, tunataka kilimo cha nchi hii kiwe na tija. Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza nimeshuhudia tangu niwe Mbunge, hii ni bajeti ya kwanza haijawahi kuambiwa kwamba ni ndogo kwa kilimo. Kwa hiyo, nimpe pongezi Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ama hakika ameonyesha kwamba yeye ni mwanakilimo kwa vitendo; kwanza kwa kututeulia watu ambao wametupa matumaini, wanakuja kukivusha kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe alikuwa Naibu Waziri, meno yalikuwa madogo, sasa ana meno kama ya mamba ya kuja kuendeleza kilimo. Vile vile msaidizi wake Anthony Mavunde, ama hakika hii ni hazina yetu sisi Dodoma. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haleluya!

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Ni mtu ambaye kila unamweka lazima aoneshe vitendo. Kwa hiyo, mimi nawapa shime muende mkayafanye, lakini Mheshimiwa Waziri angalia sana watu wa chini. Ninyi viongozi mna *commitment,* lakini huku chini hasa kwa Maafisa Ugani, nendeni mkaweke

*mechanism* ya kuangalia utendaji wao, watakuja kuwaangusha. Kwa hiyo, lazima mwangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa mkulima kwa muda mrefu, na-*declare interest.* Naweza kuwa na shamba zaidi ya heka 1,000. Kwenye eneo husika sijawahi kuona hata siku moja Afisa Ugani akija hata kuomba mbegu tu niweze kuwapa wananchi wanaonizunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa watu tulioenda kuwapa vifaa, tumeona Rais wetu ameenda kweli sasa kuongeza utaalam, kawapa pikipiki, kawapa vifaa vya kupimia udongo, nendeni mkawasimamie ili wa-*translate* yale maono yenu. *Unless otherwise they are going to fail you.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza bajeti imepanda *45.7 billion,* hiyo ni hatua kubwa sana. Tumeonga mme-*involve* vijana. Niliwahi kushauri vijana lazima watengenezewe mazingira ya kushiriki kwenye kilimo. Naona sasa kwa mipango mliyokuwanayo, ama hakika kundi kubwa la vijana ambalo nimekuwa mtetezi wao siku zote, sasa wanaenda kushiriki kwenye kilimo kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya umwagiliaji, siku zote bajeti inaenda kwenye kujenga mabwawa, lakini mmeenda mbali, mmeenda kutoa mpaka vitendea kazi. Naomba tu mjifunze, kule *Egypt* wanatumia *River Nile* kulisha karibu robo ya dunia, lakini *River Nile source* yake ni *Lake Victoria.* Sisi tuna mto, mpaka ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage jana kaongelea *Ngono Project.* Hebu tuangalie hii mito tuliyokuwanayo; Kagera na Morogoro tunaitumiaje? Tusiende kuchimba mabwawa ya *irrigation scheme* wakati tuna mito ambayo miezi 12 ina-*flow* bila kukatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikienda kwenye mawazo yangu manne: Naomba tuanze sokoni. Leo hii uhaba wa

mafuta umekuja kugundulika kupitia viwanda na biashara, lakini *source* ya upungufu wa mafuta ni kwenye kilimo. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara m-*synchronize,* mkae chini, mpange kwa pamoja. Leo hii India, nchi ambayo inaongoza kwenye kilimo, mkulima haendi kulima mpaka viwanda na biashara viseme msimu tunaoenda, ni zao gani litakuwa na soko zuri? Wanashauri watu wa kilimo, nao wanaenda kuwaambia wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, nilienda kutafuta soko la *green beans.* Tukakuta kuna watu kutoka Malawi nao wameleta *green beans.* Yale ya Malawi yalikuwa na *size* moja, yana rangi imependeza, kwa kweli tulipigwa, ila basi tu kwa vile tunaipenda nchi yetu, tukayala. Hawa sijui wanaweka madawa, wanaweka nini, lakini kitu cha kwanza ni *appearance*. Kwa hiyo, naomba sana, watu wetu wa viwanda na biashara, shirikianeni na Wizara ya Kilimo ili tuanzie sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna kitu kinaitwa *agricultural zones.* Nimekuwa nikipigia kelele kila nikichangia. Hata kipindi cha Hayati Mwalimu Nyerere ilikuwa hivyo, ndiyo maana kusini walikuwa wanalima korosho; ukija Tanga kuna Mkonge. Zao humea sehemu yoyoye, lakini linamea kwa ubora? Kuna mwaka watu walileta mikorosho huku Dodoma, imeishia wapi hiyo mikorosho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mmeweka *clusters that is the way to go. We don't have enough resources.* Hatuna *resources* za kutosha, sasa utatawanya hizo *resources* zote? Bora ukiziweka sehemu moja zitaenda kufanya kazi kwa weledi na vizuri ili tuone matokeo na tija katika kilimo chetu tunachokifanya, lakini tusiache sayansi na teknolojia Mheshimiwa Waziri. Lazima tuende sawa na dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna kitu kinaitwa *genetic modified seeds,* tunazikataa kwa nini? Leo hii tunalima

pamba, tunataka tuzalishe nguo, lakini katika nchi kumi zinazozalisha pamba hatumo. Nchi zote kama Brazil, India, China wanatumia *GM Cotton Seeds.* Sisi tunachotaka, tuleteeni hizo teknolojia halafu mkulima mwenyewe aamue. Leo mnasema oh, sijui zina madhara, ni uongo mtupu. Hayo ma-*apple* tunayoingiza kutoka nje mbona mbegu ndiyo hizo hizo zinatumika!

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji kwamba suala la *GMO* ni tofauti anavyotaka kulichukulia. Kile ni kifo unachokula mwenyewe ukiona. Siyo sumu, ni kifo unachokula unakiona. Kwa hiyo, suala la *GMO* lina utata mkubwa na ni jambo siyo katika nchi yetu kuanza kulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Ditopile, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa. Hata simu zilipoanza walituambi oh, mionzi, hamtazaa. Simu tunatumia mpaka leo na zinarahisisha kazi zetu. Tusiogope sayansi. Leo hii kuna watu wanapata mimba bila hata kuingiliwa, wanapandikiza. Hiyo ndiyo sayansi, usibishane na sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri, kusema ukweli mmefanya jitihada kubwa kupunguza riba za kwenye mikopo, lakini niseme ukweli, mkulima hakopesheki. Leo hii mimi ni mkulima lakini vilevile nina kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti. Nilienda kuomba mkopo Benki ya *NMB,*

walikuja pale kwenye ghala langu wakakuta nina dumu za mafuta za lita 20 zaidi ya 2,000, nina *stock* ya kutosha, lakini walishindwa kunipa mkopo wakiniambia kwamba nyumba yangu moja hapa Dodoma Mjini ndiyo niiweke dhamana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam, malizia *point* yako kengele imeshagonga.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake umeisha, anamalizia *point* yake ya mwisho.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi mengine nitaenda kuyachangia kwa maandishi. Niwape moyo, niwatie nguvu, kwa kweli tunaenda kwenye *the right direction.* Mimi kama mkulima na Mbunge wa muda mrefu ambaye nimekuwa nalia na kilimo, sasa tunasema dalili ya mvua ni mawingu, mawingu tumeyaona na sasa tunaona zile rasharasha. Naamini mvua kubwa inakuja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana, ambaye ameguswa na mchango, taarifa iwe fupi sana ili tumpe fursa mchangiaji aweze kutoa hoja zake.

Tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Masega, Mheshimiwa Daniel Sillo na Mheshimiwa Riziki Lulida, wajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Japokuwa jina langu umesema Tumaini Masega, naitwa Tumaini Magessa. Naomba tu nirekebishe hilo.

**MWENYEKITI:** Samahani, ni Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Yah!

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa nafasi, hii lakini naomba niseme mambo machache sana kwa sababu ya muda. Pamoja na mambo mengine, uhitaji wa sekta za uzalishaji ikiwemo sekta hii ya kilimo kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, ni muhimu sana. Kwanza ni kwa sababu asilimia 65 ya Watanzania wameajiriwa na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kwamba tukipata ukuaji mzuri kutoka kwenye hii sekta ya uzalishaji tutaajiri watu wengi; pili, uchumi wetu utakua; tatu, uwezo wa wananchi wetu kustahimili madhara ya mtikisiko wa uchumi wa kidunia ambao unakuja na *inflation* ambazo wananchi wanashindwa kuzistahimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa. Mwaka 2021 wakati naongea nilisema *Malabo Declaration* ilituhitaji tuchangie sekta hii kwa asilimia 10. Mwaka huu tumejitahidi; Mheshimiwa Rais amejitahidi, ni msikivu, ameongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 294 kwenda bilioni 751. Niseme wazi kwamba, hii ni hatua moja nzuri sana, lakini bado hatua hii tuliyokwenda nayo haitupeleki kwenye asilimia 10 tuliyoisema, bado tuko mbali kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni 751 niseme wazi kwamba hili ni hatua moja nzuri sana lakini bado hatua hii tuliyokwenda nayo haitupeleki kwenye asilimia 10 tuliyoisema bado tupo mbali kidogo. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana timu yako. Hoja yetu nataka tuhakikishe kwamba hii sekta ya kilimo inapatiwa fedha ya kutosha ili ukuaji wa uchumi wetu badala yakuwa *single digit* uwe *double digit*. Sasa hivi tuna *single digit,* na unaona inaendelea inacheza inashuka ikicheza inapanda. Tusipowawezesha hawa wananchi wetu kutokana na sekta hizi za uzalishaji hatuwezi kutoka mahali tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme wazi, pamoja na pongezi hizi tumeona wazi kwamba kuna ongezeko kwenye utafiti, mahali ambapo tumewapigia kelele sana mwaka jana, kutoka bilioni 7.35 tumeenda bilioni 11.63, umwagiliaji kutoka bilioni 11.5 kwenda bilioni 17.7, lakini mbegu kutoka bilioni 3.42 kwenda bilioni 10.38, haya ndiyo yalikuwa matatizo yetu. Sasa tukiongeza pesa ya kutosha maana yake ongezeko katika maeneo haya niliyoyataja kila atayelima atalima kwenye udongo anaoujua una *characteristics* gani? Kila atakayelima atalima eneo ambao limewezeshwa skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi, kwenye umwagiliaji hapo bado kuna shida. Tumeona wazi kwamba ukilima mpunga kwenye skimu za umwagiliaji kutoka tani mbili unapata tani nne au tani tano na unaweza kulima mara mbili kwa mwaka. Sasa, je, skimu tunazo ngapi? Tumeona wazi kabisa kwamba hadi sasa katika hekta milioni 29 sisi lengo letu ilikuwa hekta milioni 1.2 lakini bado tumefikia 700 na kitu tu. Kwa hiyo, bado tupo mbali kidogo kwenye sekta hii ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kutoka kwangu jimboni kwangu. Sisi kwetu kwa upande wa huduma za ugani tuna maafisa ugani 27 na tuna kata 37. Maana yake ni

kwamba, kuna kata 10 ambazo hazina ushauri wowote wa kitaalamu. Nimuombe Mheshimiwa Waziri atupatie maafisa ugani watakaoweza kutoa huduma za kigani ambazo zitafanya wananchi wetu waweze kupata mapato yaliyobora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba mwaka jana kwamba tupate skimu za umwagiliaji, na tukaomba kwaajili ya maeneo ya Saraburwa, Magenge, Nyamaruru pamoja na Nyakagomba, lakini mpaka sasa jimbo langu ninalotoka mimi halina skimu hata moja. Kwa hiyo, haya yanayotajwa kama ndiyo faida za umwagiliaji kwangu kule bado ni ndogo kwasababu hakuna skimu hata moja. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho ahakikisha kwamba kuna skimu fulani inayopatikana jimboni Busanda ili watu wangu pamoja na kupata wakajifunze na waweze kupata uzalishaji huu ambao wenzetu maeneo mengine wanautegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza, pamoja na ongezeko hili bado asilimia 10 ya bajeti yetu iende kwenye kilimo ili tuweze kufanikiwa. Hii tulinayo, ukipiga hesabu utagundua ni *one out of six*. Kama tuna bilioni arobaini na kitu maana yake ni kwamba tulitegemea tupate trilioni nne. Kwamba kama tuna trilioni 41 tunategemea tupate trilioni ndani ya Sekta ya Uzalishaji, lakini ukipiga hesabu unaona hapa kuna bilioni 751 ukipiga ni *one out of six,* ambayo kimsingi ukifanya hesabu utagundua hii ni asilimia 16 mpaka 20. Naomba twende kwenye namba, namba hazisemi uongo. Tukienda vizuri naamini kwamba wananchi wetu wataweza kufanikiwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Magesa tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Sillo, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa George Mwenisongole, wajiandae.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwa kidogo kwenye Wizara hii ya Kilimo, Wizara muhimu sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayofanya, pia pamoja na kuondoa vikwazo vya kufanya biashara na nchi jirani, kufungua fursa za uwekezaji pamoja na *Royal Tour* ambayo itapanua sekta ya utalii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kaka yangu Bashe, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayofanya lakini pia kwa sura ya bajeti hii tunayoiona, ya kutoka bilioni 298.1 mpaka bilioni 751; ni mwanzo mzuri sana wa kuleta mapinduzi ya kilimo katika Taifa letu, tunawapongeza sana. Tuwaombe Wizara isimamie vizuri. Bajeti hii muhimu sana tunaamini kwamba itaongeza tija na faida kwa wakulima wetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo machache; eneo la kwanza ni eneo la umwagaliaji. Naipongeza Wizara, nimesoma bajeti hii imeongeza fedha kwaajili ya kuwekeza katika maeneo ya umwagiliaji. Sote ni mashahidi, kwamba kumekuwa na upungufu wa mvua kutokana na mabadiliko ya tabianchi kumekuwa na upungufu wa mvua. Kwa hiyo, ni vema kabisa wizara ikajielekeza kwenye umwagiliaji ili wananchi wetu waweze kufanya kilimo kwa msimu wa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza maeneo machache eneo la Babati Mjini kwenye jimbo langu kuna Kata za Madunga, Nar na Kameyu, pamoja na Ziwa ambalo halikauki maji katika msimu mzima wa mwaka lina maji ya kutosha niombe sana wizara ijielekeze iwasaidie sana watu wetu hawa waweze kujenga miundombinu ya umwagiliaji maana kuna kilimo kizuri sana cha vitunguu maji pamoja na vitunguu saumu. Naamini kabisa Wizara ikijielekeza huku wananchi wetu hawa watazalisha vya kutosha na kutosheleza soko letu la vitunguu na vitunguu saumu ambalo ni muhimu sana hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata za Magugu, Magara, Kiru pamoja na Kisangaji kuna bonde zuri sana la kilimo cha miwa na Kilimo cha Mpunga. Najua wengi mmepita eneo la Magugu, mkipita pale mnanunua mpunga, mchele mzuri sana. Kwa hiyo, niombe sana Wizara hii ya Kilimo; na ninajua Mheshimiwa Bashe ameshafika pale Magugu amejionea milimo cha miwa kwenye shamba pale la Manyara Sugar. Kwa hiyo niombe sana Wizara yetu ya Kilimo iwekeze miundombinu ya umwagiliaji ili tuweze kulima miwa ya kutosha na tuweze kuzalisha sukari kwa manufaa ya wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la umwagiliaji niombe sana Wizara ya Fedha iiwezeshe Benki ya Kilimo *(TADB)* ili iweze kukopesha wakulima wetu kwa riba nafuu; ninaamini sana hii italeta tija kubwa sana kwa wananchi wetu atafanya kilimo chao na kitawasaidia sana katika kuwainua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, enelo lingine ni eneo la masoko ya mazao. Kutokuwa na masoko ya uhakika ni changamoto kubwa kwa wakulima wetu. Mkulima anahangaika mwaka mzima anafikia kuvuna hajui pakuuza. Naomba sana wizara ifanye utafiti wa kutosha kuhakikisha kwamba wananchi wetu

wanapata masoko ya mazao yao hasa wavijijini ambao wanategemea kilimo kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata za Galapo, Qash, Ufana, Secheda, nakadhalika kuna wakulima wazuri sana wa mazao kama mahindi, dengu, maharage, mbaazi na mazao mengine lakini kuna tatizo kubwa la masoko. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iwasaidie wananchi wetu hawa wanaopambana mwaka mzima; wapatiwe masoko ili wajikwamue kiuchumi na kusaidia familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu eneo la upatikanaji wa pembejeo; naomba sana Wizara ya Kilimo iwasaidie wakulima wetu wapate pembejeo kwa wakati, kama mbegu bora na mbolea, ili waweze kufanya shughuli zao za kilimo na kurahisisha kilimo kufanyika kwa wakati; lakini pia kuna dawa za kuua wadudu. Kumekuwa na dawa nyingi sana kwenye maduka lakini haziui wadudu. Kwa hiyo, naomba sana kufanyike utafiti wa dawa bora ya kuua wadudu ili wakulima wetu waweze kuvuna mazao ambayo wanatarajia kuvuna katika msimu mzima wa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nikushukuru sana kwa fursa hii naninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Sillo. Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa George Mwenisongole na Mheshimiwa Aysharose Mattembe, wajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru nanimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametujalia kuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya hasa

katika kuongeza fedha na kuongeza bajeti hii ili kufanya kazi. Amejitahidi vya kutosha kuhakikisha maafisa ugani ambao kwa muda mrefu walikuwa hawaonekani na hawana vitendea kazi wameletewa vifaa vya kufanyia kazi pikipiki; sasa kilichobaki ni kuhakikisha tunawasimamia hawa maafisa ugani ili wafanyekazi ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa kuendelea katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe, ni kijana msikivu, mwenye kupenda hasa na ana imani kuwa anataka kuleta kilimo chenye maendeleo vilevile nimpongeze Mavunde, nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Bwana Tumbo ambaye huyu ni mtaalamu wa masuala ya vifaa vya kilimo alikuwa *CAMARTEC,* amekuja pale, naye ni mchango mkubwa katika maendeleo ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza kwa muda mchache sana kutokana na muda nilio nao, na nitakwenda kwenye dhima. Dhima ya kilimo ya kwanza ni kuandaa kilimo bora chenye mazingira bora, lakini vilevile kuwaandaa wakulima wapate tija katika kilimo hicho pamoja na kutengeneza mifumo ya kimasoko ambayo itawasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda nilio nao nitazungumzia Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Ni mikoa ambayo sasa hivi kama Serikali haisimamii itaonekana na mikoa ya kimasikini wakati ni mikoa tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kunatakiwa kuwepo na mifumo ili mifumo hii iweze kuitoa hii mikoa. Itakuwa ni aibu ukienda mikoa mingine inaonekana iko *busy* inafanya kazi, kuna viwanda kuna maendeleo; lakini Mkoa wa Lindi na Mtwara hatuna viwanda, bandari hazifanyi kazi, njia kuu zote za uchumi zikiwemo barabara ni mbovu sasa unategemea watu hawa watafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninazungumzia kutokea Songea mpaka Bandari ya Mtwara ina- kilometa 657 lakini kutoka Songea kwenda Dar es Salaam ni kilomita 948 lakini kutokana na urasimu wa bandari ya Mtwara ambayo Serikali hajijataka kuwekeza mizigo yote na nafaka na mazao yanakwenda katika bandari ya Dar es Salaam. Jiulizeni, Bandari ya Dar es Salaam kuna nini ilhali ukiangalia Bandari ya Dar es Salaam sasa hivi iko *busy* kiasi ambacho watu wanakaa na mizigo zaidi ya wiki nzima na urasimu huu unafanya kuingia katika corruption katika bandari ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri ashirikiane na Waziri wa Fedha na Waziri wa Ujenzi waje watupe taarifa kuna nini mpaka bandari ya Mtwara mapaka sasa hivi haifanyi kazi. Urasimu uliokuwepo katika bandari ya Mtwara mizigo yote inayotoka Lindi na Mtwara na Ruvuma inabidi iende Dar es Salaam, hivi jamani kweli tunapiga hesabu za kibiashara hapa? Inamaana hakuna biashara inayofanyika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ufuta unalimwa Kilwa barabara ya Liwale hakuna lakini ufuta ule ule unabidi uzunguke mpaka Lindi, Lindi mpaka Dar es Salaam ilhali Bandari ya Mtwara iko karibu. Hiki ni kitu ambacho mimi sielewi; ni kama ni *zig zag* ambalo naliona kabisa. Mimi nitataka nitachangia tena katika Wizara ya Fedha, watuambie Bandari ya Mtwara na Tanga zimekwama wapi? Mazao yote yanakwenda Dar es Salaam, tumeifanya Bandari ya Mtwara ikose kazi kwa ajili ya kupeleka mizigo yote Dar es Salaam. Wao wanatoa sababu za wafanyabiashara, lakini mimi hiyo wala haingii akilini. Kama kweli kuna mikopo inaweza kusaidia Bandari ya Mtwara wakaleta makasha mimi naomba Serikali isimame na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia biashara za korosho, Kawaha na biashara mbalimbali ambayo iko katika

mikoa hiyo, kwa kweli inasikitisha, inasikitisha kwasababu hawajatengenezewa mazingira rafiki, viwanda vyote vimefungwa. Hapa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitengeneza biashara kikanda na mazao kikanda. Mkoa wa Lindi ulikuwa ni mkoa wa kulima karanga, soya, ufuta, na kahawa; ndiyo ilikuwa mikoa hiyo. Lakini mikoa mingine ilikuwa imetengenezewa kama pamba, Mikoa ya Kanda ya Ziwa wanalima pamba.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agness nilikuwa nangoja Mheshimiwa Lulida nilikuwa nangoja amalizie sentensi yake dakika zake, kengele ishapigwa, kengele naombeni sana msiombe taarifa. Mheshimiwa Lulida malizia naomba.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mikoa ya Lindi sasa imetiwa umaskini kwa ajili ya mifumo mibovu ambayo haijataka kuwa rafiki wanawananchi wa Mikoa ya Lindi ikiwemo bandari na barabara, lakini vile vile mazao hayana soko, viwanda mmefunga unategemea watanda wapi? Leo unachukua korosho unaipeleka nje *as raw material*, korosho ile ile ukibangua mwenyewe unakuja kuuza Dodoma shilingi 25,000. Je, tutaondoaje umasikini kwa watu wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tukiwa na mifumo mibovu ambayo haiku rafiki na haiongei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia tena wakati wa Wizara ya Ujenzi watueleze kwanini Bandari za Mtwara na Tanga hazifanyi kazi? Tujue, kwanini Barabara ya kutoka Kilwa mpaka Liwale haifanyi kazi? Kila mpaka Nachingwea watu wanaangaika na mazao. Unategemea watu wale watategemea nini? wataendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naunga mkono lakini sifurahi, nataka nione kabisa mfumo wa kilimo katika mikoa hii

ya Lindi inapewa kipaumbele ili wananchi wale wasionekana kama ni wananchi maskini. Hii ni mikoa Tajiri, hivyo inahitaji msukumo na mfumo ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida. Tunaendelea na Mheshimiwa George Mwenisongole, Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mheshimiwa Edward Ole Lekaita ajiandae.

Mheshimiwa George Mwenisongele hayupo kama hayupo, tuendelee na Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu ya kilomo. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuijenga nchi yetu na kwa namna ambavyo ametoa kipaumbele kikubwa katika bajeti hii ya kilimo. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa pikipiki elfu 700, vishikwambi, 384 na *extension kits* 6,700 ni kilelezo tosha Mheshimiwa Rais anayo dhamira ya dhati ya kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo. Niwaombe sana Watanzania tumuombee mama yetu mpendwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ili aweze kuendeleza nchi yetu na aweze kuongoza vyema Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe Naibu wake Antony Mavunde, Katibu Mkuu Edward Massawe na watendaji wote wa Wizara hii ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuhakikisha kilimo chetu kinakuwa ni kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika eneo la umwangiliaji na endapo muda utatosha nitachangia katika zao la alizeti na zao kitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana mabadiliko ya tabia nchi na mazingira yetu jinsi yalivyobadilika tunahitaji kujikita katika kilimo cha umwangiliaji na si kilimo cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Singida ni miongoni mwa mikoa ambayo ni mikoa yenye jiografia iliyo kame sana. Hivyo, tunahitaji sana kuwekewa mabwawa ya umwangiliaji ili kuweza kuendeleza kilimo kwa msimu wa muda wote. Ninaomba sana tuweze kujengewa mabwawa ya kutosha katika Mkoa wetu wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu Skimu ya Umwangiliaji ya Mbwasa. Niishukuru sana Serikali imeweza kututengea fedha katika bajeti hii kwa ajili ya kuendeleza skimu hii ya Mbwasa. Hata hivyo, kwa kuwa usanifu yakinifu umeshafanyika naupembuzi niombe sasa skimu hii ianze kufanya kazi na utekelezaji wa skimu hii uanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunalo Bwawa Mngamo pamoja na Bwawa la Msange ambapo wananchi wa eneo hilo wanatumia maji hayo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za Kilimo. Niiombe Serikali, endapo mabwawa haya yataendelezwa yataweza kuwa na tija sana kwa wananchi wa Mkoa wangu wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Bashe alikuja akayatembelea Mabwawa haya ya Mngamo Pamoja na Msange na kujionea namna ambavyo mabwawa haya yanavyowanufaisha wananchi wa eneo hilo. Sasa nikuombe, kwa kuwa ulishatuma wataalam wakuja kuweka

michoro na michoro hiyo imeshakamilika niombe sana sasa kazi hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Singida tunalima zao la alizeti na kitunguu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amekuwa ni kinara katika kuendeleza zao hili la alizeti. Pia nipongeze sana Serikali ambayo ilitoa mbegu kupitia taasisi yetu ya *ASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yako maeneo mengine mbegu hizi zimezalisha alizeti vizuri lakini maeneo mengine mbegu hizi azijazalisha alizeti vizuri. Hivyo niiombe taasisi hii iendelee kufanya utafiti ili sasa kwa msimu unaokuja maeneo yote yaweze kulima alizeti na tuweze kuzalisha zaidi alizeti katika Mkoa wangu wa Singida, na vile vile ili upungufu wa mafuta uwe ni historia katika nchi yetu katika Mkoa wa Singida…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aysharose Mattembe tunaendelea na Mheshimiwa Edward Ole-Lekaita Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Timotheo Mnzava wajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na kwa sababu ya muda nitakuwa *brief* sana. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyofanya kuongeza tija kwenye kilimo. Ya kwanza, tumeona bajeti

imeongezeka sana, kutoka bilioni mia mbili karibu na tisini na kitu mpaka bilioni mia saba na hamsini na kitu. Hilo kwa kweli ni *a right step in right direction.* Nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kazi za alizofanya Dubai *Expo*, tumeona mikataba mingi imesainiwa ya kuongeza tija katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri wa Kilimo, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe; Naibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima ya Kilimo kwa kazi kubwa wanayofanya. Kwa kweli tumeona *a revival* ya kilimo na tunategemea mengi sana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto ni *food basket* na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu alitembelea Kiteto. Nilikuwa nasoma taarifa hapa lile ghala la Ngusero ambalo liko chini sana asilimia 16 na anajua kwa nini iko hapo kwa sababu ya mkandarasi aliyekuwepo, Mheshimiwa Waziri a-*push* ili tumalize hili ili wananchi wa Kiteto wakapate kuhifadhi mahindi. Kiteto ripoti zake ukizisoma ile *post-harvest loss* ni karibu 40%, kwa hiyo hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana pia Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kiteto wamefarijika sana kwa kilo 25,000 alizogawa za mbegu ya alizeti. *Big up* kwake, wananchi kwa kweli wamefarijika sana. Nakushukuru vilevile kwa kazi inayoendelea sasa ya kuhamasisha watu kuhusu alizeti. Kwa kweli tumeshajiwekea mkakati kama Taifa kwamba ili tuweze kupata mafuta ya alizeti hapa nchini, ni lazima tupate mbegu nzuri na vilevile wananchi wa Kiteto wako tayari…

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Neema. Mheshimiwa Kisau pokea taarifa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Mheshimiwa Waziri asithubutu kuruhusu *GMO.* Akiruhusu *GMO* ataua kilimo chetu kwa sababu tutategemea teknolojia ya kigeni, ni unyonyaji kwa wakulima na tutapoteza asili ya mimea. Kwa hiyo Waziri asiruhusu kabisa suala la *GMO* kwenye nchi yetu ya Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Lekaita taarifa hiyo unaipokea.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijaongelea mambo ya *GMO, but I agree with her.* Ni kweli alishasema Mheshimiwa Waziri hapa siku moja na biashara ya *GMO* ni biashara kubwa sana, ina *issues* nyingi sana, inahitaji mjadala mkubwa wa kitaifa, kwa hiyo nakubaliana naye sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza kuhusu Kiteto na jinsi wakulima wangu walivyo tayari kwa ajili ya kuzalisha mafuta na mbegu za alizeti. lakini wanachotaka ni kitu kimoja tu, Serikali iweke mkakati tujue *price* ya alizeti ili tuhamasike tujue kabisa *projection* ya *prices* mwakani zikoje ili wananchi waweze kuhamasika. Nadhani tukifanya hivyo itamshawishi kila mtu na ataingia kwenye kilimo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 130, walisema walikuwa na nia ya kuwawezesha vijana 400 katika mikoa tisa na Manyara ikiwemo. Nilipiga mahesabu ni karibu vijana 45 kila mkoa na ukipiga mahesabu ya wilaya zile Kiteto ilikuwa inapata vijana sita sio chini ya sita. Sasa nataka Waziri atujibu hili wameshalifanya kwa sababu sisi Kiteto hatujasikia popote, vijana wale sita ambao walitakiwa kuwawezesha kuwapa zana hizi, nataka nisikie kwenye hitimisho. Tusije tukakaa tunapitwa, kwa hiyo *please, comment on this.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inaongelea sana kuhusu umwagiliaji na ni kweli *is a shame as a country* kwamba *projection* ukiangalia *data* za umwagiliaji tuko chini sana, *less than 2. 5 %...*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kwa ufupi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na hao vijana ambao wamemtaka Mheshimiwa Waziri katika hitimisho lake aseme chochote, wako vijana kwa ushirikiano wa Tanzania na Israel kila mwaka kama 100 wanaenda Israel kujifunza mambo ya kilimo lakini wakirudi hapa wanabaki *idle*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Lelekaita taarifa hiyo unaipokea.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea.

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa sababu ya muda naendelea kuzungumzia kuhusu suala la umwagiliaji. Ni kweli wameweka pesa nyingi kutoka bilioni 17 mpaka bilioni 51, *fine,* lakini tunapoteza maji mengi sana wakati wa mvua, tusipofanya hii, nadhani tungekuwa na *like a rapid fund* fulani ili mvua zinapotokeza tusipoteze maji kwa ajili ya umwagiliaji. Tukifanya hivyo tukawa *quick* itatusaidia tusipoteze maji mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niishie hapo lakini kwenye umwagiliaji vilevile kama tunataka

kufanya vizuri zaidi, mashine zile zinazotusaidia kwa ajili ya umwagiliaji, Mheshimiwa Waziri apiganie ili kodi ziondoke ili wananchi wapate *encouragement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa kabisa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Lelekaita, utakuwa una upendeleo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Timotheo Mnzava na Mheshimiwa Keneth Nolo wajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara ya Kilimo. Jambo la kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, moja kati ya Mawaziri ambao ni vijana, tunajivunia lakini na Bunge linajivunia, Mheshimiwa Bashe pamoja na Mheshimiwa Anthony Mavunde kwa sababu wanatupa ushirikiano wa kutosha nyakati zote, hata usiku ukimtafuta anakusaidia. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri anatuongoza vizuri vijana na tuko tayari kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya yanayoendelea kwenye bajeti zote alizozisoma Mheshimiwa Waziri, wakati ule tunagawa vifaa na hii iliyosomwa, inaonesha wazi kwamba kilimo kinaenda kubadilika kwenye Taifa letu. Waziri ana mwono wa mbali kwa kiwango ambacho mimi kama kijana najivunia sana uwepo wa Mheshimiwa kaka Bashe kwenye Wizara ya Kilimo na tunampongeza sana. Kwa niaba ya wananchi wa Makete nimpongeze sana. Uono wake wa

mbali ni pamoja na kwenye bajeti yenyewe ambayo alimwomba Mheshimiwa Rais. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya *change* kwenye kilimo kwa kuongeza bajeti hadi bilioni 700.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliomba zaidi ya trilioni mbili kwenye Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Rais kwa sasa ametuanzia na bilioni 7. Ukienda kwenye bajeti ya Kenya wanacheza na bilioni 900 hadi trilioni moja, kwa hiyo anawafukuzia, yuko nyuma yao kidogo anawasogelea, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. Akienda kwenye bajeti za Zambia na Uganda naona bado sisi tunazidi kukimbiza kwa hiki ambacho anaenda kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu uko kwenye mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza ni suala la mbolea, naungana na Mheshimiwa Waziri kwa asilimia 100. Siku ile alimwambia Mheshimiwa Rais ampe bilioni 150 kwa ajili ya ruzuku kwenye mbolea. Mimi kama Mbunge wa Makete namuunga mkono na kwa niaba ya Wabunge wa Kusini tunamuunga mkono kuhusu ruzuku kwenye mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea sisi kwetu ni siasa, mbolea kwetu ndio uhai wa wakulima wetu, mbolea kusini ndio kila kitu kwa wananchi wetu. Nimwambie wazi Mheshimiwa Waziri, yeye ndiye amebeba Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu Chama cha Mapinduzi ni chama cha wakulima na wafanyakazi. Mbolea ni kilio na naiona *direction* ya Waziri anayoenda kuichukua ya kuomba fedha bilioni 150 kwa ajili ya kwenye ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema jana kwamba ni bora Wizara ya Kilimo isifanye kitu chochote lakini iongeze ruzuku kwa wakulima. Niwaahidi wananchi wa Makete Mheshimiwa Bashe hili tutamwombea kwa Mheshimiwa Rais na namwomba Mheshimiwa Rais bilioni 150 na zaidi hapo aweze kumpatia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alifika hadi Makete Kijijini kule Kinyika alijionea hali ya wananchi wangu. Changamoto ya parachichi tuliyonayo ni kubwa sana. Parachichi, limeanza na mguu mzuri, parachichi kwa sababu halina lumbesa wanapima kwenye mizani, tunaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ya parachichi ni kwamba kumekuwa na wakulima holelaholela ambao hawafikiwi na Maafisa Ugani, uzalishaji wa miche holela holela ambao miche mingine ina ubora huu, mingine ina ubora huu. Changamoto tunayoipata tutafika wakati miti imekua hatuna wa uwezo tena wa kurekebisha kwenye miti ya mbolea. Tunaomba wizara iwahi mapema sekta ya parachichi ndani ya Mkoa wa Njombe, Mbeya na maeneo mengine iwekewe mpango mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukienda Wakenya wanaingia hadi mashambani kununua parachichi zilizoko kwenye shamba. Sasa ni vyema tukaandaa mazingira, wakulima wetu wawe na muundo mzuri wa jinsi gani biashara ya parachichi itaenda.

Mheshimwa Mwenyekiti, nimemwandikia barua Mheshimiwa Waziri na nimempelekea mezani kwake. Naomba miche milioni 15 kwa ajili ya wananchi wa Makete kwa sababu nina kampeni Makete ya nyumba moja miche 50. Leo naomba tena Waziri atuwekee kitalu cha parachichi Makete, ile miche inayozalishwa pale iendane na hali ya hewa ya Makete na izalishwe katika ubora kupitia Maafisa Ugani. Ninamsihi na namwomba Waziri, miche milioni 15 iko mezani kwake, namwomba wananchi wa Makete wanasubiri kampeni ya nyumba moja miche 50 kwa sababu tunaamini ndiko utajiri uliko na mkakati wa wazi kabisa wa kuwakomboa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata *cold room,* Mheshimiwa Waziri amesema anajenga *cold room* nyanda za juu kusini. Tunaomba hata Makete tuna eneo la karibu na *airport* ya Mbeya kwa sababu Njombe *airport* hawajatujengea. Ili tuwahishe mzigo Mbeya kwenye *airport* yetu ambayo itakuwa inapakia parachichi kwenda kule na kwenye treni, Waziri ajenge *cold room* Mbeya pale au Makete itusaidie ili wananchi wetu wasipate shida ya kuhangaika kutafuta sehemu ya kuweka *cold room.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sawasawa na hilo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la lumbesa. Waziri amehangaika kadri awezavyo, suala la lumbesa na wananchi walimwambia. Lumbesa itatatuliwa tu kwa kuweka mizani na hili ni suala la viwanda na biashara. Watu wa viwanda na biashara kama wako hapa waweke mizani tuondokane na changamoto ya lumbesa. Tuondokane na changamoto ya lumbesa kwa nini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malizia sentensi yako tu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia sentensi yangu moja. Mheshimiwa Bashe iko hivi, Wakenya wanavyokuja na wakulima wengine wanakuja kununua viazi, wananunua gunia moja lina lumbesa, lakini wakienda kwao wanapima kwa mizani. Kilo mia ni sawasawa na gunia moja. Hapa imeondoka na gunia lina kilo 140. Kwa hiyo kama liliondoka na gunia 300 akifika Kenya anakuwa na gunia 400 mpaka 500. Wakulima wetu huku wananyonywa tunafaidisha wananchi wengine. Serikali iweke mizani ili tuondokane na lumbesa. Wizara ya Viwanda na Biashara

tunaomba watusaidie,waweke mizani, lumbesa linawamaliza wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga. Tunaendelea, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Timetheo Mnzava, Mheshimiwa Keneth Nolo na Mheshimiwa Twaha wajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Sekta hii ya Kilimo ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Naomba nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Bashe kwa Naibu Waziri Anthony Mavunde, Katibu Mkuu Andrew Massawe na watendaji wote wa Wizara kwa kuhakikisha kwamba kilimo kinaweza kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa mapinduzi ya kilimo kweli kweli, wananchi wanategemea sana, wanamwamini sana Mheshimiwa Bashe kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu kwa hotuba yake ya siku ya tarehe 24, siku ambayo walikuwa wanagawa vifaa vya wagani wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu siku ile Maafisa Ugani wamepewa vifaa, lakini naomba wapatiwe elimu, hiyo elimu iendane na maeneo ambayo tunatokea. Kwa mfano, Mkoa wetu wa Iringa tunalima mahindi, chai, pareto, alizeti, parachichi basi wale Maafisa Ugani wawe angalau wana elimu ya hayo mazao ambayo tunayalima katika maeneo yetu ili rahisi kwa sababu Wizara imeanzisha mashamba

darasa inakuwa rahisi hata kutoa elimu kwa wakulima na kilimo kitakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua bado tuna upungufu kiasi gani wa Maafisa Ugani ili tuweze kujua kwamba watatusaidiaje. Pia nataka kujua tunao vijana wetu ambao wamehitimu masomo ya kilimo katika vyuo vyetu nchini. Hawa vijana wako katika wilaya zetu, halmashauri zetu lakini je, Serikali haiwezi kuwachukua wakasaidia hata katika haya mashamba darasa? Kwa sababu tulivyokuwa zamani tuna upungufu wa Walimu tuliwachukua Walimu katika masomo ya sayansi wakawa wanajitolea. Huu ndio uzalendo, lakini vijana wetu wamekatwa, wamehitimu masomo yao vizuri, wamekaa hawafanyi kitu chochote. Tunaomba pia hili Serikali iliangalie ili tupunguze hata upungufu wa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze Serikali kwa mambo yafuatayo:-

(a) Kuongeza pesa ya utafiti;

(b) Kuongeza eneo la umwagiliaji;

(c) Upatikanaji wa mbegu bora;

(d) Ununuzi wa nafaka; na

(e) Ushirika na masoko ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea tunaomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi. Mbolea ukienda kila sehemu, kila mkutano, changamoto kubwa ni bei ya mbolea. Kwa hiyo tuna imani kabisa kwamba sasa hivi tumesema kwamba kuna kiwanda, lakini ulikuwa unaomba ruzuku kwa ajili ya mbolea ili bei iweze kupungua kabisa, maana yake wakulima

wengi wameshindwa hata kulima sasa hivi, wamevuna eneo dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine, naomba pesa ya utafiti ipelekwe kwa wakati ili hizi tafiti ziweze kufika kwa wakulima, kwa sababu changamoto kubwa ya utafiti kwamba tafiti nyingi zinafanyika, lakini hazifiki kwa wakulima. Kwa hiyo kilimo kinakuwa hakina tija kwa sababu zile tafiti zinafanyika, lakini zinakaa katika vituo vya tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze uwekezaji wa eneo la umwagiliaji. Kwa kweli na niwapongeze sana kwa sababu hata katika Mkoa wetu wa Iringa tuna miradi mingi ya umwagiliaji, lakini wametukumbuka katika Mradi wa Mgambirenga katika Wilaya ya Kilolo. Kwa hiyo niombe, kwa sababu umwagiliaji ndio kilimo kinachotakiwa, ndio kilimo cha uhakika. Umwagiliaji kwa mfano, Zimbabwe mabenki hayawezi kukukopesha kama hulimi kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo niombe na sisi sasa tuweke pesa nyingi katika umwagiliaji ili wakulima wengi wamwagilie ili tuwe na uhakika wa mazao yetu tunayoyalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru sana katika Mkoa wetu wa Iringa wameweza kutupatia fedha kufufua zao la chai katika Wilaya ya Kilolo. Wilaya ya Kilolo watu walikuwa wamekata tamaa kabisa kwamba sasa hivi hatuwezi kabisa, tunaichukia na Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda Kilolo akawaahidi na sasa hivi hii Serikali ni Sikivu, inatoa pesa na zao sasa la chai katika Wilaya ya Kilolo linafufuka, Halmashauri ya Kilolo itapata pato, wananchi watapata pato na Serikali itaongeza pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kuhusu kilimo cha mbogamboga. Kwa kweli sekta hii ni ndogo lakini inaongoza katika mapato ya *export* na mapato ya soko la ndani. Hapa naomba nimpongeze Dkt. Jacqueline Mkurugunzi wa *TAA* pale Arusha. Kwa kweli tulimtembelea

pale Arusha, amesaidia sana katika kuhakikisha kwamba mbogamboga na matunda Tanzania sasa hivi inawezekana. Nipongeze pia hata Serikali yetu kwa kutafuta soko la parachichi. Lakini nimpongeze pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia pongezi yako

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hadija Jabiri pale Iringa na yeye anatusaidia sana katika zao la mbogamboga na matunda ambako wanawake wengi sasa hivi tumejikita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitaandika kwa maandishi kwa sababu naona kwamba *point* zangu zingine sijazitoa, lakini namshukuru Mungu…

**MWENYEKITI:** Pole sana Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Muda wetu ni mchache sana naomba sana muende kwenye *point* muhimu ambazo mnaona ni za lazima.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Keneth Nolo, Mheshimiwa Twaha Mpembwenwe, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Cecil Mwambe wajiandae.

**MHE. TIMETHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na wenzangu kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, vijana wenzangu, kwa uteuzi wa kuongoza Wizara hii. Tunawafahamu vizuri, tufahamu uwezo wao na tuna matumaini makubwa sana na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende harakaharaka, muda ukiruhusu nitakuwa na mambo matatu. Jambo la kwanza ni kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha Umwagiliaji kinaongeza tija, kinaongeza eneo la kulima na kinaongeza vipindi na misimu ya kulima. Ninazo takwimu kuanzia mwaka 2015 mpaka sasa tumeongeza hekta ngapi kwenye kilimo cha umwagiliaji, lakini kwa sababu ya muda sitaki kuzitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona malengo ya Mheshimiwa Waziri, ameweka malengo ya kuongeza hekta elfu tisini na tano na tano kwenye mwaka wa fedha huu unaokuja. Jambo hili litawezekana kama mambo makubwa mawili yatafanyika. Jambo la kwanza ni lazima kama nchi tukubali kutafuta fedha zaidi nje ya bajeti zetu tulizokuwanazo kwa ajili kugharamia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kuhakikisha tunasimamia na kutekeleza miradi mikubwa itakayo-*cover* eneo kubwa.  Kwenye eneo hili niwe *specific* kabisa kwenye eneo la Bwawa la Mkomazi. Bonde la Mto Mkomazi na Bwawa la Mkomazi. Tumesema sana, tumefanya vikao vingi, ni ahadi ya chama chetu kwenye uchaguzi na Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwa watu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha nataka kusikia nini kinakwenda kufanyika na wakati gani kuhusu Bwawa la Mkomazi, pamoja na urafiki na kazi anayoifanya nisiposikia kitu cha kuwaridhisha watu wa Korogwe, nitakuja kushika Shilingi.

Mheshimiwa Spika, siyo tu Mkomazi kuna Bwawa la Kwamkumbo tunayo ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo hatujaona kinachoendelea, tumekwama wapi? Ukija kwenye majumuisho nitapenda kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ili niweze kuzungumza kwenye suala zima la zao la mkonge, Mheshimiwa Waziri nimeona umesema malengo yetu ni kutoka tani 36,698 kwenda mpaka tani 60,000 kwenye mwaka wa fedha unaokuja, naomba kukumbusha jambo, hatuwezi kufikia haya malengo kama hatutaendelea kuwajali na kuwathamini wakulima wadogo wadogo, mchango wa wakulima wadogo ni mkubwa sana kwenye zao la mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2019 kwenye tani tulizozalisha, mchango wa wakulima wadogo ni asilimia 24, mwaka 2020 ni asilimia 30 na mwaka 2021 ni asilimia 37. Lakini wakulima wanachangamoto, Mheshimiwa Waziri tumehamasisha, Waziri Mkuu amefanyakazi nzuri, lakini bado kuna changamoto kubwa kwa wakulima wadogo wadogo. Mashine za kuchakata mkonge imekuwa ni changamoto. Tumeleta kampuni kule Sisalana imechukua mitambo kuwa ya katani wanawazalishia wakulima wetu. Gharama ya uchakataji ni kubwa sana inawaumiza wakulima wetu, lakini mitambo ile ni mibovu inafanya tunapata mkonge mchache lakini pia hata ubora wa mkonge wenyewe unapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema sana, ninashauri mambo matatu kwenye jambo hili. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Naibu wako alikuja Korogwe, Bodi ya Mkonge waliunda Kamati ya kupitia zile gharama, wameenda wamekwama wanasema subiri Mkuu wa Mkoa aseme. Bodi ya Mkonge ndiyo yenye dhamana ya kusimamia mkonge kwenye nchi hii. Tunawaomba toeni tamko juu ya

bei halali inayofaa kulipwa na wakulima wetu wadogo wa mkonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Waziri tununue mashine, Bodi na Wizara nunueni mashine za kuchakata mkonge muwape wakulima wetu. Jambo la tatu Mheshimiwa Waziri bado wakulima wetu wanamadai na Kampuni ya Katani. Mlichukua mitambo ya katani akapewa *NSSF* akaenda Kampuni ya Sisalana, lakini ukweli ni kwamba kwa mujibu wa Waraka Na. 31 wa 2005 wa Baraza la Mawaziri, Katani alipaswa kutengeneza kampuni ili wakulima wetu wadogo wadogo wawe hisa kwenye kampuni hizo kwenye zile *AMCOS* tulizokuwa nazo, mambo hayo hayakufanyika. Leo umechukua mitambo umempa Sisalana anawahujumu wananchi wetu, anawahujumu wakulima wetu. Mashine ambayo ilitakiwa izalishe ichakate mita 100 kwa siku leo wanachakata mita 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini cha kufanya Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Kilimo ninyi ndiyo wasimamizi wa sera kwenye eneo la kilimo. Kaeni na Msajili wa Hazina tupitie ule mchakato ulivyokuwa, tutoe hizi mashine kwa Sisalana tuwape wananchi, tuwape wakulima wadogo kwenye *AMCOS* zao wasimamie. Pia mnaweza mkatusaidia kuwa wasimamizi wa mazungumzo kati ya *AMCOS* zetu na Benki ili wakulima wetu kupitia *AMCOS* zao wakopeshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hakuna hatari kubwa kwenye zao la mkonge kama kutenganisha mchakataji na mzalishaji. Mchakataji akiwa hana uchungu na mazao ya mkulima atamkwamisha, na ndicho kinachofanyika, kampuni hii kwa sasa inawahujumu wananchi wetu. Mheshimiwa Naibu Waziri umeenda umewaambia wachimbe kisima wachakate mkonge mwingi kwa siku, watoe mkonge ulio bora Zaidi, mpaka leo hakuna kilichofanyika. Sisi ndiyo tuna dhamana kusimamia mkonge Wizara ya Kilimo, tusiwaachie watu wakacheza na mkonge

wa wakulima wetu, watawakatisha tamaa, wataacha kulima, tutarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamb la mwisho ni upande wa chai.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge muda wako umemalizika.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe dakika moja nimalizie. Bodi ya Chai isiwasahau wakulima wa Usambara kama inavyofanya kwa wakulima wa Mafinga na Nyanda za Juu Kusini, kiwanda cha Mponde tumekisubiri kwa muda mrefu ni wakati sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Oran Njeza kabla hatujaanza na Mheshimiwa Kenneth kuna mgeni kwenye *Speakers Gallery* ambae ni mgeni wa Mheshimiwa Bashe Waziri wetu wa Kilimo ambaye ni *Ms.* Angelina Ngatula ambaye ni Mwenyekiti wa Sekta Binafsi. Naomba tutambue uwepo wake, karibu sana Mwenyekiti wa Sekta Binafsi *Ms.* Angelina Ngatula.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza sasa na Mheshimiwa Kenneth Nollo na wanaofuata wengine niliowataja tutaendelea nao. *(Makofi)*

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu asilimia 23 ya ardhi ndiyo inayotumika katika kilimo. Nchi yetu ina watu milioni 40 ambao wanajihusisha katika kilimo. Kwa hiyo, ukiangalia Sekta ya kilimo ndiyo sekta kubwa

inayoajiri, ndiyo inayotegemewa katika maisha yetu katika ustawi wa Taifa letu. Kwa hiyo, nilitaka kusema jitihada za Mheshimiwa Waziri ni nzuri, lakini ukizipima siyo jitihada za kimapinduzi, bado dira ya kimapinduzi ya kuboresha kilimo chetu na kwenda katika malengo hasa ya kuliendeleza Taifa hili bado, nimeangalia hii bajeti kuna eneo bado hatujakaa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amerejea Awamu ya Kwanza Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu. Nilitaka rejea ileile ya kuanzia Awamu ya Kwanza na kuishia Awamu ya Tatu. Awamu ya Kwanza tuliamua kwamba kilimo cha nchi yetu kiwe ni kilimo cha wakulima wadogo wadogo, lakini tuliamua kwamba wananchi watengenezewe viwanda ambavyo vitahudumia kilimo chetu. Kwa bahati mbaya Awamu ya Tatu tukaja tukabinafsisha viwanda vya kuhudumia kilimo, vilevile tukabinafsisha mashamba makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka kusema na ili nimshauri Mheshimiwa Waziri Bashe, kwamba pamoja na jitihada zake kubwa ni lazima tuamue tunafanya kilimo cha wananchi wengi au tunataka kufanya kilimo cha kibepari au tunataka kuunganisha kilimo cha wananchi wengi pamoja na ubepari. Ninasema hivyo kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika hoja ya msingi ukitaka tulete makampuni makubwa, kampuni kubwa inahitaji uwe na eneo kubwa, Wilaya nzima ya Bahi unaipa kampuni kubwa iweze kulima na iweze kusafirisha. Lakini kwa wananchi wetu katika umoja wao, unaweza ukawaunganisha ukawatengenezea ushirika mzuri na tukaweza kulima kwa pamoja na tukawa na viwanda vya kutuhudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo naliona katika nchi yetu bado tunapandishia mifumo, tunachukua

mfumo wa Kimarekani tunachanganya na mfumo wa China na mfumo wa Vietnam hatuwezi kusogea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu kwa mfano Vietnam, Vietnam sasa ndiyo inayouza mchele ukijumlisha mchele wa Afrika wote katika ku-*export* hauwezi kuifikia Vietnam nchi ndogo. Wenzetu wamefanya katika maana ya ushirika, vyama vyao vya Ushirika vina nguvu. Kwa hiyo, kazi ya Serikali kwanza itoe fedha katika ku-*finance agriculture* ambapo tumeanza kwenye umwagiliaji kwa kiasi kikubwa lakini vilevile ushirika wetu tuimarishe, mahusiano ya Serikali na Ushirika usiwe kama Polisi na mtuhumiwa! Kwenye Ushirika bado kuna shida hakuna Uongozi. Kwa hiyo, nilitaka kwanza hiyo *contradiction* Wizara ya Kilimo na Serikali waweze kuiangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka nichangie kuhusu Kanda ya Kati. Kanda ya Kati tuchukulie kuanzia Mkoa wa Tabora, Wilaya za Nzega kuja Singida na Dodoma, bado Serikali haijawekeza kwenye kilimo! Hali ya chakula bado ni mbaya, tunasumbuliwa na ukame, lakini bado hatujawa na sera madhubuti kwamba ni namna gani tunasaidia kilimo katika Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Nigeria walianzisha sera ya maeneo yenye ukame na wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo sisi bado, pamoja na hisi skimu ambazo mmetuletea nazo nilikuwa nazihesabu ni kidogo mno lakini bado suala la Kanda ya Kati hatuja-*address* kilimo hiki, bado kuna *dilemma* kubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme kuhusu suala zima la zabibu. Mimi nimekua katika miaka ya 1980 tulikuwa tunalima sana zabibu, bahati mbaya zabibu ikaja ikafa kwa maana ya kuharibu kile kiwanda na tukakosa soko Zaidi, lakini sasa….

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi ya mwisho.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iamue kuwekeza kwenye zabibu, kiwanda chetu cha *DOWICO* kirudishwe lakini tuanzishe bodi ya kusimamia zao la zabibu, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Nollo tunaendelea na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Constantine Kanyasu ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Twaha hayupo naomba tuendelee na Mheshiwa Jacqueline Msongozi na baadae Cecil Mwambe ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Kilimo bajeti hii ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma hii bejeti na maudhui yake yote ni bajeti ya kupigiwa mfano toka nimekuwa Mbunge Awamu ya Kwanza na sasa Awamu ya Pili. Kutoka Shilingi Bilioni 274 mpaka kufikia Shilingi Bilioni 751 siyo mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi niombe sasa, Mheshimiwa Waziri nia yake ni njema, amekuwa akifanyakazi vizuri sana na tunayo matumaini makubwa sana Watanzania kupitia Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Hussein Bashe kwa namna ambavyo amejipata vizuri yeye na timu yake kuhakikisha kwamba analeta mageuzi makubwa sana katika sekta ya kilimo. Sisi tunakutakia kila la kheri Mwenyezi Mungu akupe afya njema wewe pamoja na Naibu wako na Watendaji wako, tunamuomba tu Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania aendelee kukuacha hapo kwenye nafasi hiyo ili malengo yako na ndoto yako ya kuwatumikia wananchi na kufanya mageuzi yatimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumze kuhusiana na suala la mbolea. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza, kwamba tarehe 4 Aprili, katika ukumbi wa Jakaya Kikwete hapa Dodoma, Mheshimiwa Rais alizungumza na Watanzania kupitia mkutano ambao ulikuwa umeandaliwa na Waziri wa Kilimo, akaahidi kwamba katika sekta ya kilimo atahakikisha kwamba anaweka ruzuku ya shilingi bilioni 150 ili kuenda kuwasaidia wakulima kupata nafuu na afueni kwenye suala la mbolea. Ninaomba isije ikawa hapa ndani ya Bunge kazi yetu ni kudemka tu na utekelezaji haupo. Niwaombe sana Wizara ya Fedha, pesa hizi ambazo Mheshimiwa Rais amesema ziende kilimo Shilingi Bilioni 150 mkazitoe ziende na Mheshimiwa Rais anamaanisha kama hamzazijua rangi zake basi Wizara ya Fedha safari hii kama hamjapeleka fedha hii bilioni 150 mtaona rangi halisi za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nizungumzie suala la Benki ya Kilimo. Tunahitaji Benki ya Kilimo katika Mkoa wa Ruvuma. Ninaomba sana leo hii nazungumza hapa kuhusiana na suala la Benki ya Kilimo nataka nitumie lugha ya kudemka, msituchukulie kwamba kazi yetu kudemka, leo nachangia hapa nimeshauliza maswali mengi ni kama siku ya 13 ninachangia suala hili la Benki ya Kilimo, ninaomba Benki ya Kilimo ipelekwe katika Mkoa wa Ruvuma kwa sababu zifuatazo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa ambao ni Benki ya Chakula, tunawahakikishia tutashika nafasi ya tano katika uzalishaji wa mazao ya nafaka. Ni wazi kwamba Mkoa wa Ruvuma unachangia pato kubwa sana katika Pato la Taifa, linachangia fedha nyingi sana kupitia suala la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wakulima wangu wanalima kwa kutumia majembe ya mkono mpaka sasa hivi pamoja na kuwa tumekuwa tukiongoza na ni benki ya chakula, kwa nini Wizara ya Kilimo msitupelekee Benki ya Kilimo katika Mkoa wa Ruvuma? Tunahitaji Benki ya Kilimo na niseme Mheshimiwa Bashe kupitia hili suala la Benki ya Kilimo nimechoka kuzungumza ndani ya Bunge hili na ninakuambia kabisa ninakusudia kukamata shilingi ya yako kuzuia bajeti yako isipitishwe, endapo kama utakapokuwa unakuja hapa una-*windup*, huna maneno mazuri yatakayo-*stimulate* wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kupata Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maneno yapita yanasema kwamba ooh! Benki ya Kilimo, tumeshakopesha huko, nenda kaone wapi, tunataka iandikwe pale kama ilivyoandikwa benki nyingine *Microfinance Bank* tunataka iandikwe pale Benki ya Kilimo, Mkoa wa Ruvuma. Wananchi waingie pale, anayekuwa na shamba dogo la heka tano akakope, mwenye shamba la heka 10 akakope, badala ya hizo blaah! Blaa! za chini ya pazia, tunahitaji Benki ya Kilimo, unahitaji *degree* ngapi kujua kwamba Mkoa wa Ruvuma kuna umuhimu wa kupeleka Benki ya Kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilitaka kupanda juu ya meza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacquline naomba umalizie, umeeleweka sana. Mheshimiwa Jacquline umeeleweka sana. Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline.

Tunaendelea na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Constatine Kanyasu, Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Luhaga Mpina wajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana Wizara ya Kilimo na kama tunavyofahamu kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kazi kubwa sana inayofanywa na Mheshimiwa Bashe na Msaidizi wake Mheshimiwa Mavunde na Wizara yote kwa ujumla na imekuwa yenye tija kubwa kwa wakulima. Nitakuwa na mchango wangu wa maandishi ambao tayari nimeshautuma ukihusu suala la Bodi ya Zabuni inayosimamia masuala ya pembejeo pamoja na magunia, madeni ya wazabuni mbalimbali kwenye Bodi yetu ya Korosho kwa maana ya *CBT*. Pia nimeleta mchango wangu wa maandishi kuhusu udhaifu wa Menejimenti ya *CBT* na malalamiko ya watumishi pamoja na viambatisho vyake, nimeleta pia mchango wangu kwa maandishi kuhusu madeni ya Wazabuni mbalimbali hasa madeni ya *bond*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo, tunashukuru maazimio yaliyofanywa na Serikali kuhusu suala la pembejeo lakini ninamuomba sana Mheshimiwa Bashe kwamba mara nyingi pembejeo hizi zinaletwa bure huwa hazitoshelezi kwenye soko lote. Hapo nyumba tulikua na utaratibu wa ruzuku, sasa uone namna ya kusaidia kwa sababu pembejeo zinakwenda chache hazifiki mara nyingi kwa wakati lakini wakulima bado wanalazimika kwenda kununua kwenye maduka ya kawaida ya kibiashara. Sasa wanapofika kwenda kununua ili waweze kuongeza pembejeo ile iliyotolewa na Serikali bure wanakuta pembejeo hiyo ikiwa na gharama kubwa sana. Kwa mfano, mfuko wa *sulphur* unaweza kufika shilingi 50,000 au shilingi 80,000 ili waweze kujitosheleza. Kwa hiyo, ninakuomba tuangalie sasa na ule utaratibu wa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, jingine ni kuongezee kwamba wakati huu Serikali imeweze kulipia hizi

pembejeo zinazoitwa za bure kutokana na fedha ambayo ilikuwa ni ya *export levy* iliyokuwa inachangiwa na wakulima hapo nyuma, jambo hili halipo kisheria na Mheshimiwa Waziri umelifanya labda kwa sababu mahusiano yako mazuri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sasa ninaomba wakati wa *Finance Bill* muilete hiyo, muibadilishe ili fedha hii ya *export levy* itamkwe kabisa kwamba inakwenda kulipia pembejeo na wakulima wa korosho na wengine wapate pembejeo hizo za bure tunazoziita lakini kwa kutumia fedha hiyo na iwe kabisa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni usambazaji. Mwaka jana tulishuhudia upungufu kidogo kwenye usambazaji hasa zaidi kwenye upande wa magunia, sasa Waziri utakapokuwa unahitimisha pia utueleze Kama umejipanga kiasi gani mwaka huu kuhakikisha hakuna uhaba wa magunia kwenye zao la Korosho kwa sababu ilisumbua sana kwenye misimu iliyopita, kwa hiyo tunaamini wewe pamoja na Wizara yako umejipanga vizuri kwenye hili sambamba na masuala ya *Sulphur* ili wakulima waweze kupata *Sulphur* inayojitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ninakuomba hakikisha sasa unasimamia vizuri ili magunia yaeleweke pamoja na hizi *Sulphur* mchakato wa usajili wa wakulima, zoezi hili lilianza lakini mpaka sasa hivi halijakamilika na ni muda mrefu sana. Nikukumbushe pia kwa sababu ya muda suala la Bodi. Bodi yetu ni mpya lakini huduma inayotolewa na Bodi….

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Cecil Mwambe naomba usubiri, Mheshimiwa Katani.

**T A A R I F A**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kuwa Mheshimiwa Waziri tena kwake kule kwenye Tumbaku ameweka mfumo sahihi wa wakulima na hakuna dhuluma ya kwenye pembejeo. Sasa taarifa yangu anapo *windup* ahakikishe kile alichokifanya kwenye Tumbaku kinakwenda kwenye korosho ili aweze kubaini wakulima sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe unapokea hiyo taarifa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Katani na mimi nimuongezee Mheshimiwa Waziri kwamba hata kwenye masuala ya viwanda, tulikuwa tuna viwanda vya korosho Masasi, Lindi, Mtama, Nachingwea pamoja na Newala lakini sasa tunaona Mheshimiwa Waziri anatumia juhudi kubwa sana kufufua Kiwanda cha Tumbaku kilichopo Morogoro cha *TLTC* labda kwa sababu pia nacho kama anavyoniambia Ndugu Katani kwamba ni mdau wa tumbaku na anatoka Tabora anataka kuwapendelea zaidi watu wa Tabora na sisi watu wa Mtwara kutuacha nyuma kidogo. Kwa hiyo, nimuombe kabisa, mikakati ile iliyofanyika kwenye Tumbaku na mazao mengine ailete sasa kwenye korosho ili tuweze kwenda nae sambamba, tuweze kumshukuru kwa kazi nzuri anazozifanya, tuendelee na tunaamini kwamba haya yote atayafanya katika mwaka huu wa fedha ili tusiwe na malalamiko Wabunge tunaotokea kwenye maeneo yanayozalisha korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo waangalie na masuala ya bei. Kuwe na timu ya uhakika kwenye Bodi yetu ya Korosho inayoweza kupata bei za uhakika ili hata wanunuzi wanapokuja kununua kuwe kunafanana kidogo na bei zilizopo kwenye soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mwaka 2021 bei zikidondoka, tunaambiwa matatizo yalikuwa ni UVIKO na mengine. Tunaamini kwa sababu UVIKO sasa umekwisha, bei zitakuwa bora. Miaka miwili mitatu iliyopita korosho iliuzwa mpaka Shilingi 4,000/= lakini mwaka 2021, hapo kati kati tumeshuhudia korosho inauzwa kwa Shilingi 1,500/= mpaka Shilingi 2,000/= kwa wastani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine namwomba Mheshimiwa kuhakikisha tunarasimisha ule utaratibu wa upili. Hata kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi lipo hili suala. Upili ni Soko la Umoja kwa maana ya ile *Primary Market*. Hili ni lile soko ambalo linawasaidia wananchi kuweza kutatua matatizo yao kwa mara moja. Huwa linatumika jina la Kangomba, lakini siyo neno jema kwa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka sisi ni kwamba mwananchi ambaye ana korosho debe moja ndani ya nyumba yake, baba yake anaumwa, anatakiwa kumpeleka hospitalini, maghala hayajafunguliwa, atazipeleka wapi korosho zake akazibadilishe ziwe fedha aweze kupata huduma? Kwa sababu hawezi kupeleka debe la korosho hospitalini akapata huduma. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nitachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa kutumia vizuri dakika hizo. Tunaendelea na Mheshimiwa Oran Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Nusrat Hanje wajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa hii fursa ya kuchangia hii Wizara muhimu. Nami napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara hii kwa kutuletea bajeti nzuri sana ya kilimo. Hii bajeti ya kilimo kwa kuiangalia kwa juu juu, itatuletea mapinduzi makubwa ya uchumi wetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nami napenda kuishukuru Kamati ya Kilimo, imetoa maangalizo mazuri sana ambayo naomba Mheshimiwa Waziri, ayafuatilie kwa ukaribu, la sivyo bajeti hii asipoangalia hayo maangalizo ya Kamati, inaweza isitekelezeke kama anavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo Kamati imeelekeza, ni kwa jinsi ya wataalam waliopo kilimo inaona kama hawajitoshelezi, lakini naona kama wataalam wanajitosheleza. Unapokuwa na *transformational budget* kama hii, inabidi lazima ubadilishe na *culture* ya watu utakaowakuta. Kwa vile kwa muda mrefu walikuwa hawajawahi kuona fedha nyingi kiasi hiki, sasa unapowapelekea fedha nyingi kiasi hiki, watashindwa hata namna ya kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ukiziangalia zinatokana na mkopo wa *IMF* ambao *wana discipline* kubwa katika matumizi ya fedha zao. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nina imani na taaluma yake kwa kiasi kikubwa, hebu aangalie kwa namna gani haya matumizi ya fedha za *IMF* ambazo ni za uhakika zitatuletea fedha nyingi zaidi? Naamini Sekretarieti yake, Katibu Mkuu wake, ni mtu

mwenye uwezo mkubwa sana; hebu mtumie vizuri, nina imani kuwa Wizara hii itabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea siyo ruzuku tu, mbolea ni namna ya uagizaji wa mbolea. Mwelekeo wa bei za mbolea sasa hivi haueleweki. Shilingi bilioni 150 zinaweza kusaidia, lakini hizi zitawapa matumaini wananchi. Mimi naona bado tunahitaji kuufumua muundo mzima wa mbolea. Mbolea haiagizwi kama kama tunavyokwenda sokoni, mbolea inatumia taasisi ambazo ninaimani Waziri anazifahamu kuna mambo yanaitwa *futures,* hygiene na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndiyo ambazo zinaweza kutusaidia kununua mbolea kwa wakati muafaka, wakati bei ni sahihi kwa nchi yetu. Kwa kuwatumia wafanyabiashara watanunua kwa bei kubwa watatuuzia kwa bei kubwa. Kwa hiyo, nchi ichukue jukumu la kuagiza mbolea yenyewe, aidha kwa kuwadhamini hao wafanyabiashara, tununue katika kipindi ambacho Brazil na zile nchi ambazo zinatumia mbolea kwa kiasi kikubwa haziagizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, jukumu la kuagiza mbolea lisiwe kwa walanguzi wafanyabiashara. Hawa ni *traders,* hawawezi kukusaidia. Hebu chukua jukumu wewe mwenyewe, weka miongozo, lakini hiyo iendane pamoja vile vile Shukuma kuwepo na Sheria ya Kilimo. *Transformation* kama hizi huwezi ukazitekeleza bila ya kuwa na sheria sahihi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, napenda kwenye kuongeza thamani za mazao; zao la pareto. Pareto inaweza kutusaidia kwenye viuadudu. Kwa kutumia kiwanda chetu cha Kibaha, pareto inaweza kusaidia kuzalisha viuatilifu. Sasa ni kwa nini tusiwe na mpango kabambe wa taasisi zetu za utafiti ifanyike haraka ili tuweze kukisaidia kile

kiwanda kiweze kuzalisha viuatilifu pamoja na mbolea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo jambo ni muhimu sana, litatusaidia, kwa vile pareto inayolimwa Tanzania, wengi hawajui, tunaongoza Afrika, ni wa pili duniani. Hii inaweza kutusaidia kutuletea fedha nyingi za kigeni na kuwasaidia wananchi ambao kwa sasa hivi wanalanguliwa sana kwa bei ndogo ya pareto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge hili, kwa hiyo, naomba kwa sababu Bunge hili tuliamini na tunaamini kuwa ni Bunge ambalo litajikita kwenye kilimo, kwa hiyo, tunaomba huo mwongozo ambao ulikuwa umeutoa tuendelee nao tuhakikishe kuwa kilimo ndiyo kinabebwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Constantine Kanyasu, halafu Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Luhaga Mpina wajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba pia nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, wanafanya kazi yao vizuri. Kwanza naunga mkono hoja na ninaipongeza Serikali kwa ongezeko la bajeti ambalo limefanyika mwaka huu karibu asilimia 255, lakini pia dhamira ya dhati ya kutaka kuleta mabadiliko kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijazungumza ninayotaka kusema, nataka nimkumbushe Waziri, mezani kwake kuna andiko la Ibanda *Irrigation Scheme,* ambalo lilikuja ofisini kwake mwaka 2021. Ni imani yangu kwamba utekelezaji wa mradi huu utaanza mwaka huu. Mradi huu sisi Halmashauri ya Mji wa Geita tumekubali kwa niaba ya wananchi kutoa

takribani Shilingi milioni 500 kusapoti Serikali ili mradi huu uweze kuanza. Kwa hiyo, tunaomba wasituangushe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka Mheshimiwa Waziri wakati *ana-wind-up* aniambie kuhusu *ginnery* ya Kasamwa na mkakati wa Serikali wa namna ya kuifanya ifanye kazi. Tunazo ahadi za takribani miaka sita, lakini tunaona hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, juzi nilitembelea Morogoro, palikuwa na Maonesho ya Kilimo. Naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nilikutana na wadau wake wengi. Nilikutana na *PASS* nikakutana na *TADB,* nikakutana na watu wanajiita *TACT* na wengine wanajiita *Tanzania Agriculture Trust Input Funds.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, nitatamani ajaribu kutuonesha mchango wa haya mashirika yake yote kwenye kilimo. Nilizungumza na watu wa *PASS* ambao wanamchangia mkulima asilimia 20 mpaka asilimia 60 na asilimia 40 benki, lakini mkulima huyu akienda benki, anakwenda kukutana na *commercial loans* ambazo *interests* zake siyo rafiki wa mkulima. Ukienda *TADB* wanakopesha mpaka *75 percent* halafu nyingine inayobaki ni ya kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ikawa, hivi hii *25 percent* kwa nini isitafsiriwe kwenye *value* ya *land* ya shamba ili nikiwa na heka zangu 100, hiyo *25 percent* wanipe *75 percent* kwa sababu tayari *value* ya *land* inaweza ikafidia hilo eneo. Sikupata majibu sahihi zaidi. Nilikutana na wengine wanaitwa *TACT (*Tanzania *Agricultural Catalytic Trust),* hawa ni *private firm* hawajulikani sana, lakini ukiwasoma ni kama vile *wame-centralize,* wako Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu hapa ni nini? Ukikopa leo Tanzania *Agricultural Development Bank,*

wakikupa mkopo, kwa sababu mkulima wa Tanzania analima kwa hali ya hewa, mwakani usiporejesha kulingana na *schedule* waliyokupa, watakutembelea, watakuuliza sababu, na *wata-restructure* mkopo wao, kwa sababu *interest* yao siyo kuuza. Pia katika kipindi chote watakupa ile *technical support* na kukutembelea na kukufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa uliyonayo kwenye *Agricultural Trust Input Fund,* wanajifungia ofisini, nami sijui kama huwa mnapima wamefanya nini kwa mwaka? Kwa sababu mimi sijawahi kuona wanachofanya. Wakikukopesha riba yamkopo wao wa Shilingi milioni 30, ni Shilingi milioni mbili labda, lakini mkopo ule ni wa miaka mitano. Shilingi milioni mbili ni kwa mkopo mzima, ni *interest*. Miaka mitano huyo mkulima kama *ali-delay* hapa katikati kulipa, utakuta *interest* ni Shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukashangaa, *interest* ya *principal* nzima ni Shilingi milioni mbili, *interest* ya kuchelewesha ni Shilingi milioni 15. Mkulima huyo unayemkopesha ni mkulima ambaye anakopa kwa kilimo cha kutegemea mvua. Matarajio yangu ni kwamba, kabla hujamwekea *interest* na kabla hujaenda kutangaza kutaka kuuza mali yake, umemtembelea, umeona mwaka huu ali-*plan* kupata gunia 100 hajapata, umefika pale umegundua kwamba hana sababu ya kutokurejesha, ni kilimo cha hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajaribu kufanya mabadiliko sasa hivi, mapinduzi makubwa ya kwenda kwenye *Irrigation Scheme,* lakini asilimia 95 ya wakulima wanategemea mvua ya Mungu. Sasa wewe unanikopesha mimi kwa mkataba wa mvua ya Mungu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** …mazao sikupata, unanipiga *fine.* Mimi nikanunue mvua wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri hawezi kufumua *Agricultural Trust Input Fund,* wanapoteza fedha za Serikali. Ni bora mwapeleke huko wakawe Mabwana Shamba au vinginevyo, hakuna kazi wanayoifanya kwa sababu hawam… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Tunaendelea na Mheshimiwa Nusrat Hanje, halafu Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Yahya Ali Khamis na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory wajiandae.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat, dakika tano.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kabla sijaanza, hii ni bajeti ya washikaji zangu, naomba niseme hivyo. Yaani hii Wizara ni ya wazazi, yaani kuna mzazi *one,* na mzazi *two,* wanajuana wenyewe Wizarani huko wanavyofanya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, kwa niaba ya vijana, kwa sababu ni miongoni mwa Mawaziri ambao sisi vijana tunajivunia, kwa hiyo, wanafanya vizuri, yaani mnafanya poa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kwa nini nasema hivyo kwamba wanafanya poa? Ni kwa sababu mwaka 2021 mimi nilichangia wakati tunajadili hii bajeti ya Wizara ya Kilimo na kuna vitu ambavyo nilivishauri hapa na vimefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tunaposema wamefanya poa, ni kwa sababu wako hatua moja mbele, wanafikiri tunavyofikiri. Yaani wanafikiri namna ambavyo Watanzania wanaamini kwamba sekta ya kilimo inastahili kupewa heshima inayopewa. Wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza kwa sababu kuna mambo wameyafanyia kazi. Jambo la kwanza, nilizungumza mwaka 2021 kwamba muda ambao vijana wetu wanakaa *field* ni mfupi sana, yaani kijana ili awe *ame-master* vizuri kabisa sekta ya kilimo akitoka Chuo, Waziri amezungumza kwamba wanafanya mikakati. Tunaamini, kwa sababu tutawauliza tena; wameongeza muda wa vijana kukaa *field* mpaka mwaka mmoja. Ni kitu kizuri, kwa sababu ninaamini wanajifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tulizungumza kuhusu ku-*miliaturize* sekta ya kilimo. Nilisema kwamba tunatamani, yaani kipenga kikipigwa Wizarani, Maafisa Ugani *(extension officers)* wanaitikia, mambo yanaenda. Wamefanya vizuri. Wasiwasi wangu, hawa Maafisa Ugani *(extension officers)* wako chini ya TAMISEMI. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI sekta zao ni tofauti, lakini hawa ambao Wizara ya Kilimo inatenga fedha nyingi na kuwapa vitendea kazi; na tulishuhudia pale, wamepewa vifaa vya kupimia udongo, wamepewa usafiri, wamepewa vitu vingi na ni kitu kizuri, na walikuja tukawaona lakini wako sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tumsaidie Mheshimiwa Waziri kuhamisha *extension officers* (Maafisa Ugani) warudi kwenye mikono ya Wizara ya Kilimo. Kwa sababu pale, mwenye uchungu na hizi fedha, kwa sababu tunasifia wote kwamba fedha ya kwenye Wizara ya Kilimo imeongezeka, lakini hatutaona tija, kama watu ambao tunaamini ndio askari

wetu hatuna *mandate* nao, yaani Wizara ya Kilimo haina *mandate* na Afisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe, pamoja na kwamba tunasema bajeti ya Wizara imeongezeka na tunajua imeenda kwenye umwagiliaji na sehemu nyingine, lakini ikumbukwe kwamba mpaka sasa hivi kwenye upande wa fedha za maendeleo, imetekelezwa kwa asilimia 35.86 tu upande wa miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, bado tunasisitiza kupelekwa kwa fedha tunavyopitisha kwenye Bunge hili, kwa sababu mikakati iko vizuri, tunaongea hapa sana lakini fedha hazipelekwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nichangie upande wa pili ushiriki wa vijana wa Taifa hili kwenye kilimo. Bado vijana wanajitahidi kwa kiasi kikubwa sana kupambana na kushiriki katika mnyororo wa thamani kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanalima, wanachakata, wanafanya kazi za *consultation,* wako vijana ambao wamejifunza masuala ya kilimo, wanashauri vijana wenzao. Kwa hiyo, tunashiriki kwa kiasi kikubwa, tunajitahidi kushiriki. Hata hivyo, bado tuna changamoto, kuna vijana wako *field* wana mashamba makubwa, wana *greenhouse,* wamejiandaa, wako tayari kushiriki kwenye mnyororo wa thamani katika sekta nzima ya kilimo lakini hawapati mikopo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongea Mheshimiwa Mariam Ditopile hapa, kuna watu kabisa wana kitu, yaani siyo kama labda anachukua mkopo ili akaanzishe, kuna wengine tayari walishaanza, wanatakiwa kuwa *boosted* tu, lakini ni hizo *bureaucracy* (urasimu) kupewa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ili vijana washiriki kwenye kilimo, tulisema tunataka tufanye kilimo kiwe *romantic*. Nafikiri

tunaelewana. Tukifanye kilimo kiwe rafiki, kwa sababu najua vijana ndio hao wa *millennials,* hutegemei aende akashike jembe la mkono alime. Sasa huwezi kuzungumza *ku-romanticize* kilimo halafu usizungumze kuhusiana na teknolojia na ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwenye Taifa letu tuna kituo cha kukuza ubunifu na zana za kilimo cha Arusha *CAMARTEC*. Hiki Kituo wametengeneza matrekta, mashine za kulimia, mashine za kupanda, wanajitahidi wametengeneza ziko pale, lakini kile Kituo hakina fedha. Hakijapewa fedha kwa ajili ya kuhamisha maarifa yao kupeleka kwa wakulima. Kwa hiyo, wametengeneza vitu vikubwa wamebaki navyo pale kituoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anatenga fedha kwa ajili ya kuwapelekea kituo hiki waweze kuhamisha ujuzi kutoka kituoni kupeleka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kumalizia… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi ya mwisho kabisa hiyo.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha za Benki ya Kilimo zimechukuliwa Shilingi bilioni saba. Mheshimiwa Waziri kuna watu walizungumza, nami naomba nisisitize; tunaomba majibu ya hizo Shilingi bilioni saba kwa sababu zilikuwa za mikopo, vijana wangepata mikopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje. Tunaendelea na Mheshimiwa Luhaga Mpina halafu

Mheshimiwa Yahya Ali Khamis, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory na Mheshimiwa Issa Mchungahela wajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Nimemsikiliza na nimesoma kurasa zote 277 za hotuba yake, zimesheheni mambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wakulima kote nchini, nawapongeza wakulima wangu wa Jimbo la Kisesa kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya uzalishaji mali. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amezungumza suala la kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika. Hili suala la kuanzisha Benki ya Ushirika ya Taifa halina tija yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, watu wa ushirika hawajakosa mahali pa kukopa. Tuna Taasisi nyingi sana za mikopo ambazo zinaweza zikatoa mikopo kwa washirika. Tunayo Benki ya Kilimo, unakwenda kuanzisha benki nyingine ya nini? Benki yenyewe hii ya Kilimo bado hatujaiimarisha, tunaenda tena kuanzisha benki nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, wanazungumzia urahisi wa kupata mikopo. Masharti na vigezo vinasimamiwa na Benki Kuu. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba eti washirika wakianzisha benki watapata mikopo kiurahisi ni nadharia, kwa sababu vigezo na masharti yote yanasimamiwa na Benki Kuu na yatakuwa ni yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, majukumu ya Vyama vya Ushirika ni mengi sana. Tumewapa jukumu la kufufua viwanda vilivyotelekezwa, tumewapa jukumu la kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora, kuwasaidia wakulima waweze kupata huduma ya afya ya udongo, kupambana

na magonjwa. Wanaliacha hili jukumu la msingi, wanakimbilia kuanzisha benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mfano, kuna Benki hapa zilianzishwa kwa mbwembwe nyingi, matokeo yake benki hizo tumeenda kupata hasara kubwa, benki zikafungwa, fedha za Watanzania zimo humo ndani. Kwa mfano *Bank (M)* iko wapi? *Twiga Bank* iko wapi? Benki ya Wanawake iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa hayo hayo, leo tunaenda kuanzisha Benki tena za mfano huo huo. Hata kidonda hiki bado hakijapona, Benki Kuu bado wanalitatua hili tatizo, hatujamaliza kulitatua, leo Waziri unaenda kuruhusu kuanzisha Benki nyingine, kwa ajili ya jambo gani? Benki Kuu nanyi mmekubali kuanzisha hii Benki wakati tunayo Benki ya Kilimo? *Duplication* hizi ni za kazi gani? Mnataka kuzichukua fedha za wananchi ambazo zingeweza kuwasaidia wananchi, ziende zikagawanywe huko kujenga majengo na mambo mengine wakati wakulima wana shida kubwa hapa! *(Makofi)*

Benki Kuu na ninyi mmekubali kuanzisha hii benki ilhali tunayo ya kilimo, *duplications* hizi za kazi gani? Mnataka kuzichukua fedha za wananchi ambazo zingeweza kuwasaidia wananchi ziende zikagawanwe huko kujenga majengo na mambo mengine ilhali wakulima wana shida kubwa hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la mbolea. Wenzangu wanezungumza hapa, upandishaji wa bei za mbolea, narudia kusema mfumuko bei za mbolea zetu ni wa kutengenezwa. Waziri amekuja hapa ameshindwa kusema utatuzi wa bei za mbolea zilizotengenezwa. Moja, kwa wafanyabiashara wametengeneza, bei za mbolea zimepanda, urea hapa imetoka 50,000/= imeenda mpaka

110,000/= mpaka 150,000/= kwa maeneo mengine, lakini ukiangalia kwa undani hizi bei zimetengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninasema, na hasa takwimu ambazo wanazo Serikali waziangalie. Kwa mfano Waziri anaposema kwamba, bei za mbolea zimepanda katika soko la dunia, bei ya urea imepanda kutoka dola 251 mpaka dola 1,214; kwa maana hiyo katika soko la dunia unataka kutuambia kwamba, bei ya mbolea ya urea kwa kilo 50 imepanda kutoka 28,000 mpaka 139,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hizo ndizo takwimu mnazotuambia, kama katika soko la dunia mbolea ya urea ya kilo 50 inauzwa kwa bei ya 139,000/= utaiuza kwa bei gani hapa? Kwa hiyo, hizo takwimu zenyewe sijui ni *source* gani na sijui kama Serikali wanajiridhisha na takwimu hizo, zinatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu ni Serikali na Wizara hii ya kilimo; waliamua kufuta utaratibu wa *bulk procurement system.* Badala ya kutatua matatizo yaliyokuwemo kwenye *bulk procurement system* wakaenda kuiondoa *bulk procurement system* ili kufanikisha njama za wafanyabiashara wachache waliokuwa wamepanga njama za kuja kuwaongezea wakulima bei za mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri atuambie toka walivyoondoa mfumo wa *bulk procurement system* mwaka 2021, Juni, bei za mbolea zilianza kupanda palepale, hata kabla ya vita ya Ukraine ambayo ndiyo inayozungumzwa hapa bei za mbolea zilianza kupanda kwa kasi bila usimamizi. Kwa hiyo kuna usimamizi dhaifu katika jambo hili. Na kwa uthibitisho hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe anakiri kwamba wale *TFRA* walipoenda kufanya ukaguzi walienda kukuta mambo ya ajabu, wakakuta mbolea zinauzwa zikiwa hazijasajiliwa, hazina vibali, ziko wazi na vilevile kulikuwa na zilizokuwa na uzito wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanathibitisha kwamba, hakuna usimamizi thabiti katika hili eneo la mbolea na kusababisha wananchi kwenda kuuziwa mbolea kwa bei kubwa sana. Halafu sasa mfumo tumeutengeneza sisi wenyewe nab ado kuna nchi jirani zetu ambao wanauza mbolea chini. Wanatumia Bandari ya Dar-es-Salaam, wanasafirisha mbolea na bado wanaenda kuuza huko kwa bei ya chini; kwa nini sisi hapa bei yetu hapa iko juu? Na haya yote tunayokubali na tumeyatengeneza sisi wenyewe Wizara ya Kilimo halafu tunatoka tunasema kwamba, eti bei ya mbolea tunamfumuko wa bei ya mbolea kwa bei ambazo tumezitengeneza wenyewe? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha Mheshimiwa, nilikupa umalizie tu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema hapa…

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** … ni majonzi makubwa sana kwa Taifa letu, tunatengeneza mfumuko wa bei sisi wenyewe.

**MWENYEKITI:** Muda wake umekwisha Mheshimiwa, anamalizia sentensi yake ya mwisho.

**MHE. LUHAGA J. MPINA: …**leo hii tunatenga fedha trilioni 150 kwa ajili ya kwenda kuweka ruzuku, unaenda kuweka ruzuku kwenye bei iliyotengenezwa?

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** … fedha hizi za Watanzania bilioni 150 ziende kwenye bei ya halisi ya mbolea. Wizara ya Kilimo ihakikishe kwamba inaenda kuondoa makandokando yote yaliyosababisha bei za mbolea kupanda… *(Makofi/kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Luhaga Mpina ahsante. Mheshimiwa ahsante sana.

Waheshimiwa jitahidini, dakika tano ni kidogo naelewa, lakini naomba muweke *point* muhimu kama wengine ambavyo wameweza kuchangia. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Ali Khamis, Mheshimiwa Kavejuru Eliodori, Mheshimiwa Issa Mchungahela, Mheshimiwa Yustina Rahi na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe wajiandae.

**MHE. YAHYA ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya mwanzo, namshukuru Mwenyezi Mungu. Pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama katika Bunge hili Tukufu, pia namshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mama yetu Rais wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa safari ya Dubai na kwa safari ya Marekani. Safari hizo zimefungua milango kwa Tanzania. Leo ukizunguka duniani Tanzania watu wanaielewa vizuri kwa mambo mazuri yanayokuja kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde, Katibu na wengine katika Wizara ya Kilimo kwa kuweza kuleta mambo mazuri katika nchi yetu kwa mwelekeo huu wa bajeti unaokuja. Tunajua kwamba sasa Tanzania inafunguka kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika ni kidogo lakini nilikuwa nataka dakika 10 leo mimi kwa sababu leo nina mambo mahususi. Nina mambo maalum, nina mambo mahususi na muda maalum ya kuchangia kwa siku ya leo. Kwa mara ya mwanzo kabisa kuchangia katika Bunge hili dakika tano ni kidogo kwa sisi watu wa darasa la saba. Ilikuwa leo unipe kama dakika 10 hivi nichangie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya kwa kuwa ni mara yako ya kwanza nakuongezea dakika mbili, utumie dakika saba vizuri. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Tanzania tuna fursa kubwa ya mambo ya kilimo, tuna mashamba makubwa kwa ajili ya kilimo, lakini mashamba yale hayaendani na mfumo wetu wa kilimo cha sasa. Mashamba yale yamekuwa ni mashamba yapo tu, lakini mashamba ambayo hayaendani na kilimo tunachokwendanacho sasa. Na mashamba haya nitayataja; kwa sababu, mashamba kama yanafanya vizuri tutayataja na kama mashamba yanafanya vibaya tutayataja kwa sababu ni mali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba la mwanzo ambalo linafanya vibaya haliendani na mambo yetu ya kilimo ni Shamba la Madibila Kapunga. Shamba la pili ni shamba la Madibila. Shamba la tatu linakwendakwenda kidogo, la Ubaruku, linakwendakwenda kidogo. Mashamba mengine ni; *West Kilimanjaro,* Kilombero Morogoro, Dakawa Morogoro, Njombe, Kagera pamoja na Ruvu Mkoa wa Pwani. Mashamba haya hayaendani na wakati. Naiomba Serikali iwe karibu na mashamba yale kama kweli tunataka kuleta mfumo wa kilimo cha kisasa cha umwagiliaji ni lazima mashamba yale Serikali iwe karibu na iyasimamie kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama huyu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefungua mipaka kwa ajili ya wawekezaji ili Tanzania tupate mafanikio. Sasa nikawa ninajiuliza Wabunge wanasema kwamba, mama anaupiga mwingi? Hili neno hili ikawa mimi nalitafsiri hii kuupiga mwingi ni nini? Lakini baadaye nikajua kumbe kuupiga mwingi ni uvumbuzi wa mambo. Ukae, upeleke akili yako ufikiri, ili ujue nini utasaidia Watanzania. Sasa kama tafsiri ni hiyo kwamba, mama anaupiga mwingi ni mvumbuzi basi na mimi namwambia leo Mheshimiwa Bashe kwamba, leo; mara ile nilimuona amevaa *combat* na mimi namwambia Mheshimiwa Bashe lile *combat* moja anipatie. Anipatie *combat* ili na mimi ni niwe mvumbuzi kwenye kilimo. Na kwa sababu tulimsikia siku ile mama anamuelekeza Mheshimiwa Bashe, kwamba na mikoa ya pwani ipate skimu kwa ajili ya mashamba ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uvumbuzi wangu na mimi nimezunguka Mkoa wa Pwani, kata baada ya kata na kijiji baada ya kijiji. Nimekwenda kwa baskeli, kwa miguu na mvua yangu; naanguka na pikipiki, lakini kwa sababu tunataka tumsaidie mama huyu anaupiga mwingi na sisi Wabunge tuupige. Tuzunguke katika mikoa yetu kila mahali ambapo tutajua kwamba, kuna vyanzo vya maji basi tupeleke mashamba kwaajili ya umwagiliaji. Hiyo ndiyo tafsiri yangu ya kuupiga mwingi, sasa na mimi nimeupiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda katika Kijiji kimoja kinaitwa Maparoni kina eka 10,000. Nimekwendsa katika Kijiji kimoja kinaitwa Kwasalie kina eka 12,500. Nimekwenda katika Kijiji kimoja kinaitwa Msalala kina eka 7,000. Nimekwenda katika shamba moja Mbuchi A lina eka 8,200. Nimekwenda katika Kijiji kinaitwa Mbuchi B kina eka 4,600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni mashamba ambayo kama tutapeleka skimu tukafanya mashamba ya umwagiliaji,

basi Mkoa wa Pwani tunaitengeneza Mbarali nyingine. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa Bashe aanze na mashamba ya Mkoa wa Pwani na huko tutapata mashamba mkakati kwa ajili ya kupeleka mashamba ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona dakika saba sitazifika kwa leo, naomba nimuachie mwenzangu. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Ali Khamis. Hongera sana, kwa mara ya kwanza kufika dakika hizo ulizofika. Waheshimiwa Wabunge kuongea kwa mara ya kwanza si jambo rahisi sana. Tumpongeze sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Kavejulu Eliedori, badaye Mheshimiwa Issa Mchungahela na Mheshimiwa Yustina Rahi wajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipa. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Bashe Waziri wa Wizara ya Kilimo na watendaji wakuu wote wa Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma hotuba hii ya kilimo ukurasa ule wa 83, nimejiuliza, na umezua manung'uniko makubwa sana kwa sisi wakulima wa kahawa. Mazao ya korosho, pamba na tumbaku ni mazao ya kimkakati sambamba na zao la kahawa. Haya matatu yana ruzuku, lakini zao la kahawa halina ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika mauzo ya nchi, zao la kahawa kwa muhula uliopita limetuingizia Tanzania Dola za Kimarekani milioni 142, tumbaku milioni 90. Tumbaku ina ruzuku, lakini zao la kahawa ambalo linatuingizia fedha nyingi za kigeni halina ruzuku. Ninaleta kwako

manung'uniko makubwa sana ya wakulima wa kahawa kutoka katika Mkoa wa Kagera, Ruvuma, Songea, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha, Kigoma, Mara, Tanga, Njombe, Iringa, Manyara, Katavi, Morogoro, Mwanza, wanaomba ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii Serikali inatakiwa iwe na *will*. Haiwezekani kabisa tukalia miaka yote. Ukilinganisha na nchi zinazolima zao hili la kahawa, ukiangalia Uganda ambayo kila mwaka inauza tani 389,000 na Ethiopia ambayo inauza zaidi ya 457,000 uzalishaji wao unaongezeka, lakini sisi unadorora, sababu kubwa ni kuwepo kwa manung'uniko kutoka kwa wakulima wa kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mapendekezo yangu ili hakika kabisa kuwepo na mapinduzi makubwa katika uzalishaji wenye tija wa kahawa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja. Serikali iweke mipango madhubuti ya kuendeleza zao la kahawa. Mpaka sasa hivi hakuna mipango chanya yoyote ile ya kuendeleza zao hili la kahawa ambayo inaonekana licha ya kutupatia fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Kipaumbele kiwekwe kwenye uzalishaji wa mbegu bora na miche bora. Sisi Tanzania kwa takwimu iliyopo kila mwaka tunazalisha miche bora milioni 20, wenzetu wa Uganda kila mwaka milioni 124, tuongeze ruzuku hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. KAVENJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaomba angalao hata dakika mbili. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umemaliza muda. Sentensi yako ya mwisho imeeleweka, nimeikatiza kwenye sehemu inayostahiki.

**MHE. KAVENJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Mchungahela, Mheshimiwa Yustina Rahi na Mheshimiwa Saasisha, badaye atafuata Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nijielekeze moja kwa moja katika uchangiaji wa hotuba kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, kilimo ni uti wa mgongo kama ilivyoanza kusemwa hapo mwanzo. Kilimo ni chakula, watu tunaishi kwa sababu ya chakula cha kilimo, lakini kilimo ni biashara. Takribani asilimia kubwa ya biashara yetu ya ndani na ya kimataifa inategemea sana kutoka kwenye mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uchumi. Takribani asilimia 30 ya Pato la Taifa inachangiwa na mazao kutoka kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni ajira. Takribani asilimia 70 ya ajira zote za Tanzania zinachangiwa na kilimo. Katika hali kama hii hakuna njia yoyoye tunaweza tukapishananacho kilimo. Tunatakiwa kwa nguvu zote tuwekeze kwenye kilimo ili kuhakikisha kwamba, uchumi wetu unakua, lakini unakuwa imara. Nchi zote zilizoendelea ni kwa sababu, zimefanya mapinduzi ya kilimo na kwa kupitia

mapinduzi ya kilimo ndipo unaweza ukaenda kwenye mapinduzi ya viwanda kwa sababu, viwanda na kilimo vinategemeana; kwa nini? kilimo chenyewe kinakuwa ni malighafi ya kiwanda, kwa hiyo huwezi kuzungumzia suala la kiwanda kama kilimo hakiko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka na mipango iliyowekwa kwenye kilimo na Mheshimiwa Waziri na timu yake, ameweka mipango mizuri kabisa. Shaka yangu ni jinsi mtiririko wa fedha kutoka kwenye vyanzo hivyo; kwa maana ya vyanzo vya bajeti kwenda katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi, muhula uliopita wa bajeti kilimo katika eneo la umwagiliaji kwenye suala la maendeleo kiliwekewa kiasi cha takribani bilioni 46.5, lakini cha kushangaza mpaka Februari mwaka 2020/22 imepelekwa milioni 590 pekee, hivyo kufanya asilimia 1.27 pekee katika suala la maendeleo la umwagiliaji, hasa ukizingatia kwamba umwagiliaji ndilo dira na umwagiliaji ndiyo maamuzi sahihi ya kufufua kilimo na kufanya kiwe bora. Sasa kwa mtindo huo sioni kama kweli tunaweza tukafikia lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hapo naomba nijielekeze mchango wangu katika kilimo cha nyumbani kwetu; kwa maana kilimo pendwa. Kilimo cha mazao pendwa, mazao ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hapo, naomba nielekeze mchango wangu katika kilimo cha nyumbani kwetu kwa maana ya kilimo pendwa, kilimo cha mazao pendwa cha mazao ya korosho. Korosho limekuwa ni zao pendwa, kadri siku zinavyoongezeka limekuwa zao mahsusi kabisa katika matumizi ya shughuli mbalimbali katika dhima za kitaifa na za Kimataifa. Kwa maana hiyo hata wanunuzi wa korosho wamekubali wenyewe kabisa kuwa na

hiari kutoa bei nzuri kabisa katika korosho, lakini cha kushangaza ni kwamba bei hii haimfikii mkulima. Kwa maana hiyo Waziri pamoja na timu yake kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba bei halisi inamfikia mkulima ambaye ni mvuja jasho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojaribu kuzungumzia tatizo kubwa la bei linatokana sana katika maeneo mawili, eneo la kwanza ni kwa sababu korosho zinauzwa ghafi huko India pamoja na nchi nyingine za Mashariki. Pia korosho zimezingirwa na wadau waliokosa weledi. Wadau wengi waliozingira kwenye korosho wamekosa weledi kwa namna moja au nyingine. Wako kwa mfano wafanyabiashara ambao wao kwao faida ndiyo msukumo pekee kwenye biashara hii au kwenye sekta hii. Halikadhalika wapo madalali ambao wao wamekaa kwa ajili ya kuwanyonya wakulima na wala hafanyi jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba korosho zinakuwa zao lenye tija kwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango huo.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Yustina Rahhi. Mheshimiwa Saashisa Mafuwe, Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Anastazia Wambura wajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo. Nitakuwa mchache wa shukrani, wa fadhila kama sitatambua na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama Samia Suluhu

kwa kuiheshimisha nchi ya Tanzania na kuwaheshimiwa wakulima wa Tanzania kwa kuweka bajeti hii ya kihistoria mwaka huu. Nampongeza pia Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa tatizo kubwa katika kilimo ni uzalishaji mdogo kwa eneo na uzalishaji huu mdogo unasababishwa na upungufu au ukosefu wa pembejeo za kilimo zikiwemo mbegu, mbolea pamoja na viuatilifu. Tunafahamu kabisa ikifika wakati wa msimu upatikanaji wa mbegu unakuwa wa shida kabisa na zikipatikana bei yake inakuwa juu na wakati huo ndiyo wakati ambapo wakulima wanakimbizana na unyevunyevu wa mvua. Naomba kuishauri Serikali kwa bajeti kubwa iliyoipata ya uzalishaji wa mbegu, mbegu nyingi tuzizalishe huku Tanzania, tupunguze mbegu tunazoziagiza kutoka nje ili wakulima wetu waweze kumudu bei ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile watu wameongea kuhusu bei ya mbolea, tunafahamu changamoto tulizozipata kipindi kilichopita, lakini mwarobaini wa tatizo hili ni kuwa na viwanda vyetu wenyewe huku ndani, hatuwezi ku-*control* bei ya mbolea tunazoagiza kutoka nje na ruzuku iwekwe katika viwanda vinavyozalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kuchangia kidogo kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Tuna fursa kubwa sana katika kilimo cha umwagiliaji. Tuna maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji, *potential area* zaidi ya hekta milioni 29 na pointi, lakini japokuwa sasa hivi tumeweza kuendeleza hekta kwenye 700,227 na lengo la kwenda kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ni hekta 1,200,000. Bado eneo hili ni dogo na Serikali haiwezi kufanya kila kitu, naomba kuishauri kwamba, Wizara ikaweke fursa katika eneo hili ili kuwahamasisha wawekezaji waweze kuweka mchango wao katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hiki ndiyo kilimo ambacho nategemea kitajenga mazingira mazuri kwa vijana, kiweze kuwafanya vijana wawekeze katika kilimo cha umwagiliaji kwa sababu anaweza kupata mapato mapema zaidi hata kuanzia wiki tatu, mwezi au miezi miwili. Hapo vijana watapata kipato kutokana na kilimo cha umwagiliaji. Nimeona mpango wa Wizara unaoitwa *National Strategy for Involvement of Youth in Agriculture,* mahali hapa nategemea Wizara itawatafutia vijana mashamba kwa kufidia maeneo na kuweza kuwakodisha vijana ili waweze kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea pia katika bajeti hii kubwa iliyowekwa kwenye kitengo hiki cha umwagiliaji wataenda kuchimba mabwawa na kuvuna maji ya mvua ambayo mara nyingi yanasababisha mafuriko, vile vile kwenda kuboresha miundombinu. Kuna miradi mingi ya mabwawa ambayo yameshachimbwa ambayo bado ufanisi wake haujawa mkubwa kwa sababu ya kutokuweka miundombinu ya kupeleka maji katika mashamba na mifereji mingine tunajua inapoteza maji. Kwa hiyo mifereji hiyo pamoja na miundombinu ingesakafiwa na kutengeneza miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kule Manyara, Mradi wa Bwawa la Dongobesh umekamilika lakini hauna miundombinu ya kupeleka maji mashambani. Naomba uwe mmojawapo pamoja na kuchimba mabwawa. Naomba bwawa ambalo limewekwa katika mpango wa Mheshimiwa Waziri, Bwawa la Dawi, lipate kuchimbwa. Vile vile kuna wakulima wanapenda kilimo cha umwagiliaji lakini mashamba yao yako juu ya mifereji wanatumia *pump* na *generator* kumwagilia mashamba yao. Niiombe Serikali kabisa kwa nia njema waweze kutoa kodi kwenye vifaa hivi ili wakulima wengi waweze kununua *pump* hizi na waweze kumwagilia maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kidogo, kwa sababu tumepata bajeti hii kubwa ya kihistoria, katika ufanisi naomba kushauri tu kwamba, Wizara iajiri watendaji wa kutosha, kwa mfano, Wahandisi wa Umwagiliaji kule kwenye halmashauri hawapo na ndiyo wanaoenda kusimamia miradi hii. Vile vile kuna vitengo kwa mfano Kitengo cha *Agro-mechanization* ambacho kilikuwepo, wale waliokuwepo baada ya kustaafu Serikali imeacha kuwaleta watu hawa, ndiyo maana wakulima wanabaki kwenye kilimo cha mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wamenunua trekta zilizoharibika, hakuna mtu wa kuwashauri. Kuna *power tiller* tulihamasisha, wakulima wana ma-*power tiller* yameharibika hakuna mtu wa kuwasaidia. Kwa hiyo katika ajira ijali tusiangalie tu labda pengine ma-*agronomist,* kuna vitengo hivi vya *agro mechanisation,* kuna wakulima bado wanalima kwenye miteremko mikali, lakini kulikuwa na washauri, hawa watu wa *land use,* tunaomba tu Wizara ikaangalie hivyo vitengo muhimu ili kwenda kuwasaidia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha, tayari kengele imepiga.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi. Tunaendelea na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Anastazia Wambura wajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Kwanza nianze kwa kumpongeza

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kama vile lile alilolifanya hivi karibuni, watumishi wa umma wanashukuru sana kwa ongezeko la mishahara, lakini na kima cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba bajeti iliyopita ya Kilimo, mwaka wa Fedha uliopita, nilisimama hapa nikasema sitampongeza Waziri mpaka pale atakapomaliza matatizo yaliyoko kwenye ushirika. Sasa kwa kuwa ameshaanza kumaliza matatizo yaliyoko kwenye ushirika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na wananchi wa Jimbo la Hai wanampongeza, si tu kwenye ushirika lakini kwenye mambo makubwa aliyoyafanya ndani ya Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hakika anaitendea haki Wizara hii, tukimsikilizam tukiona matendo yake na namna anavyoenenda anafanya vizuri sana, ashikilie hapo hapo, imani ambayo Mheshimiwa Rais amempa kwenye eneo hili ana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko afanye kazi hiyo, nampongeza sana. Nampongeza pia kwa kuwa ameamua kwenda kutengeneza *common use facility* pale Hai, tunamshukuru sana. Nimeona humu kwenye hotuba ametuwekea fedha kwenye skimu, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme hili, kwenye ushirika tuna matatizo makubwa sana. Tunamshukuru kati ya vyama 40 vilivyoko Siha na Hai vyama 20 ameanza navyo na kwenye vile vyama vyama viwili amefuta mikataba yao, namshukuru sana. Hii ilikuwa changamoto kubwa sana. Hata hivyo, nimwambie nampongeza kwamba, ameweza kuvuka hila za hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, katika eneo ambalo lina matatizo katika nchi hii ni ushirika, lakini Mheshimiwa Waziri huyu ameweza kuruka hila zao. Kitendo cha kukubali na kuvunja

mikataba ile najua ameruka hila za watu wa ushirika na ameungana na wananchi wa Jimbo la Hai, namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, yale mashamba ambayo tumevunja mikataba, sasa tunaanza utaratibu upya wa kutengeneza mikataba mipya yenye tija, ikiwemo na Shamba la Makoa. Lile Shamba la Makoa najua Waziri anavyosumbuliwa, ameshapewa barua lakini bado anahangaika mtaani. Nimwambie tu Mheshimiwa Waziri, yule mwekezaji pale amekaa miaka mingi, hakuna alichokifanya, ametutia hasara, tumeshaamua, ushirika wenyewe wamepiga kura wakasema aondoke, nimwombe Waziri, aondoke kweli kweli. Najua anapita huku na huku kwenda kwa viongozi wakubwa kubembeleza arudi, sisi watu wa Hai hatumtaki, labda kwa kifupi wamwambie tu kwamba hatumpendi kwa sababu amerudisha maendeleo yetu nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka sasa hivi, katika lile eneo tutafute mtu anayeweza kutufanyia biashara pale, sisi tulienda anafanya ufugaji pale, Halmashauri ya Wilaya ya Hai haipati chochote, haajiri pale kwetu, hatuna tunachonufaika nacho. Tulienda pale na Waziri wa Maliasili na Utalii akiwa na viongozi wake wakuu hakuna chochote, mikataba iliyoko pale ni ya hovyo, yule pale ni dalali. Kama tunataka mwekezaji, basi awe ni mwekezaji mwenye tija, aje pale kwa ajili ya kufanya biashara ambayo ina tija kwa Halmashauri ya Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri pale tumeshatengeneza *business plan* ambayo itatusaidia. Pale kuna biashara ya utalii, biashara ya kuuza vitu vya utalii, lakini kuna kilimo mle ndani na bahati mbaya sana ameua kinu chetu cha kahawa pale, lakini bado anaendelea kung'ang'ana anataka kurudi na kuzunguka huku na huku, hatumtaki, pamoja na wapambe wake.

Mheshimiwa Waziri ni kwa sababu tu amenipa hela nyingi, nilikuwa nimejiandaa kweli kumwonyesha vitu ambavyo anafanya visivyofaa pale, ila kwa sababu ametupa hela nyingi na yeye anatusikiliza narudisha hapa. Hata hivyo, ujumbe wetu, hatumtaki, tutatafuta utaratibu mwingine wa kupata mwekezaji tuendelee pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nizungumze hivi, hivi vyama vya ushirika vinapata shida lakini ipo Taasisi ya Uchunguzi na Ukaguzi, hawa watu wanatusaidia jambo gani? Wanakagua kitu gani? Niombe wapewe fedha ili wafanye kazi yao, waende wachunguze vyama hivi, wamefanya uchunguzi, Mheshimiwa Waziri kwenye taarifa yako unasema, kuna hati mbaya Tanzania nzima 1,729, wanachukua hatua gani? Kama kuna sheria ina upungufu, iletwe hapa ifanyiwe marekebisho ili tuwape meno, waweze kusimamia matatizo yaliyoko kwenye ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza watu wa Hai, ugomvi na ushirika umekwisha kabisa, viongozi wangu wa ushirika tunasikilizana, tunazungumza lugha moja sasa hivi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saashisha kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Amandus Chingwile wajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, najua dakika tano ni chache sana nitaongelea mambo mawili. Suala la kwanza ni masoko ya kibiashara ambayo hayo masoko Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukieleza sana watu wa Mkoa wa Kagera. Nimeangalia kwenye taarifa ya Waziri sijaona amesema nini. Hayo masoko ndiyo biashara kubwa, hayo masoko ndiyo

kiunganishi tunachokitegemea ili tukafanye biashara. Masoko yako Nkwenda, Mrongo na pia Mtukura. Hayo masoko yamejengwa kwa fedha za mikopo, lakini pia na Serikali, sasa kuyatelekeza haina maana ina maana hakuna *value for money*. Naiomba Wizara hii na Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi, hebu aseme neno moja na watu wa Mkoa wa Kagera ili wapone. Kwa hiyo hilo ni suala la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hayo masoko ninayoyaongelea yana uhusiano sana na biashara tunayofanya. Sisi ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya ndizi, leo tunavyoongelea biashara kubwa ya ndizi zinaelekezwa Uganda. Nakumbuka wakati fulani nilimpigia simu Mheshimiwa Waziri nikitaka atatue mgogoro wa wafanyabiashara wa Murongo na wafanyabiashara wa Uganda kuhusu ununuzi wa ndizi. Tulipata *solution* kwamba ndizi ziweze kuuzwa eneo la wazi pale Mrongo, chafu limechakaa, lakini sasa tukiwa na hayo masoko tutaweza kufanya biashara nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndizi ni *asset* kwa Uganda kwa sababu wanasafirisha nje. Ukienda kwenye Mataifa mbalimbali unakuta ndizi *produced* from Uganda wakati *in reality* zinatoka Kagera, ni ndizi za Kagera zinavushwa zinaenda kupandishwa hadhi na kuuzwa nje ya nchi. Kwa hiyo naomba sana hayo masoko yapewe umuhimu ili tuweze kuweka tija katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kama walivyoongea wengine kuhusu zao la kahawa. Nilikuwa nasoma *journal* moja wamesema ni *journal business insider Africa,* wanasema baada ya maji na chai kinachofuata kwa kunyweka zaidi ni kahawa. Kwa hiyo kuna fursa nzuri ya biashara tukiwekeza vizuri kwenye kahawa. Nimeangalia nikafanya *study* tu kwamba tumeweza kuzalisha tani 65,000 *it is a peanut,* lakini leo tunakuwa na malengo ya kuzalisha tani 72,000, *its still small,* kwa Mkoa wa Kagera tu ukiangalia wana

uwezo wa kuzalisha zaidi ya hekta milioni moja, lakini eneo linalozalisha ni hekta 600,000, lakini siyo hiyo kahawa tu, wanazalisha *less than* hekta 48,000. Kwa hiyo unaona kwamba maeneo makubwa hayajaweza kuzalisha vya kutosha bado tuna *potential* ya kuzalisha zaidi kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnadhani kwa nini watu hawapendi kuzalisha kahawa kwa wingi, kuna wakulima takriban 130,000 kwa Mkoa wa Kagera, ni wachache sana kwa sababu eneo la Mkoa wa Kagera linaweza kuzalisha zaidi kwa jinsi *nature* yake ilivyo. Watu hawazalishi kwa sababu ya rasimu kwenye biashara ya kununua na kuuza kahawa. Niishukuru ofisi yao kupitia Waziri Mkuu, leo wanatangaza biashara ya kahawa itapata uhuru wa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia ameongelea minada na bado nabaki hapa kwenye swali langu, bado tumejiridhisha kiwango gani kwamba wale wanaokuja kununua kwenye minada hawataweza kuwa na maswali ya *price fixing*. Kwa sababu hilo pia lipo, wanaweza kuwa wamepanga wakaja watu 10, wameshaweka idadi au kiwango wanachotaka kununua, kwa hiyo *automatic* mkulima ataumia. Kama hatutapata fedha nzuri ya kuuza kahawa, wasidhani kwamba tutaongeza uzalishaji wa kahawa. Watu watatelekeza kahawa, wamekuja kwetu, namshukuru Naibu Waziri alikuja akagawa miche zaidi ya milioni mbili kwa Mkoa wa Kagera, Kyerwa…

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa

## T A A R I F A

**MHE. SAASHISHA. E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa pamoja na mchango wake mzuri na maelezo yake na faida za kahawa, lakini nataka kumpa taarifa kahawa hiyo haijapewa ruzuku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nimeipokea na niongezee hapo hapo. Nimem-*quote* mkulima mmoja anasema unaweza ukapepeta ukaweka kahawa kwenye magunia, lakini bei inavyokuja hairidhishi. Kwa hiyo *automatic* kama bei ya kahawa haiwezi kuridhisha, mkulima ata-*ignore* biashara ya kahawa. Kila siku tutakuja tunatoa mifano mizuri ya Uganda, leo ameeleza Mbunge mmoja hapa, Uganda leo ina *rank, the second in Africa* kwa kuzalisha kahawa wakati kahawa inatoka Mkoa wa Kagera, siyo sawa, *which means* kuna shida kwenye soko letu. Tuna shida katika kuendesha masoko na ununuzi mzima wa kahawa kwenye eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuomba sana kwamba mfumo ambao nimeona na mwongozo wameweka wausimamie vizuri, tuone kama utaleta tija. Kuna madalali wanaumiza sana wakulima, lakini hatuwezi ku-*avoid,* tutengeneze mfumo madhubuti ambao hawa madalali hawatawaumiza wakulima. Pia walipwe kwa wakati, *first come first save*. Mkulima anaweza kupima mazao yake leo akaja kulipwa baada ya wiki tatu, yule anayelipwa wa kwanza ni yule anayetoa chochote. Wakiweza kusimamia hiyo mifumo, tunaweza kuleta mabadiliko kwenye soko la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia kwa kutumia muda wako vizuri. Tunaendelea na Mheshimiwa anastazia Wambura, Mheshimiwa Amandus Chingwile na Mheshimiwa John Salu wajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nimshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa rehema zake. Nianze mchango wangu moja kwa moja kwa suala zima la ukuaji wa kilimo katika nchi yetu. Suala la ukuaji wa kilimo limekuwa gumu kwa muda mrefu na niseme tu sababu kubwa sana ambayo imechangia shida ya ukuaji wa kilimo ni kuongeza maeneo ya kilimo, lakini hatuangalii vizuri suala la *productivity* ambalo ni *production per unit area*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia pia hapa Serikali au Wizara ina mpango wa kuongeza eneo la umwagiliaji na niombe sasa kwa kuwa bajeti imeshaongezeka ijikite zaidi kwenye suala la *productivity* kwa sababu kwa bajeti hii sasa tunaweza kuwa na mbolea na tumesikia pia tutakuwa na mbegu bora, huduma za ugani zimeshaimarishwa na kadhalika. Kwa hiyo niombe Serikali sasa ijikite kwenye *productivity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye utoshelevu wa chakula. Tumesikia mara kadhaa kwamba kuna dalili kwamba Bara zima la Afrika litakuwa na shida ya utoshelevu wa chakula, lakini sana kwa upande wa kwetu ngano tunaona kwamba ina upungufu mkubwa na kwa takwimu tumesikia kwamba mahitaji ya ngano katika nchi yetu ni tani milioni moja na wakati huo huo sisi tunazalisha tani 70,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunaona kabisa kwamba hapa tunahitaji kuagiza ngano nje lakini mimi sikubaliani sana na hili suala la kuagiza ngano nje. Kwanza tunao hawa waagizaji wa ngano, tunaweza tukawatumia hawa hawa, tukawawezesha tukawapa maeneo, tukawapa *extension services* wakazalisha ngano, hata kama haitafikia hiyo tani 1,000,000 Watanzania sasa tubadili mitazamo yetu tuna chakula cha aina nyingi sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi niwapongeze wale Watafiti ambao wamefanya utafiti na kuboresha viazi wakatengeneza viazi lishe wamevifanyia *Biofortification* sasa hivi unaweza ukapata keki nzuri sana kutokana na unga wa hivi viazi, ukapata maandazi na ukapata pia *biscuit* kutokana na hivi viazi, ninaomba tutumie pia mazao yetu. Tuna mazao ya aina nyingi sana tunayo mihogo, tunayo viazi mviringo, tunayo magimbi, tunao mchele tunapata pia hata mkate kutokana na mchele, vitumbua tunaweza tukatengeneza bagia kutokana na dengu tunalima dengu, tunaweza tukatengeneza bagia kutokana na kunde. Kwa hiyo mazao tunayo mengi sana ambayo tunaweza tukatumia, tuachane na huu mtazamo kwamba bila mkate bila chapati za ngano, bila maandazi huwezi ukanywa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mazao kama korosho unaweza ukafanya mchanganyiko mzuri korosho, maboga pamoja na matunda ukapata *breakfast* yako nzuri sana, sitaki kuwarudisha labda kwamba tunafanya mambo ya kizamani lakini ndivyo vyakula ambavyo tunavyo na ni vyakula ambavyo vina lishe bora. Kwa mfano, maboga yanasaidia pia kwenye suala la kudhibiti *diabetes,* ni mazuri sana ukitumia ukaepukana na mkate au maandali ni mazao mazuri sana. Tunazo karanga pia kwa hiyo hata ndizi ni nzuri sana unaweza ukatumia kwenye *breakfast* uka-*balance* pamoja na karanga pamoja na matunda ukatengeneza mlo wako mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sana tutoe kipaumbele kwenye umwagiliaji wa mazao haya ili yaweze kupatikana kwa mwaka mzima, tunaweza pia hata tukawasaidia wakulima wetu wakapata kipato badala ya kupeleka fedha nyingi kununua ngano tani 1,000,000 wakulima wetu wadogo wanaweza wakapata kipato na wakatusaidia pia kupata lishe bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hifadhi ya chakula naomba nizungumzie kidogo eneo hili muda ni mdogo, tuna matatizo ambayo yametokea wakati Fulani, watu wamepoteza maisha kutokana na sumukuvu na hii mara nyingine inatokana na hifadhi ambayo siyo nzuri ya nafaka au mazao ya karanga. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kuna wasambazaji wa ile mifuko ambayo hairuhusu hewa kupita au unyevunyevu, tuhitimize sana hii mifuko isambae kwa wakulima wa mahindi ili waweze kuhifadhi nafaka. Naomba dakika moja, mifuko iweze kusambazwa kwa sababu hii inazuia sana sumukuvu na tunaweza tukapata chakula ambacho kipo *safe* zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna wale wabanguaji wadogo wa korosho wawezeshwe kupata *vacuum sealer,* Tanzania nzima ukitafuta *vacuum sealer* hazipo mpaka uagize nje na ukiagiza nje hizi zinatozwa *VAT,* mimi naomba *VAT* iondolewe kwenye *vacuum sealer* ili wabanguaji wadogo wabangue korosho na ziweze kuhifadhiwa vizuri kwa kutumia *vacuum sealer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesahau kuunga mkono hoja, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Wambura. Tunaendelea na Mheshimiwa Amandus Chinguile, Mheshimiwa John Sallu na Mheshimiwa Condester Sichalwe wajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, awali ya yote ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenijalia uhai na hatimae kusimama

mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kweli bajeti hii sasa inakwenda kujibu mahitaji ya wakulima wetu ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Bashe, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Waziri umekuwa ni kielelezo kwa vijana wachapa kazi sana pamoja na Naibu Waziri mnatuheshimisha sana. Mheshimiwa Waziri ninakushukuru na kukupongeza sana namna ambavyo umeshughulika na Ushirika, kati ya maeneo ambayo walikuwa hawamuelewi Mheshimiwa Rais anataka nini ni eneo hili la ushirika. Mheshimiwa Waziri nikupongeze tena kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye suala la mbegu ya alizeti. Katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Nachingwea tulitumia mapato ya ndani tukanunua tani moja na nusu mbegu hizi za alizeti na tukatoa kwa bei ya ruzuku kwa wakulima mapokeo yalikuwa ni mazuri sana, sasa kwenye mpango wa Wizara juu ya kutoa ruzuku hii kwenye mbegu za alizeti Mkoa wa Lindi haumo, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri aiangalie Lindi hususani kwenye Wilaya hii ya Nachingwea ambayo tayari tumeshaanza kuonesha nia na wakulima wetu wamepokea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ninaishukuru sana Wizara kwa kutoa bei elekezi kwenye pembejeo, huu ni mwanzo mzuri Mheshimiwa Waziri, kazi hii iendelee, hii itatufanya wakulima wetu waweze kupata bei nafuu na hivyo kuondoa ile changamoto ya bei kupanda mara kwa mara. Mheshimiwa Waziri eneo jingine ni kwenye upatikanaji wa

pembejeo Jimbo langu la Nachingwea uhitaji kwa msimu huu ni tani 1,000, mpaka sasa tumepokea *Sulphur* peke yake tani 99, tunaona bado upatikanaji umekuwa ni wa chini mkituwezesha kupata kwa muda muafaka itatusaidia kuzalisha kwa wingi zaidi pia kuendana na muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wakulima wa Wilaya ya Nachingwea kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya. Hata hivyo, ipo changamoto na kadhia ya Tembo, nafahamu kwamba ninachangia kwenye Wizara ya Kilimo lakini mazao yanayoshambuliwa ni ya kilimo, Wanyama hawa waharibifu ni kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii. Adha hii ni kubwa na kwakweli kwenye maeneo yetu huko changamoto hii ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16 juzi yupo mwananchi mmoja amekanyangwa na kuuawa na tembo, Serikali hii ni moja, Wizara ya Kilimo niiombe sana kwa sababu mazao haya yanayoharibiwa ni mazao yatokanayo na kilimo lakini waharibifu wapo kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, zungumzeni lugha moja ili muone namna ambavyo hawa wananchi wetu mtawasaidia, changamoto hii ni kubwa kweli kweli, yapo maeneo ambayo ukifika leo utawaonea huruma, anakwenda shambani anakwenda kufanya nini kwa sababu hawa wanyama wameshaharibu sana. Maeneo ya Namapwia, Nditi, Kata ya Ngunichile, Namikango, Lionja, Kipara, Kilimarondo, Matekwe, Kiegei hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Mheshimiwa Msambatavangu juzi alizungumzia hapa juu ya afya ya akili, hebu huyu mkulima ambaye amefanya kazi kubwa kwa kilimo tena cha kizamani kwa jembe la mkono halafu hawa Wanyama wanakwenda kufanya uhabiribu, matokeo yake kwa kweli huyu mtu anaweza akapata tatizo la afya ya akili. Katika hili ninaiomba sana Serikali izungumze lugha moja, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii na hapa nisema

tu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii najua bajeti yake inakuja kwenye hili aandae kwa kweli maelezo ya kina yatakayonifanya nisiondoke na Shilingi yake kurudi nayo kule Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali inatisha hali ni mbaya na sisi kama wawakilishi hatueleweki na mara kadhaa nimekwenda na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii alituahidi kutujengea kituo na kutuletea Askari, mpaka sasa hicho kituo hakuna na eneo hilo ni kubwa. Siyo hilo tu, kwenye Mkoa wa Lindi yapo maeneo mengine ambayo yamekubwa na kadhia hii, kwenye Jimbo la Mchinga kwa mfano, eneo la Milola, Kiwawa, huko nako waliahidiwa kujengewa kituo huko kwa ajili ya Wanyamapori eneo la Lutamba-londo bado hicho kituo kiliahidiwa tangu 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa uchungu zaidi kwa sababu maisha ya yule mpiga kura wangu hayawezi kurudi tena hata kama akipata fidia, hayawezi tena kurudi kwa sababu tayari ameshafariki, tuchukue hatua sasa kabla ya madhara mengine zaidi kutokea. Hii siyo la kwanza mwaka jana mwezi wa Novemba hawa tembo walishawahi kusababisha tena madhara ya namna hiyo ya kuuawa kwa mtu mwingine, tulikwenda na Naibu Waziri alikwenda kutoa pole hapo, tunachotamani hapa ni kupata dawa ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo wananchi wale sasa wanakata tamaa kwa sababu hakuna namna ya kwenda shambani tena. Hawa tembo sasa ukienda maeneo haya kwa mfano ya Namapuya ni kama ng'ombe sasa wapo tu wanazagaa, hata leo ukifika inatisha, hii hali hatueleweki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chinguile. Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na michango yetu tuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Antony Mavunde ambao ni Ndugu Riziki Tunga kutoka *TPSF* karibu sana mgeni wetu kutoka *TPSF*. Pia tunae Ndugu Janeth Muhizi ambaye pia anatoka *TPSF* karibu sana, Tunae Frank Mushi ambaye anatoka *Africom Africa* karibu sana. Karibuni sana wageni wetu kwenye Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mheshimiwa John Sallu na baadae Mheshimiwa Condester Sichalwe na Mheshimiwa Josephine Genzabuke wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ninatoa shukrani nyingi kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa na *political will* kwenye kilimo, hii inatusababisha wakulima sasa tuwe na imani kwamba kilimo kitakuwa ndiyo mkombozi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninashukuru sana Mheshimiwa Bashe Waziri wa Kilimo, Naibu wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa jinsi ambavyo wanachapa kazi. Kwa mfano, katika Bunge hili niliwahi kuongelea inzi weupe wanaosumbua matunda hususani machungwa kwenye Jimbo langu, kwa kweli timu hii ilifanya kazi kwa haraka sana na wakaleta viuatilifu katika awamu mbili, kwa kweli wakulima wangu wamenufaika sana na hivyo viuatilifu na Kata zote zinazolima machungwa sasa hivi wanakamata wale inzi na machungwa yanaendele kuwa bora, nashukuru sana timu yote ya Wizara ya Kilimo kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninashukuru Watafiti, kwetu zao la muhogo liliingia kama zao la kuokoa njaa lakini baada ya muda limekuwa ni zao la uchumi. Watafiti pale walituunga mkono wakaja kutukomboa kutoka kwenye kilo tatu mpaka tano kwa shina, mpaka kilo 10 hadi 15 kwa shina na sasa muhogo umeendelea kuwa na tija. Uzalishaji baada ya kuhamasika umekuwa mkubwa sana, sasa hivi hekta zipatazo 70,135 zina muhogo ambazo tuna makisio ya kuvuna takribani tani Milioni Kumi lakini tatizo kubwa linalotukabili sasa ni masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANTRADE* wamejitahidi kututafutia masoko ya nje lakini bado yanasuasua, kuna soko la ndani ambalo hatujaligusa kabisa, kwa utafiti nilioufanya tuna makampuni takribani 20 yanayoagiza *starch* kutoka nje lakini hawanunui kabisa *starch* yetu ya ndani. Namuomba Mheshimiwa Waziri Bashe akishirikiana na Wizara ya viwanda tuweze kuli-*tap* hili soko kwa sababu soko la ndani ni soko la uhakika zaidi ambalo linaweza kuleta tija kwa wananchi wetu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Viwanda tuhakikishe kwamba waagizaji hawa wa *starch* waweze kutumia *starch* yetu ya ndani. Kweli kuna ambao wanaweza kutumia hii *starch* moja kwa moja kama *raw* ilivyo, lakini wapo wanaotumia *modified starch,* kwa hiyo Wizara hizi zishirikiane kuona kwamba hiyo *modified starch* inayotakiwa ni ya mtindo gani ili viwanda vyetu viweze kuelimishwa na hata wale ambao wanataka kuwekeza sasa wanaweza kujua wawekeze kwenye viwanda vya namna gani ili kukidhi soko hilo la ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye muhogo niende kwenye alizeti, napenda kumshauri Waziri ana mikakati mizuri ya kukomboa nchi yetu kwa zao la alizeti lakini katika ile Mikoa aliyoweka ya kimkakati Mikoa ambayo ina mvua mbili kwa mwaka hawakuiweka. Kuna Mikoa ambayo ina mvua

mbili kwa mwaka ambapo na Jimbo langu lipo kwenye eneo hilo, ambalo unaweza kulima alizeti mara mbili kwa mwaka na ukavuna mara mbili kwa mwaka. Hii ingeweza kutatua tatizo la mafuta tulilonalo kwa haraka Zaidi. Ardhi tunayo ya kutosha, wananchi wapo tayari kabisa, tunaomba hizo ruzuku za alizeti nazo zije kwetu tuweze kukomboa shida iliyopo kwenye nchi yetu kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umwagiliaji nchi yetu ina mabonde mengi ya umwagiliaji na vilevile kwenye Jimbo langu kuna Mabonde ya mto Pangani na mabonde ya mto Msangazi, ninaomba Idara ya umwagiliaji ifuatilie mabonde haya na kuweza kuweka mbinu sahihi ya kutumia mabonde haya ili tuweze kuzalisha mbogamboga kwa wingi ambazo zinaweza kutuletea tija kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nashukuru sana naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Sallu kwa kutumia muda wako ipasavyo. Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nianze kuipongeza Serikali kupitia Wizara yake ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza pamoja na *crew* yako yote bila kusahau Katibu Mkuu na Watendaji wote. Kwa dhati kabisa naomba nimpongeze Mkurugenzi wa *TAHA* Dada yangu Jackline Mkindi, kwa kweli tunakupongeza sana kwa namna ambavyo umeendelea kuwapa matumaini Wizara ya Kilimo, umeonesha mfano kwa akina mama ambao wanafanya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Bunge hili niseme naomba urafiki wetu usiishie tu kule Arusha sasa hivi tuhamie Jimboni Momba tunatamani kukuona. Mheshimiwa Waziri

kabla nielekeze mchango wangu kwenye mambo mawili kwenye Benki ya Kilimo pamoja na umwagiliaji naomba nitoe ushauri. Mheshimiwa Waziri hotuba yako ni njema sana na imeleta matumaini sana kwa wakulima wa nchi hii, kwa namna hata ulivyokuwa unawasilisha mwili wako ulivyokuwa unazungumza inaonesha umebeba matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hili ili bajeti yako iweze kutekelezeka vizuri, angalau kupungue siasa kidogo, ili siasa ipungue ili matumaini haya uliyowaonesha Watanzania wakati unawasilisha naomba tuanzie hapa. Sasa hivi bei elekezi ya Mahindi ambayo mmetangaza kwa kilo ni Shilingi 570 vyovyote vile, Mheshimiwa Waziri tumepata janga la mvua hapakuwa na mvua kabisa na hayo yalikuwa ni mabadiliko ya hali ya hewa, pia tulipata mfumuko wa bei kwenye mbolea, wananchi hawajalima na hata walipolima kwa kutumia uwezo wa Mwenyezi Mungu hawakuweza kwa sababu mazao yamekauka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kukuambia huko vijijini mahindi ni bei ghali. Bei ya debe moja la mahindi linauzwa shilingi 10,000, shilingi 9,000 hadi sehemu nyingine shilingi 12,000, mwananchi huyu atanunua kutoka wapi? Tunaomba kama inawezekana kwa kuwa *NFRA* lengo lake kubwa ni kwa ajili ya usalama wa chakula, tunaomba bei ya mahindi kwenye maghala yetu kwa mkulima wa kawaida yauzwe kwa kilo shilingi 300, tukiwa na maana kwamba yakiuzwa shilingi 300, kilo 100 yatauzwa shilingi 30,000 sawa sawa na ile bei ambayo huwa wachuuzi wanaanza kwenda kununua kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kula lazima uliwe! Kwa hiyo ambavyo Serikali huwa inaenda kuonekana wakati wa kununua tu sasa hivi tunaomba na yenyewe ikubali

kuingiliwa, wananchi hawana kabisa mahindi huko vijijini hakuna, hata wakipika hizo pombe za kienyeji hawana uwezo wa kununua mahindi. Kwa hiyo, tunaomba bei ya mahindi ishuke kwenye maghala iwe Shilingi 300. Utajuaje kwamba itaenda kumnufaisha mwananchi wa kawaida kwa sababu tunajua wafanyabiashara watachukua hiyo nafasi kwa ajili ya kujinufaisha, wale wanajeshi wako uliokuwa umewaleta pale juzi wanawajua vizuri wananchi wa kawaida wale Maafisa Ugani, wanawajua vizuri kabisa kwamba huyu ni Bibi hana uwezo na huyu ni mfanyabiashara, yule Bibi ambaye anataka kununua kuanzia gunia moja, debe mbili hadi gunia 10 tunaomba mahindi yauzwe kwa kilo moja Shilingi 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda kutokuwa rafiki kwenye suala la umwagaliaji, nimeshawasilisha maandiko yangu kwa watendaji wako. Yapo mabonde kadhaa kwenye jimbo langu ambapo pia mwaka 2021 nilikwambia; tunalo Bonde la Msangano ambalo likiwezeshwa kwenye umwagiliaji litahudumia vijiji zaidi 10. Pia tunalo Bonde la Kamsamba ambalo likiwezeshwa litahudumia kata zaidi ya nne pamoja vijiji zaidi 15. Vile vile tunalo Bonde la Kapele pamoja na bwawa ambalo linabeba Bonde la Kasinde pamoja na Mto Tesa, litahudumia kata zaidi ya sita pamoja na vijiji zaidi ya 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea lango la *SADC* tunamaanisha Wilaya ya Momba. Wilaya hii ina majimbo mawili; Tunduma na Momba. Sisi Momba ndiyo tunalima, Tunduma hawalimi. Sasa Mheshimiwa Waziri itakuwaje usituwezeshe sisi huku ambao ndio tunaanza kupokea kwenye lango la *SADC* kwenye umwagiliaji? *How comes* mtu unaweza usitengeneze sebule ukaenda kutengeneza chumbani, mgeni akija atajuaje? Kwa hiyo, tuanzie hapa ambayo ndiyo mapokeo ya lango la *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchele wote ambao unauona upo pale Tunduma unatoka Kamsamba na mchele wa Kamsamba unauzika sehemu yoyote. Kwa hiyo, tunaomba sana; *Zambians* wanakula mchele wetu, Kongo wanakula mchele wetu. Tunaomba kuwezesha kwenye mabonde yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo namwomba Mheshimiwa Waziri hili tusaidiane. Ataongea vizuri na watu wa TAMISEMI, tunaelewa dhati kabisa ya moyo wake ya kwamba anataka kuwasimamia wale Maafisa Ugani, lakini *how comes* mzazi awe na mtoto ambaye amemzaa, na ana uwezo, anaweza kumhudumia, lakini awe anakulia nyumba ya pili? Maafisa Ugani warudi kwenye Wizara yake. Hiyo *D by D* tunaona kabisa imeshindwa kufanya kazi. Haiwezekani hata kidogo…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia hiyo sentensi yako ya mwisho.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Kule kwenye Halmashauri zetu Maafisa Ugani wanatumwa kazi nyingine na wakati mwingine hata wakipewa magari wananyang'anywa. Sasa nani ambaye ataweza kusoma kama hali. Kwa hiyo, tunaomba Maafisa Ugani warudi kwenye Wizara yako ili tuone huo usimamazi unaotaka kuwasimamia sisi tuje kukubana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Sichalwe. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Yahaya Massare, ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye wingi wa Rehema kwa kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako tukufu. Namshukuru sana Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu kwa jinsi inavyowatumikia Watanzania. Nampongeza Mheshimiwa Bashe kwa kazi nzuri anayoifanya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunafahamu kwamba Sekta ya Kilimo imeajiri watu wengi sana. Asilimia 65 ya Watanzania wote wameajiriwa na kilimo, wakiwemo wanawake na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo imejipanga kwa ajili ya kukiinua kilimo. Kilimo kikipewa kipaumbele wananchi wataweza kufanya vizuri katika kilimo. Ni ukweli usiopingika kwamba wananchi wakiwekewa mazingira wezeshi katika kilimo wataweza kufanya vizuri. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri, Serikali iweze kutoa ruzuku kwa ajili ya mbolea. Kwa muda mrefu sana mbolea imekuwa ikileta shida kwa wakulima. Maeneo mengine mbolea inachelewa kufika na tunafahamu kabisa kwamba mvua za kwanza ni zakupandia na maeneo yanatofautiana. Kigoma na Rukwa ni tofauti, na hata Tanga. Kwa hiyo, mvua zinazoanza kunyesha Kigoma pengine Tanga zinakuwa hazijanyesha. Kwa hiyo, tunaomba mbolea ifikishwe kwenye maeneo husika mapema kabla wakulima hawajaanza kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru Serikali kwamba kwa muda mrefu tumeona imekuwa ikitumia pesa nyingi kuagiza mafuta kutoka nje, lakini kwa sasa Serikali imedhamiria kabisa kuhakikisha mazao yanayotoa mafuta

yanapewa kipaumbele. Naishukuru Serikali kwa kuendelea kutusaidia sisi watu wa Kigoma, na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyoendelea kuhamasisha michikichi katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Kigoma walihamasishwa na wakahamasika kulima kilimo cha mchikichiki. Walio wengi tayari wamelima michikichi na inaanza kutoa matunda. Hata hivyo, bado mahitaji ya miche ya michikichi ni makubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kutusaidia miche ya michikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia miche 3,000. Mheshimiwa Waziri naomba uendelee kuniongeza miche mingine kwa sababu mimi ni mama ninayezunguka Mkoa mzima wa Kigoma na mahitaji ya miche ya michikichi ni ya Mkoa mzima. Kwa hiyo, naomba niongezewe miche mingine ya michikichi ili wananchi waweze kulima kilimo hiki na hasa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zao la alizeti nalo wananchi wameweza kuitikia kulima zao hilo. Naomba katika mikoa ile ambayo itapewa mbegu ya alizeti naomba na Kigoma nayo iweze kupewa kwa sababu alizeti inastawi katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa sasa mazao katika Mkoa wetu wa Kigoma mahindi na maharage kwa wakati huu wanapovuna bei ipo juu kidogo. Niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri mipaka iwe wazi ili wananchi waweze kuuza mazao yao nje ya nchi, kwa sababu wakiuza mazao yao nje ya nchi wanapata bei ambayo ni nzuri. Kwa hiyo, wanaweza kunufaika wao wenyewe, lakini wanarudisha gharama wanazozitumia wakati ule wanapokuwa wanalima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzunguma maneno hayo, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Genzabuke kwa kutumia muda wako wa dakika tano ipasavyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare na baadaye Mheshimiwa Tabasam Hamis, ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii nami nichangie Wizara hii ya Kilimo. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali na pia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kuikomboa nchi kutokana na utegemezi na kwa bajeti hii ya Wizara ya Kilimo ambayo kwa kweli kwa mara ya kwanza mimi nikiwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, nimeona Serikali imetenda haki kwa wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa dhamira yake ambapo alisaidia sana wananchi wa Mkoa wa Singida, Simiyu na Dodoma kwa mbegu za alizeti ambazo zilikuwa zina daraja kidogo nafuu ambazo kwa sasa zinaenda kuongeza tija na uzalishaji wa mafuta katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishauri Serikali yangu hii kupitia Mawaziri hawa vijana, waongeze mbegu zilizo bora. Walitupa mbegu za kawaida ambazo zitaongeza tija ya mafuta. Tuna upungufu mkubwa wa mafuta katika nchi hii. Tunatumia mafuta ambayo yana *cholesterol* nyingi, inatakiwa tutumie mafuta haya mazuri ya mbegu za alizeti ambayo yatasaidia wananchi wetu kuepuka maradhi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu walizotupatia ni nzuri kwa kiasi, lakini mbegu zinazofaa sana kwa kilimo ni mbegu za *hybrid* ambazo ndiyo zina tija na uzalishaji mzuri sana wa

zao hili la alizeti. Sisi Mkoa wa Singida ni Mkoa wa kielelezo, lakini Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Simiyu ambao mmewapa ruzuku na kuifanya kuwa mikoa ya kielelezo, mmeona jinsi ambavyo tumezalisha vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ambayo imeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa asilimia 155. Natamani kuona Serikali inaweka ruzuku katika mbolea lakini iongeze ruzuku katika pembejeo yakiwemo matrekta. Matrekta ndiyo yatakayokomboa kilimo cha nchi hii. Mkulima mmoja akinunua trekta katika Kijiji, anawalimia wanavijiji zaidi ya 20 mpaka 30 mpaka 50 kwa kipindi kimoja. Kwa bei za trekta za sasa wananchi wetu wanashindwa kununua matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iweke ruzuku ya kutosha, pale ndiyo unamsaidia mkulima. Kumsaidia mkulima kwa kilimo cha mkono bado hatujamkomboa na ndiyo maana mnatamani kuleta wakulima wakubwa kwa sababu wakulima wetu wanatumia kilimo duni. Sasa kama tuna dhamira ya kuwasaidia wananchi wa Tanzania katika kilimo na hasa vijana ambao wamekosa ajira, hebu tuwasaidie katika kuwawekea ruzuku ya kutosha katika pembejeo hasa matrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji pia ni suluhisho kubwa sana. Tukiendelea kutegemea kilimo cha mvua, bado uduni wa wananchi wetu na uchumi wa wananchi wetu utaendelea kudumaa. Tukiweka kilimo cha umwagiliaji hasa mikoa ile ambayo ni mikame; mje na mkakati wa kujenga mabwawa katika mikoa kame hii ya Singida, Simiyu, Dodoma na baadhi ya Mikoa ya Tanga kama Handeni huko ambako ni kukavukavu na Kilindi. Tukijenga mabwawa wananchi watalima mazao ya chakula na mazao ya biashara, tutatoka katika sura hii ambayo tunayo sasa ya kutegemea kilimo cha mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lipo mbele yetu, Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kusema hapa amezungumza kwamba njaa ipo. Nchi itakumbwa na njaa. Naomba sana Wizara hii kupitia *NFRA* waanze mapema sana kutoa chakula cha bei nafuu. Hatuhitaji msaada, wananchi wetu wamelima alizeti, wamelima mazao mengine, wakiuza basi kipatikane chakula ambacho ni cha bei nafuu ili tuweze kutoka. Katika kipindi cha kilimo kijacho wananchi wasianze kuhangaika, waweze kulima vya kutosha na waweze kuingia katika kilimo wakiwa na chakula ambacho kinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameitikia wito lakini hali ya mvua haikuwa nzuri sana, mvua ilikatika mapema na mazao mengine hayakuwezwa kupandwa, sasa hivi watu wanahangaika na dengu ambazo pia nazo pengine zikawa na mashaka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii uliyonipa nami niunge mkono hoja hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Yahaya kwa kutumia muda vizuri. Tunamalizia na Mheshimiwa Tabasam Hamis.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesikiliza hotuba ya Waziri Mheshimiwa Bashe. Mheshimiwa Bashe ni ni Waziri wa 27 wa kilimo katika nchi hii toka tumepata Uhuru. Katika hao Mawaziri 27 ni kwamba tulikuwa tuna Mawaziri wanane baada ya kupata Uhuru. Mawaziri hawa wanane walisimama katika uzalishaji wa mazao makuu sita katika tuliyokuwanayo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hawa Mawaziri wanane tuliokuwanao katika utawala wa Hayati Baba yetu wa Taifa

Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere, ni Waziri mmoja tu aliyekaa katika miaka mitano; 1975 mpaka 1980, Mheshimiwa John Malecela ambaye yuko hai, katika miaka yake mitano alisimamia mazao sita ya kimkakati. Zao la kwanza likiwa pamba; zao la pili likiwa kahawa; zao la tatu, mkonge; zao la nne, korosho; zao la tano, chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mazao yalileta pesa nyingi sana za kigeni, lakini mazao haya yalionesha biashara. Mapinduzi ya biashara yalianza kuonekana katika misimu yetu katika nchi hii, ikawa ni misimu yenye kashikashi ya biashara. Unajua kwamba mwezi wa sita bei itatangazwa ya pamba, mwezi fulani itatangazwa bei ya Kahawa na mwezi fulani itatangazwa bei ya kitu fulani, mwezi wa kumi itatangazwa bei ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili lilileta mapato makubwa katika nchi hii; na idadi yetu ya wananchi katika nchi hii walikuwa ni wachache, leo nchi inakwenda kuwa na wananchi zaidi ya milioni 60, lakini tumeondoka katika haya mazao yetu ya kimkakati, haya mazao yameachwa. Nawe Mheshimiwa Bashe sasa hivi tunavyozungumza, ni kwamba umekuja kuongeza mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mpo katika Wizara yenu ninyi, hii ya kilimo katika mwaka 2011 mpaka leo, wamekaa Mawaziri zaidi ya wanane na wewe hapa sasa hivi unakuwa ni Waziri wa tisa. Mmeongeza zao la mchikichi, mmeongeza zao la alizeti, mmeongeza zao la mpunga, mmeongeza mahindi na parachichi kama matunda, lakini hayo mazao yote ya kimkakati, ninachoona mimi, ushauri wangu Mheshimiwa Bashe ni kwamba lazima ifikie mahali mkamshauri Mheshimiwa Rais kwamba tunahitaji sasa wawepo Manaibu Wawili katika Wizara yako. La sivyo, utachoka. Huwezi kusimamia mazao ya kimkakati 12, wakati huo huo mwende katika mazao mengine mchanganyiko, na

wakati huo huo tunataka mbolea, wakati huo huo tunataka viuatilifu, itakuwa ni ngumu sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba bajeti hii ya kilimo ni ya kwanza toka tumepata Uhuru ya kiwango cha juu kiasi hiki. Inaonesha dhamira ya Mheshimiwa Rais moja kwa moja kwenda kwa wakulima kuwasaidia waweze kutoka. Sasa kama tunataka tutoke kwa kilimo hiki tulichonacho, nimekuona Mheshimiwa Bashe umejitahidi sana. Wewe ni miongoni mwa Manaibu Waziri waliokaa na Mawaziri tofauti karibu miaka sita. Ni Naibu Waziri pekee katika nchi hii aliyekaa kwa miaka mingi, alikuwa ni Sumaye. Sumaye amekaa kwa miaka 10 kama Naibu Waziri, na baadaye akafanya vizuri akaja kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na historia ya Wizara Kilimo ilivyo, Manaibu mnaokuja kupata nafasi hii kuwa Mawaziri wa Kilimo mmepita katika changamoto nyingi katika nchi hii. Sasa nafasi yako kama kijana, uende kwa hawa wazee, bado wako hai; nenda kwa Malecela ukamsikilize aliwezaje ku-*perform*? Nenda kwa Sumaye ukamwulize, aliwezaje ku-*perform?* Kwa sababu naye alikuwa kijana kama ninyi. Leo mkiacha kuwasikiliza hawa wazee, ni kwamba bado mtapewa fedha nyingi na hamtaweza kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba hizi pesa zilizotajwa kwa wingi wake, ni kwamba kwenye *irrigation* tayari kuna ongezeko kubwa la pesa tumepewa, kwenye utafiti kuna pesa nyingi tumepewa. Sasa hizi pesa zigawanyike vizuri katika suala la utafiti. Ushauri wangu ni kwamba, hivi vituo vyetu vya utafiti, kuna *TARI* halafu kuna Mwanza pale Ukiriguru, tunaomba waingie katika utafiti katika mazao haya ya kimkakati. Tuangalie mbegu gani ambazo zitakazoweza kutumika na mbegu ambazo tutaweza kutoa mazao mengi ndiyo zifanyiwe kazi. Pia gharama za

utafiti pia mziangalie sana, zinaweza zikawa kubwa na zisije kuwa na tija. Hili uliangalie sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine cha msingi katika jambo hili ni kwamba tunakuja kuzungumzia suala la umwangiliaji. Tumepata skimu nyingi sana za umwangiliaji katika nchi hii, zinakuja kuongezeka na fedha mmepewa nyingi za kutosha. La kwanza ambalo linanitia shaka, kwenye kituo hicho cha umwangiliaji hapo *Iringa Road,* hao watu wanaokaa pale kwa ajili ya utafiti wa umwangiliaji na kushughulika masuala ya umwangiliaji wanakaa kwenye mabanda ya stoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hawa watu mnaenda kuwapa zaidi ya Shilingi bilioni 200 na kitu, kama 300, angalia na ofisi zao hao watu wanazokaa. Wanakaa *garage*. Mimi nimeenda juzi kuangalia, wapo *garage* Mheshimiwa Waziri. Unayeenda kumpa pesa kiasi hicho, bado hata ofisi hana, itawezekana wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika suala hili ni kwamba usiangalie mabwawa ya *irrigation* peke yake, lazima mchimbe visima tuingie katika umwangiliaji wa visima. Wenzetu Kenya sasa hivi wanamwagilia mashamba yao kwa kutumia visima. Hapa tumefaulu.

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine, naona kengele imelia…

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa. Muda wetu wa kuchangia asubuhi hii umeisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Dah, sasa…

**MWENYEKITI:** Malizia kuunga mkono hoja.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo, naogopa kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Muda wetu umeisha kwa sababu *time* ya asubuhi ndiyo hiyo imeishia hapo.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam Hamis. Huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naelewa ugumu wa wanasiasa kuzungumza kwa muda mfupi, lakini niwapongeze sana wale wote ambao wameweza kutumia muda wa dakika tano kwa kuweza kuongelea hoja zao. Niendelee kuwasisitiza wenzangu wengine, tuendelee kujifunza kutumia muda mchache katika kuwasilisha hoja muhimu ambazo tunaona ni za msingi kufika kwa mdomo. Basi na zile nyingi ambazo hatukuweza kuziwasilisha tuziwasilishe kwa maandishi kwa sababu pia nazo zinabaki kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, kwa vile wachangiaji wetu wamebaki hapa, wacha niwataje ili waweze kuchangia jioni. Tuna Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Esther Malleko, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mheshimiwa Michael Mwita Kimbaki, Mheshimiwa Robert Chacha, Mheshimiwa Regina Ndege na Mheshimiwa Noah Lemburis Mollel na wengine watatajwa baadaye.

Kabla hatujasitisha shughuli zetu, tuna wageni wamekuja mchana huu ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wa kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambaye ni kaka yake kutoka Majohe Jijini Dar es Salaam ambaye Ndugu Harun Maarifa. Yule pale yupo, karibu sana ndugu yetu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 100 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma ambao baadhi yao ni wapigakura wake kutoka Moshi Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Gerald Swai. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo cha Mipango hapa Dodoma. Natumaini mmefaidika kwa yale ambayo yanaendelea hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu umefika mwisho, sasa niwatakie mchana mwema. Pia niahirishe Shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, namwita sasa Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole. Wajiandae Mheshimiwa Twaha Mpembenwe na Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu ya wananchi na wakulima wetu. Kwanza nianze kabisa kwa kumpongeza na kumshukuru sana Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuongeza bajeti hii ya kilimo kutoka Shilingi bilioni 294 mpaka Shilingi bilioni 751. Kwa kweli huu ni ushindi mkubwa sana kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja ambacho nataka Wabunge wenzangu tukione na kama tunaweza kusaidia kubadilisha. Mwaka jana bajeti ilikuwa Shilingi bilioni 294 na katika hizo fedha za maendeleo zilizochangiwa kwenye hiyo bajeti zilikuwa Shilingi bilioni 164, lakini ni asilimia 46 tu ya bajeti nzima ya maendeleo iliyotoka Serikalini kwenda kwenye Wizara ya Kilimo. Sasa mwaka huu bajeti imepanda zaidi imekuwa Shilingi 751 bilioni, na katika hizo bajeti zaidi ya Shilingi bilioni 630 zinakwenda kwenye maendeleo kwa mafungu yote mawili 43 na 05. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali la kuuliza. Je, hizo fedha zitatoka? Kwa sababu kupanga bajeti na hela kutoka ni vitu viwili tofauti. Kama tutakaa hapa tutaongea hata kwa wiki nzima nakushauri hiki, nakushauri kifanyike hiki au kipi tunataka lakini kama Serikali haitatoa fedha za bajeti ya maendeleo kwenye hii Wizara ya Kilimo itakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimuombe Waziri wa Fedha aiangalie bajeti hii ya Wizara ya Kilimo kwa jicho la tatu. Au ikiwezekana sisi Wabunge tufunge angalau kwa wiki moja tumuombe Mwenyezi Mungu awaguse Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhakikisha bajeti ya Wizara hii ya Fedha fedha zote zilizoombwa zinakwenda kama zilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tangu uhuru haijawahi kutokea bajeti ya Wizara ya Kilimo ikazidi Shilingi bilioni 300; lakini mwaka huu bajeti imekuwa mpaka Shilingi bilioni 751. Na kama Mungu akitujalia hii bajeti yote ikapita kama ilivyo na fedha zote zikaenda, mimi naamini nchi yetu ya Tanzania itakuwa imepiga mageuzi makubwa sana kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana bajeti zote za ushirika zitafanya kazi, miradi yote ya maendeleo itapata fedha, kila kitu kilichoombewa kitakuwa na fedha, na kaka yangu Bashe nafikiri utaongezeka *at least* kilo 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nafikiri imefika sasa tuwe na sheria ya kilimo. Huko vijijini watu wanauza mbegu feki. *AMCOS* nyingi hazilipi wakulima zinachukua mazao zinalima. Hawa watu hata wakikamatwa wakipelekwa mahakamani inageuka kuwa ni kesi za madai. Sasa mtu umemuuzia mtu mbegu feki, mtu umekopa fedha zake hujalipa mazao yake itakuwaje kesi ya madai? Mimi naomba hii iingizwe iwe kesi ya uhujumu uchumi. Na mimi naomba Mheshimiwa Waziri kama hutaleta muswada kwenye bajeti ya mwezi wa tisa hawa watu *tu-criminalize* basi mimi nitaleta muswada binafsi na ninaomba Wabunge wenzangu mniunge mkono hii iingizwe iwe sheria ya uhujumu uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani watu wawauzie wakulima mbegu feki, vyama vya ushirika visilipe mapato yao kwa wakulima alafu iwe ni kesi ya madai. Hichi kitu hakiwezekani tunawatia umasikini. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa hii sheria ya kilimo ije.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho; mimi natoka Mkoa wa Songwe. Sisi tunalima sana mahindi lakini mbegu zetu bora tunazotumia zinatoka Zambia. Sasa mimi naomba, na ambacho ninachoomba Wizara kama basi tunashindwa

kuwaruhusu watu wetu waende Zambia kuchukua mbegu basi tufanye mpango hizo mbegu bora za Zambia zije zizalishwe hapa Tanzania. Kwani kuna ubaya gani hizo mbegu za Zambia zikija zikazalishwa hapa? Kwa sababu mbegu zilizopo Tanzania hazikubali kwenye mikoa yetu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mpembenwe; Mheshimiwa Kandege, jiandae Mheshimiwa Esther Malleko**.**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kunijalia afya njema niweze kusimama hapa. Baada ya kilio kusikika cha zao la soya naamini Wizara imeelewa vizuri, itafanya marekebisho kidogo ili kilimo cha soya kiweze kuenea Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba nijielekeze katika maeneo machache kama mawili matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote; na niwakumbushe kwamba hakuna Taasisi hata moja iliyoanzishwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo haikuanzishwa kwa makusudi. Nianze na *Food Security.* Kama Taifa lazima tuwe na uhakika wa chakula ndiyo maana ilianzishwa *Food Security* ikaja ikaitwa *Strategic Grain Reserve ikaja* ikaitwa *National Food Reserve Agency. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau kwamba ukitaka kupata mazao yaliyo bora lazima ujihakikishie kwamba unakuwa na mbegu iliyo bora, lazima uhakikishe kwamba pembejeo kwa maana ya mbolea inapatikana iliyo bora; na ndiyo maana zikawepo *TFC*, na *NRFA*. Pia kukawa na Taasisi ambayo inachunguza na kuhakikisha kwamba tunakuwa na pembejeo zilizo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa katikati kuna kosa kubwa ambalo kama Taifa tulitaka kufanya. Nashukuru Mheshimiwa Waziri umekumbuka kuhakikisha kwamba tunaifufua *TFC* kwa kuiwezesha kimtaji na kuhakikisha kwamba hii habari ambayo umekuwa unahangaika na makampuni ya watu binafsi kwa kuwa *cartel* na kuwa na bei ambazo mwananchi wa kawaida hawezi kumudu. Hakika kwa kuwawezesha kampuni hii nina uhakika kama taifa tutakuwa na uhakika wa pembejeo kumfikia mwananchi wa kawaida, na hasa mbolea, na kule Kalambo zitafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu fedha ambayo tunayo kwa ajili ya ruzuku haitoshi. Ikupendeze kwamba kwa taasisi ya Serikali ambayo una uwezo wa ku-*monitor* na kufuatilia kuhakikisha inamfikia mwananchi ambaye umemkusudia tuanzie na taasisi hii, tukipata nguvu ndipo tuje kwenye hizo kampuni nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kampuni nyingine zinataka kupeleka kule ambako wanapata faida. Nimeshuhudia hivi karibuni ukawa unakimbizana nao, wanaweka bei ambayo mwananchi wa kawaida hawezi kumudu hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikumbushe, kuna taasisi moja inaitwa *Early Warning and Crop Monitoring,* kilikuwa ni kitengo katika Wizara yako ambacho kilikuwa kinakupa taarifa mwenendo wa hali ya chakula nchini na

kama Serikali inaweza ku-*make decision timely*. Ni vizuri kitengo hiki ukakifufua ili kifanye kazi iliyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo na baada ya kuwa na uhakika kwamba zao la soya limeeleweka kilichobaki tu ni maeneo ambayo umesahau kutaja. Maeneo ya Mikoa wa Songwe, Rukwa lakini Manyara pia soya inakubali. Naamini sasa tunaenda kufanya mapinduzi makubwa tuhakikishe kwamba tunakuwa na mafuta ya kutosha nchini na mafuta ambayo yako bora. Mungu akubariki, mapinduzi haya ambayo yameanzishwa na Mheshimiwa Rais wa Tanzania asilimia zaidi ya 75 watanufaika na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Namuita Mheshimiwa Esther Malleko, wajiandae Mheshimiwa Bupe na Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika sekta hii nyeti kabisa ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana sana Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo Tanzania. Tumeona *Royal Tour* ikitikisa Tanzania nzima, tumeona mishahara ya wafanyakazi inazungumziwa kila mahali hapa Tanzania. Lakini kubwa zaidi ni katika bajeti ya kilimo ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu ni maajabu makubwa sana na haijawahi kupatakutokea kwa kuwa bajeti ya kilimo imeongezwa kutoka Shilingi bilioni 294 hadi kufikia Shilingi bilioni 751, sawa na asilimia 155. Kwa kweli Mama yetu

anafanya kazi kubwa, wote tunapaswa kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nichukue pia nafasi hii kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo pamoja na Mheshimiwa Mavunde kwa kazi kubwa sana wanayoifanya katika sekta hii ya kilimo. Wamekuwa ni wachapakazi lakini si hivyo tu, wamekuwa na ubunifu mkubwa katika kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nijikite kuchangia katika zao la kahawa. Zao la kahawa limekuwa ni uti wa mgongo kwa Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro unalima zao la kahawa tangu kabla ya uhuru. Lakini si Kilimanjaro tu, takribani mikoa 15 katika Tanzania inalima kahawa. Ni sawasawa na kwamba nusu ya Watanzania wanalima kahawa. Hivyo ukigusa kahawa umegusa nusu ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha sana kahawa hii ambayo ilikuwa inaiingizia Tanzania pato kubwa kabisa kuliko mazao mengine yoyote limeachwa nyuma na kwa sasa hata ruzuku halipati. Mazao ya korosho, tumbaku na pamba yanapata ruzuku, lakini tunajiuliza ni kwa nini kahawa haipati ruzuku?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu sana, lakini leo bila kupepesa macho, nimepanga kuondoka na Shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri kama hatatoa majibu ya kujitosheleza ya kwa nini kahawa haipati ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuwa ni changamoto kwenye kahawa ni suala la miche. Wananchi hasa wa Kilimanjaro wanahitaji miche bora ya kahawa; ile miche ambayo inaweza kustahimili hali ya hewa

ya sasa lakini pia inayoweza kustahimili magonjwa huku ikiendelea kutoa mazao mengi tofauti na ile ya zamani. Mibuni mingi iliyopo katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro imezeeka. Leo tunahitaji miche mingine ili tuweze kupata kahawa iliyobora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana Wizara kwa kuwa bajeti ya sasa kwenye uzalishaji wa mbegu imetoka kuanzia Shilingi bilioni 10.58 hadi Shilingi bilioni 43.03, haya ni mapinduzi makubwa sana. kwa hivyo, ninaamini wananchi wa Kilimanjaro Watanzania wote wanaolima kahawa watapata miche bora itakayosaidia zao hili kufika pale lilipokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la taifa lilikuwa ni kufikia kuvuna tani 300,000 ifikapo mwaka 2025. Lakini mpaka sasa mwaka 2021/2022 tumeweza kuzalisha tani 65,235 ilhali tulikuwa tunalengo la kuzalisha tani 72,000. Hatuwezi kwenda kwa staili hii tukaweza kufika huko tulikokuwa tunataka kwa 300,000. Kwa sababu leo tuko tani 65,235 mpaka tufike tani 300,000 itachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, ninaomba zao hili lipewe kipaumbele, zao hili lipewe ruzuku. Leo tuna maafisa ugani ambao tumeona mmewapa mapikipiki wakafanye kazi kubwa kwenye zao hili pia… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata. Jiandae Mheshimiwa Kembaki.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kaka yangu Bashe na Naibu wake; lakini pia niwapongeze Makatibu Wakuu wote watatu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kipekee nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mama Samia Suluhu kwa kazi nzuri na kwa kuijali Wizara ya Kilimo kwa kuongeza takribani shilingi bilioni 751. Hiki si kitu kidogo, hongera sana Mama yetu, kazi unaipiga na unaupiga mwingi Mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kwenye hoja zangu. Kwa sababu ya muda niongelee suala la pembejeo. Mkoa wa Rukwa maisha yetu sisi ni kilimo lakini pia mbolea ndiyo kila kitu. Hata hivyo, changamoto iliyopo mbolea imepanda bei kubwa sana. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kuhusu mbolea. Mbolea ndiyo habari ya mjini, mbolea ndiyo imeshika maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bashe akiweza kutatua changamoto ya mbolea kwa bajeti iliyopangwa hii kwa kweli maisha ya Watanzania na kilio cha Watanzania na machozi ya Watanzania yatafutika.

Mheshiimwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Rukwa unalima mazao mengi sana ikiwemo mahindi, maharage, ufuta, miwa na mazao mengine mbalimbali yanalimwa Mkoa wa Rukwa. Hata hivyo changamoto kubwa ni hilo suala la bei ya mbolea. Tunaomba Serikali iweke ruzuku. Hili si ombi, ni lazima Serikali iangalie suala zima la kuweka ruzuku kwenye pembejeo hasa kwenye mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kwenye suala zima la kilimo cha miwa Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa pamoja

na kulima mazao mengine yote tunalima pia miwa. Tunaomba Serikali ifanye utafiti iweze kujenga kiwanda cha kuchakata miwa, tutaweza kupata sukari ambayo imekuwa nayo ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia suala la matrekta. Wizara hii kupitia taasisi yake ya *NBC* iliweza kukopesha matrekta kwa Watanzania, lakini matrekta haya yamekuwa ni kichomi, adhabu, matrekta ni mabovu, matrekta uki-*test* mitambo tu ukiwa shambani trekta linabongonyoka, trekta linakuwa kama muhogo, ukilishika kidogo mara kichwa kule, mara kiwiliwili huko, matrekta hayaeleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ikayachukuwe matrekta kwa wananchi, matrekta yale imekuwa ni kichomi, matrekta yale yanawatesa wananchi wanawekwa ndani kila siku. Kama unaweza kuona hata Wabunge humu walikopa yale matrekta yani yale matrekta yamekuwa ni kichomi, ikiwezekana Serikali iweze ikayabeba ikayarudisha huko walikoyatoa, kuliko adhabu hii wanayopata wananchi, wanawekwa ndani wanalipa kila siku, lakini matrekta ni mabovu hayaeleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee tena suala lingine, niingie kwenye suala la benki. Benki ya Kilimo haijatunufaisha hasa sisi wa Mkoa wa Rukwa. Benki ya Kilimo tunaisikia tu iko Dar es Salaam na Dodoma, lakini kwenye mikoa hii ambayo inalima sana mazao hakuna hiyo benki. Sasa maana yake ni nini benki inaitwa Benki ya Wakulima, kwa wakulima hakuna benki hiyo, basi naomba Serikali iweze kupeleka benki kwenye mikoa ambayo inalima sana mazao, kwa mfano, Rukwa ipelekwe kabisa iandikwe Benki ya Kilimo kama zilivyoandikwa benki zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki nyingine zinaandikwa Benki ya *NBC*, *NMB* zinaeleweka, lakini Benki ya Kilimo

hatujaona, kwa hiyo Serikali ijitathimini sana kupitia Benki hii ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee tena suala lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, wajiandae Mheshimiwa Robert Chacha na Mheshimiwa Regina Ndege.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika sekta hii ya kilimo ambayo ni uti wa mgongo katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoelewa nchi yetu asilimia kubwa ya wananchi wetu wanategemea kilimo ili kujipatia kipato cha kila siku, matatizo mengi yanaweza kutatuliwa kupitia sekta hii ya kilimo ikiwemo chakula, pesa za kigeni, malighafi katika viwanda vyetu na ajira kwa vijana wetu. Majibu ya matatizo haya yanayoikabili nchi yetu yanaweza kutatuliwa pale ambapo Serikali itawekeza na kuipa kipaumbele sekta hii ya kilimo ambapo itaweza kutatua changamoto ya ajira katika nchi yetu lakini pia kupata malighafi za kutosha katika viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi nzuri na kuwekeza pesa nyingi katika upande wa utafiti. Kama unavyojua ili kilimo chetu kiweze kufanya vizuri Serikali inapaswa iweke pesa nyingi katika utafiti, maana utafiti

utaweza kuleta majibu ni wapi tunaweza tukalima mazao mazuri na yakafanya vizuri. Pamoja na kuwekeza pesa nyingi katika utafiti, umwagiliaji bado tija ni ndogo sana, hauleti majibu ambayo yanatosheleza. Kwa mfano, tunavyo vituo vingi vya utafiti katika nchi yetu mfano tunavyo vituo vikuu ambavyo ni *TARI* Kihinga, Ilonga, Tumbi, Buyola, Makutupola, Seyani, Ukiriagulu, Naliendele Mlingano, lakini pia tunavyo vituo vidogo ambavyo ni *TARI* Mikocheni, Tengeru, Naruku, Dakawa, Ifakara, Hombolo na Kifyulilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vituo hivi vyote, Serikali imekuwa ikipeleka pale pesa nyingi, utafiti umekuwa ukifanyika na majibu yanapatikana. Mfano, tulitembelea Kibaha tulipata watafiti wamefanya kazi nzuri sana, kuna muhogo mkubwa ambao ni zaidi ya kilo tano uko pale na umekuwa kama maonyesho katika kituo kile. Pia wataalam wale wamegundua wadudu rafiki ambao wakitumika badala ya kutumia viuatilifu ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, lakini pia wamegundua hazina kubwa ya tafiti ambazo ni za udongo ambao unafaa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti hizi ambazo zinagunduliwa na wataalam wetu haziwafikii wakulima wetu. Ni masikitiko yangu kwamba, pale katika Jimbo langu la Tarime Mjini, tumeshaacha kulima zao la muhogo, kwa sababu wadudu wanashambulia muhogo na haufanyi vizuri. Vilevile kuna ugonjwa ambao unashambulia migomba na wataalam hawa wamegundua mbegu nzuri ambayo wakulima wakilima haishambuliwi na magonjwa, lakini bado wakulima hawafikiwi na tafiti hizi ambazo zinafanywa na wataalam wetu. Pamoja na kwamba Serikali inatoa pesa nyingi katika tafiti lakini haifikishi kwa wakulima, hivyo haina tija kwa sababu walengwa wakubwa ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa niseme hakuna haja ya kutoa fedha kwa watafiti ambapo tafiti hizi zinawekwa kwenye madroo na zinawekwa kwenye

makabrasha badala ya kuchukuliwa na kupelekwa kwa wananchi. Nitoe ushauri wangu kwa Serikali wanapokuwa wanatenga fedha kwa ajili ya utafiti, watenge fedha kwa ajili ya kupeleka ujumbe au matokeo ya tafiti zinazopatikana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivi, kwa sababu kazi yote tunayojadili hapa, hoja zote zinazotolewa na Wabunge hapa, lengo lake ni wakulima ambao wengi wao wako vijijini hawako mjini. Mara nyingi wanapofanya maonyesho, wanafanya mjini wanaacha wakulima pale vijijini. Ningependa Waziri wa Kilimo kaka yangu, ahakikishe fedha zitengwe kwa ajili ya kuwafikia walengwa ambao ni wakulima, wapate taarifa sahihi. Kwa kufanya hivi wakulima…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri, mengine andika.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha, wajiandae Mheshimiwa Regina Ndege na Mheshimiwa Noah Mollel.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwa ajili ya Taifa letu. Juzi ameongeza asilimia 23 ya mishahara ya watumishi wa Serikali, ambao naamini ametimiza wajibu wake kwa nafasi yake, lakini na watumishi wa Serikali kwa sehemu yao na wao wana sehemu yao ya kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo maji ni uhai, chakula nacho ni uhai, lakini pia huduma za afya nazo ni uhai. Kilimo ni uti wa mgongo wa kwetu sisi Tanzania, lakini pamoja na kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, wakulima wetu uwezo wao wa kulima chakula chao, tofauti na mikoa mitano, mikoa mingine wananchi wetu wanalima chakula chao ambacho hakiwezi kuwatosheleza hata kwa mahitaji yao kwa mwaka, jambo ambalo ni hatari kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo matatu ni mambo muhimu kwa afya ya binadamu. Leo mimi Mbunge nasimama Bungeni kuzungumza bila ya kuwa na afya bora, bila ya kunywa maji, bila kula chakula, uwezo wa kuzungumza sitaupata. Kwa hiyo, najaribu kuishauri Wizara ya Kilimo kwamba suala la chakula ni suala muhimu. Jambo muhimu hapa Taifa letu litengeneze utaratibu au Wizara na wataalam wetu wa kilimo, nchi yetu iwe na uwezo wa kujiwekea akiba ya chakula kwa muda angalau miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za wenzetu wao wana mafuta yao kwa sababu uwezo wao ni mafuta yao wamejiwekea akiba ya kutosha, wanaweza wakaamua kuyafungia mafuta yao halafu sisi huku Tanzania tukawa tunalalamika, wakati hatuzalishi. Sasa na sisi kwa nchi yetu kwa sababu Mungu ametupa ardhi, na mvua tunapata kwa kiasi cha kutosha, ningeishauri Wizara ije na mpango wa kuhakikisha kwamba nchi inajiwekea akiba ya chakula kwa muda wa miaka mitano, angalau ikitokea siku moja au miaka miwili au mitatu mvua hainyeshi, wananchi wetu waweze kupata chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi tunayo, mvua tunapata ya kutosha, lakini bado wakulima wetu chakula wanachokilima hakitosheleza mahitaji yao ya mwaka. Napata tabu sana kwenye jambo hili. Kila jambo sisi kama

nchi au Wizara hatutakuwa na uwezo wa kujitosheleza, ardhi tunayo mvua tunapata, halafu wakulima wenyewe wanalima chakula kidogo ambacho hata wao wenyewe hakiwatoshelezi. Kwa hiyo Wizara itengeneze utaratibu au mkakati wa kuhakikisha kwamba wananchi wote wanahamasishwa kuhakikisha kwamba wanajilimia chakula ambacho kinawatosheleza kujilinda kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara hasa Wilaya ya Bunda zao kuu la kibiashara pale lilikuwa ni pamba, lakini leo pamba takribani miaka 10 haifanyi vizuri. Sio kwamba wakulima wale walikuwa hawana uwezo wa kulima isipokuwa tatizo ni soko, soko limeleta tabu, kwa hiyo limesababisha wale wakulima, badala ya kulima pamba sasa na kwa sababu wanalima pamba halafu uwezo wa kupanga bei hawana, anayewapangia bei mtu mwingine, wao wamekata tamaa ya kulima pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wananchi wetu wamerudi kuwa maskini. Naiomba Wizara ya Kilimo kwa sababu ina wataalam wa kilimo ambao wao wanaweza kutusaidia kututafutia zao mbadala hasa Mkoa wa Mara ambao sisi zao letu kuu la kibiashara lilikuwa ni pamba ili kwamba zao lile Wizara itakalotuletea lipate kuwasaidia wananchi wetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Regina Ndege, wajiandae…

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** …Mheshimiwa Noah Mollel na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze katika kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuona kwamba kilimo ndio kipaumbele katika nchi yetu, ukizingatia kwamba wananchi wetu wengi asilimia 60 wanajihusisha na shughuli nzima ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara nimpongeze kaka yangu Hussein Bashe Waziri wa Kilimo pamoja na Naibu Waziri kwa kufanya kazi kubwa kuhakikisha kilimo kinaenda kusonga mbele. Kwa kupitia Mawaziri hawa tulionao nina uhakika kutakuwa na mapinduzi makubwa katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa nchi yetu unategemea usalama wa chakula na usalama wa chakula unategemea kuwa na mbegu bora na mbegu bora upatikana kwa Serikali yetu kuamua tuzalishe mbegu hapa nchini. Asilimia 45 ya mbegu ya mahindi hutoka nchi za nje, lakini asilimia 95 mbegu ya mboga mboga inazalishwa nchi za nje. Hivyo basi inapelekea tunapokea mbegu ambazo si bora na wakulima wengi wanapopata zile mbegu na kwenda kufanya shughuli za kilimo uzalishaji unapungua siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iwekeze katika utafiti. Tukiwekeza katika utafiti tutawasaidia wakulima wadogowadogo. Sasa hivi wakulima wetu wanafanya kilimo kisichokuwa na tija. Wanalima bila ya kuelewa ardhi hii inastahili kuotesha nini, kwa sababu hawajui udongo ule unafaa kwa zao lipi. Kwa hiyo niombe sana Serikali iwekeze sana katika Vituo vyetu vya Utafiti ili wananchi wetu wapewe elimu kulingana na ardhi iliyopo. Wananchi wetu wapewe

elimu kuangalia ni mbegu gani inastahili kuoteshwa katika eneo hilo, tukifanya hivi tutawasaidia wakulima wengi na hatimaye suala zima la kilimo kitakuwa kinapanda siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la utafiti, Vituo vyetu vya Utafiti havifanyi kazi vizuri hii ni kwa sababu kuna kodi kubwa katika vifaa vile vya utafiti. Niiombe Serikali ipunguze au iondoe kabisa kodi katika vifaa vile vya utafiti. Utashangaa sana katika Serikali yetu hata vifaa vinavyoletwa na taasisi za kiserikali vinatozwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linapelekea vituo vyetu vya utafiti vinashindwa kufanya kazi. Sasa ni muda muafaka tuelekeze kwenye suala zima la utafiti, nina uhakika tutafanya mapinduzi makubwa katika suala zima la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kuwekeza katika kilimo cha mbogamboga na matunda *(horticulture)*. Sasa hivi kuna mwamko mkubwa sana kwa wananchi hasa vijana wengi na akinamama, wamepata mwamko mkubwa wa kujishughulisha na shughuli nzima ya kilimo cha *horticulture,* kwa sababu ni kilimo pekee ambaye unapata matokeo kwa muda mfupi, ni miezi mitatu hadi miezi sita unapata mavuno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwekeza kule, tatizo kubwa lililopo ni kwamba hawana mitaji na hawana vitendea kazi. Naiomba Serikali iwekeze kule ili angalau vijana wengi na akinamama wengi waweze kujiajiri na kukuza mapato yao ili kuendeleza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niendelee kuipongeza Serikali kwa kuweka msukumo mkubwa katika kilimo cha umwagiliaji. Hii hapa itasaidia sana wananchi kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kila jambo litafanywa na Serikali, niiombe Serikali iweze kuondoa kodi katika mitambo ya uchimbaji wa mabwawa ili wananchi wenyewe au wakulima waweze kununua hiyo mitambo na kuweza kujishughulisha na shughuli za umwagiliaji. Ukiondoa kodi katika mitambo ya uchimbaji itapunguza bei kwa asilimia 30 hadi 40. Kwa hiyo tuwasaidie wakulima wetu ili waweze kununua mitambo hiyo na kujishughulisha na shughuli nzima kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufikia hapa naomba niunge mkono hoja. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Noah Mollel, jiandae Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu nzima ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa suala la mbolea. Mbolea ya Tanzania imekuwa ni changamoto sana kwa wakulima wetu kwa sababu imekwenda juu sana. Jinsi ambavyo mbolea imepanda ukiangalia mwaka jana, mfano kwenye Mkoa wa Arusha, 2021 *Sulphate Amonia* ilikuwa ni Sh.45,000 kwa mfuko wenye kilo 50, lakini mwaka huu ni laki Sh.145,000. Hili ni ongezeko kubwa sana. Ukiangalia 2021 *Urea* ilikuwa Sh.65,000, mwaka huu 2022 ni laki Sh.150,000. Ukiangalia mbolea ya kupandia *DAP* ni Sh.75,000 mwaka jana, lakini mwaka huu ni laki Sh.165,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni janga kwa wakulima wa Tanzania kwa sababu hawana uwezo wa kufikia kiwango hicho cha mbolea kupanda. Ukiangalia wale wananchi wangu wa Kata za Ikiding'a ambao wanatumia mbolea

Sambasha, Olomontoni, Soko Ntu, Nimnyaki na Oldonyosambu hawana uwezo ya kununua mbolea kwa gharama kubwa hivyo. Tunaishauri Serikali kwamba lazima ifike mahali iweke ruzuku ya kutosha kwenye mbolea ili wakulima wale wadogowadogo na hata wale wa kati waweze kumudu mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbegu, nalo ni changamoto. Kumekuwepo na mbegu feki zinazoingizwa nchini na Mawakala, mbegu ambazo hazina tija, imekuwa kama ni kilio wale wakulima wanaponunua mbegu, wakidhani wananunua mbegu bora, wanaona ni bora wangerudi kwenye zile mbegu zao za zamani, kwa sababu umekuwa ni utapeli, watu wanachukuwa rangi, wanaweka kwenye mahindi, hivyo wakulima wanaona kama ni mbegu bora lakini kumbe ni mbegu feki. Hili nalo tunaishauri Wizara iangalie suala la mbegu hasa kwa kuwaangalia watu wanaouza mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madawa ya kunyunyuzia mimea, kwa maana ya mazao, nalo hili ni janga kwa sababu wakati mwingine madawa yananunuliwa, lakini hayana uwezo wa kuuuwa wadudu katika mazao. Kwa hiyo hili nalo naomba Wizara iliangalie na Mheshimiwa Bashe sina wasiwasi naye na Naibu wake kwamba kazi hii wanaiweza na wanaiweza kwa dhamira ya dhati, niwaombe sana kwamba kazi hii kubwa waliyekabidhiwa na Mheshimiwa Rais waweze kuifanya kwa uaminifu na uadilifu ili mwisho wa siku wapate karama yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba mwaka huu katika maeneo mengi hasa ukanda wa Kaskazini kuna upungufu wa chakula kwa sababu mvua ni kidogo. Kwa hiyo, naomba pia Wizara ilione hili na kulichukua kuwe na tahadhiri ya kwamba kutakuwepo na suala la upungufu wa chakula katika Ukanda wa Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila jambo wakati ule wa Serikali zingine zilizopita za kwetu kulikuwa na *slogan* mbalimbali, Siasa ni Kilimo, Kilimo ni Uti wa Mgongo. Haya yote ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunahamasisha jamii na Serikali kwa ujumla kujihusisha na kilimo ili kuleta tija ndani ya Taifa letu. ninaomba Serikali yetu kama mnavyojua sehemu kubwa ya Watanzania wanapata ajira kupitia kilimo, kama tunasema tunaongeza ajira Mheshimiwa Bashe na Naibu wako mnayo kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata ajira kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukitumia mashamba makubwa ya kilimo na mkayafuatilia kwa makini mashamba yote yanayojihusisha na kilimo na masuala ya umwagiliaji tutaongeza suala la ajira kwa vijana wetu na wengine wote kwa ajili ya kuinua uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo mpaka shamba liwe pori ndiyo muweze kufuatilia, fuatilieni mashamba ya kilimo hata kabla hayajawa mapori, mwisho wa siku wale wanatelekeza mashamba na wamekopa kwenye benki mbalimbali, wakishakopa wakidhani wanaendeleza hayo mashamba lakini mwisho wa siku wanatelekeza yanakuwa ni mapori, ndiyo Serikali tunakuja kushtuka sasa tunasema uzalishaji wa maeneo hayo umekufa. Kwa hiyo, nayasema haya nikiamini kwamba Waziri na Serikali kwa ujumla itaona kwamba inafuatilia mashamba yote ya kilimo ili kuleta tija kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mpembenwe jiandae Mheshimiwa Nyamoga, jiandae Mheshimiwa Muharami Shabani.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa hili. Sambamba na hilo nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuwapa dhamana wadogo zangu Mheshimiwa Bashe pamoja na Ndugu yangu ili kuweza kuiendeleza Wizara hii, kiukweli wamekusudia kuweza kutengeneza *legacy* ya aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi mzuri ni yule ambaye anao uwezo wa kuchukua maamuzi na kuyasimamia maamuzi hayo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Bashe, pale kwetu katika Mkoa wa Pwani tulikuwa na mfanyabiashara ya uchuuzi wa kukamua mafuta lakini kwa bahati mbaya hakufuata taratibu husika ikiwemo kupata leseni za kibiashara, vyombo vya usalama vilimkamata lakini nikushukuru sana Mheshimiwa Bashe ulichukua maamuzi magumu na uliweza kusimama katika maamuzi yale, ulisema kwamba asaidiwe mtu yule ili aweze kufanyiwa *registration* na *process* zingine zote hivi ninavyozungumza umefanya *multiply effect* ya hali ya juu, mtu yule sasa hivi anaichangia Serikali kwa kulipa kodi, safi sana endelea Ndugu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najivunia kuwa na Rais Samia kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Samia kuwa kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, pia najivunia vilevile Chama cha Mapinduzi kuwa ndiyo Chama kilichotengeneza dola. Kuna sifa nyingi sana lakini nitagusia sifa moja Serikali hii ni Serikali sikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama hapa mwaka jana, nilileta kilio cha watu wa Jimbo la Kibiti wakiwa wanalalamika

katika mambo makubwa mawili, jambo la kwanza ilikuwa ni suala zima la bei ya korosho na ufuta lakini jambo la pili ilikuwa ni suala zima la tarehe za kufanyika minada. Wale Ndugu zangu Wamakonde kule Mtwara na pale katikati Lindi walikuwa wanafanya minada tofauti nasi huku Baba zao watu wa Rufiki, hii ilikuwa inapelekea wakulima wetu kuuza mazao kwa bei ya chini, nilivyoleta kilio hicho nakushukuru sana Mheshimiwa Bashe na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana bei ya juu ya ufuta iliuzwa shilingi 2,556 katika Mkoa wa Pwani, kama hiyo haitoshi bei ya korosho iliuzwa shilingi 2,155 tunakushukuru sana na tunamshukuru Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa Alhaji Abubakar Kunenge, Baba yule anafanyakazi kwelikweli, alihakikisha anafanya *transformation* katika masuala mazima ya kilimo ndani ya Mkoa wetu wa Pwani. Namshukuru sana Mkuu wangu wa Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo makubwa mawili tu ya kushauri kwa Serikali, jambo la kwanza hili Bonde la Mto Rufiji kule ambako kuna ule mradi wanasema Rufiji *Hydroelectric Power* kuna *upstream* na *downstream,* sisi tupo kule *downstream* Wandengereko watu wa Rufiji, watu wa Kibiti pamoja na watu wa Mkuranga, ninaishauri Serikali tuweze kuangalia uwezekano wa kufanya kilimo cha umwagiliaji, nililisema hili mwaka jana lakini ninakuamini Mheshimiwa Bashe utalichukua na utakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka niishauri Serikali ni kwamba katika taratibu zetu za kufanya mambo ya mauzo ya korosho na ufuta kuna kitu kinaitwa Fomu Na. Saba.

Mheshimiwa Bashe niliwahi kukufuata katika jambo hili, tunapozungumzia suala zima la Fomu Namba Saba ni pale ambapo wale *venders* wanaonunua ufuta ama korosho wakiwa wanalipia kama tani 500, wanapokwenda katika ghala wanakuta tani 200, kwa tafsiri hiyohiyo makampuni ya *insurance* yanakuwa yanahusika kuweza kuwalipa. Mwaka jana 2021/2022 fedha ambazo mpaka hivi sasa zipo kule katika Bodi ya Maghala tunazungumzia bilioni 1.4. katika fedha hizi shilingi milioni 600 tu ndiyo zimelipwa. Kuna baadhi ya makampuni ya *insurance* hayalipi malipo hayo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Kanuni zetu za Kibunge naomba niyahifadhi makampuni hayo lakini Mheshimiwa Bashe nitakufuata nikwambie makampuni gani yanayotuangushwa. Hawa *venders* ndiyo wadau wetu wakubwa wa maendeleo, tunategemea kwa kiasi kikubwa sana tunapokuwa tuna shughuli mbalimbali za kimaendeleo wao ndiyo wanakuja kutuchangia, pale ambapo wananunua mazao halafu mazao yale hawayapati na pale ambapo panakuwa panatokea upungufu halafu hawalipi kwa wakati hii inawakatisha tamaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi nianze kwa kuishukuru sana Wizara hii ya Kilimo kwa mambo kadhaa ambayo yanaendelea kufanyika pia ninaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa nia na dhamira ya dhati ya kuimarisha

kilimo tunaiona kwenye bajeti hii na ninaamini tutaona makubwa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu nazielekeza kwa Waziri na Wizara nzima kwa jinsi wanavyoshughulikia suala la chai la Kilolo na ninawataarifu tu wananchi wa Kilolo kupitia Bunge lako kwamba muda siyo mrefu suala la Chai Kilolo litakamilika kwa jinsi ambavyo Wizara hii inalishughulikia na nina imani tutakamilisha suala hilo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili niendelee kushukuru sana Wizara hii kwa jinsi inavyoshughulikia suala la kilimo cha parachichi na uanzishwaji wa kitalu cha miche ya parachichi katika Wilaya ya Kilolo. Hapa nimtaje Dkt. Mkamilo wa *TARI* ambaye amefika kule na tayari kitalu kile kimeshaanzishwa na tunatarajia kupata miche ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokuwa hapa kwenye eneo la parachichi watu wa Kilolo tumejipanga na tunajua sasa Kilimo kinaendelea lakini changamoto ndogo tuliyonayo wanaolima sasa hivi siyo wananchi wakawaida wengi wanaolima ni wakulima wenye mashamba makubwa kidogo. Sasa hapa ninapendekezo la *block farming* kwa wakulima wadogo nitakuomba sana Mheshimiwa Waziri upokee pendekezo hili la Vijiji 25 ambavyo wakulima wadogo wadogo wataanza kulima eka moja moja na sisi tutafuta namna nzuri ni eka moja hadi tano lakini tutafuta namna nzuri ya wakulima hawa kuweza kupata *farm input* lakini kila *block* itakuwa na zaidi ya eka 50 mpaka 100 kwenye shamba moja. Kwa hiyo, tunalo hili pendekezo tutakukabidhi Vijiji 25 tuanze navyo kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo wa parachichi ili tusiwaache nyuma wananchi wa Kilolo halafu wawekezaji wengine wakaja wao wakabaki vibarua. Nitaomba nikukabidhi kwa ajili ya kulifanyia kazi na wewe nitakuomba unipe Afisa ambaye nitakuwa nafuatana naye ili hili liweze

kutekelezeka na unaijua ufuatiliaji wangu na hili nalo nitakusumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba pia Mheshimiwa Waziri kuhusu skimu chache ambazo zimetajwa kwenye bajeti ya mwaka jana, skimu ya Mgambalenga imetengewa shilingi bilioni moja lakini mpaka leo kwenye Tume ya Umwagiliaji ukiangalia kwenye randama ukurasa wa 52 utaikuta, bilioni moja ilitengwa na mpaka leo haijatolewa hata shilingi, ninakuomba kwa kipindi hiki kilichobaki skimu hii ipate basi hela hata kidogo ili ianze kutengenezwa ianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru nimeona skimu ya Nyanzwa imetajwa kwa ajili ya tathmini ya mazingira. Nimesoma ukurasa wa 82 mpaka 84 wa randama nikaona chini kuna kujenga skimu 14 na hazijatajwa. Kwa hiyo, kwa sababu tathmini yamazingira inafanyika Nyanzwa na pale chini kuna skimu 14 zitafanyika ukurasa 82 hadi 83 wa randama, naomba Nyanzwa iwemo mojawapo kati ya zile 14 ambazo nimeziona pale kwenye randama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ningependa kuliongelea hapa, Mheshimiwa Waziri umesimama hapa mara nyingi sana kukemea suala la lumbesa, watu wa kule tunalima mboga mboga *horticulture*, nakukumbusha kwamba korosho inapimwa kwa kilo huwa aina lumbesa, kawaha inapimwa kwa kilo huwa aina rumbesa, pamba inapimwa kwa kilo huwa haina lumbesa. Sasa tuje kwetu vitunguu tunavyolima vina lumbesa, nyanya tunazolima wanajua wenyewe wananvyopanga, tuje viazi vina lumbesa, mazao yote ya mboga mboga yana lumbesa, umekemea mara nyingi hapa kama imeshindikana itungwe sheria mahsusi ya vipimo vya mazao ya kilimo ili wale wananchi waweze kunufaika na kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kulikuwa na zao la *pears,* matunda tu ya kawaida na nilifika kule Kijiji kimoja cha

Ilamba, tenga moja ni kama matenga matatu, mtu anaweka mpaka atakapoamua mwenyewe ni Shilingi Elfu Kumi, lakini ni kwa sababu hakuna kipimo madhubuti kinachotumika kupima yale mazao. Ninakuomba sana pamoja na kukemea huko bado tatizo hili ni kubwa, ninakuomba tuangalie namna gani tutawakomboa wakulima wanaolima mazao ya mboga mboga ili na wao waweze kujikomboa kama haya mazao mengine yalivypata ufumbuzi kwenye suala zima la lumbesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Shabani, jiandae Mheshimiwa Masache Kasaka, jiandae Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza kabisa ningependa nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anafanya kwa bajeti hii ya kihistoria ambayo ameipatia Wizara hii ya Kilimo, Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na *crew* nzima ya Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika masuala makubwa matatu. Suala la kwanza ni suala la motisha kwa Maafisa Ugani. Wiki chache zilizopita umefanya jambo kubwa sana kugawa pikipiki 7,000 kwa Maafisa Ugani, haijapata kutokea toka Wizara ya Kilimo imeanza. Hili ni jambo la kutia moja kwa maafisa wetu wa ugani ambao wanafanya kazi kubwa kabisa katika kuinusuru sekta hii ya kilimo nchini. Vilevile nilikusikia ulimuomba Mheshimiwa Rais kwamba pikipiki zile wakizitumia kwa muda wa miaka miwili basi wazichukue ziwe mali yao, hili ni jambo kubwa sana na jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba isiishie hapo tu hawa Maafisa Ugani sasa hivi wanatakiwa wapangiwe utaratibu kwa mazao yote ya kimkakati katika Mikoa, wanatakiwa sasa hivi waambiwe kabisa kwa mfano, ile sehemu ambayo wanatakiwa walime alizeti wapewe kiwango au *target* kwamba tunataka Mkoa fulani mzalishe tani fulani na mtakapozalisha tani fulani za alizeti basi mtapata *percent* fulani itakuwa mali yenu, ninakuakikishia hao watafanyakazi usiku kucha hawatalala kwa sababu ya kufukuzia hizo *percent* ambazo utawapatia na mambo yatakuwa mazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu umwangiliaji, nimeona bajeti kubwa sana ya umwangiliaji imeongezeka kutoka Bilioni 46.5 mpaka Bilioni 361.5 haya ni mageuzi makubwa sana. Lakini kuna sehemu ambazo umezisahau katika miradi ya umwagiliaji, kwa mfano pale kwangu Bangamoyo kuna skimu ya umwangiliaji ya Ruvu maarufu kama *JICA* haimo kabisa katika mpango wako, siyo tu Bangamoyo nimesoma *almost* hotuba yako yote, Mkoa wote karibu skimu niliopata ni moja tu ambayo iko Rufiji inaitwa Ngongoro ambayo iko katika upembuzi yakinifu, lakini katika skimu za umwangiliaji zilizofanyiwa upembuzi yakinifu hakuna, skimu za umwangiliaji za Mwaka wa Fedha 2022/2023 hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyotambua Bangamoyo kuna mradi mkubwa sana, sasa hivi tunawaandaa *outgrowers* kwa ajili ya kilimo cha miwa ili waweze kulisha shamba la Bagamoyo *Sugar* lakini hakuna utaratibu wowote na wala hakuna mpango wowote wa kujenga bwawa au kuweka miundombinu ya umwangiliaji kwa ajili ya kunusuru wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho ni la uboreshaji wa masoko, tutakuwa tunasema kilimo tunapanga mipango ya kulima kwa bidii zote lakini tusipokuwa na

masoko kwa bidhaa zetu tunazolima tutakuwa tunajisumbua. Lazima tuwekeze nguvu zetu sasa hivi kuhakikisha kwamba tunapata masoko kwamba wananchi wanapohamasishwa kulima wanalima lakini baadaye inakuja wamelima kwa nguvu zote, masoko hakuna wanarudi nyuma, mwaka unaofuata hawalimi tena Taifa linakuwa kila siku linapiga *mark time* tu haliendi, kwa hiyo tuelekeze nguvu zetu katika Maafisa wa Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ikiwezekana hawa Maafisa wa Masoko waambieni kabisa mtu atakayetutafutia soko la bidhaa fulani nchi fulani tutampa kamisheni kutokana na mauzo yatakayofanyika ya yale mazao ambayo yataunzwa katika nchi husika. Kwa hiyo hapa kutakuwa na jitihada kubwa sana ambayo inafanyika watajitahidi, vilevile tusisite tuongee na Wizara ya Mambo ya nchi za Nje, tuwatumie *diaspora* kule watutafutie masoko ya bidhaa zetu kwa sababu tunalima. Tumeona miaka miwili iliyopita anguko la mbazi, mbaazi ilikuwa bei yake kubwa sana, mimi niliwahi kulima mbaazi, niliuza kilo Shilingi 2,300 shamba kipindi cha nyuma, lakini baadaye mbaazi ikashuka ikawa inauzwa mpaka Shilingi 300 kwa kilo na wanunuzi hakuna. Sasa lazima tujipange kuhakikisha kwamba masoko yanafanyiwa kazi na hawa Maafisa Masoko waandaliwe ili waweze kuinusuru Wizara na kulinusuru Taifa ili liweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka jiandae Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu. Kwanza niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutuletea bajeti hii ambayo sasa imeakisi kwamba Serikali imekuwa na dhamira ya dhati kabisa kuweza kumkomboa mkulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ujumla kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Pamoja na dhamira kubwa ambayo Serikali imeendelea kuifanya kwenye Wizara hii, tunaona namna ambavyo kule kwetu ambako tunalima zao la tumbaku wameweza sasa kuona umuhimu wa zao hili na kuhakikisha kwamba tunakwenda kupata makampuni mengine zaidi kwa ajili ya kununua zao la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Serikali imepata kampuni, kampuni ya *AMIS* ambayo nayenyewe tayari imeshachukua kiwanda cha kichakata tumbaka pale Morogoro na wametuhakikishia kwamba kwenye mwaka huu wataweza kununua tani milioni 10, tunawapongeza kwa kazi kubwa ambayo mmefanya, yale ambayo tulikuwa tunawashauri mmeyachukua na mmeenda kuyafanyia kazi, tunawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo hii kampuni imetuhakikishia kwamba mwaka ujao wa kilimo itanunua tani Milioni 30, hii maana yake tunaenda kuongeza makisio kwa wakulima wetu wa zao la tumbaku na tutakapoongeza makisio watalima zaidi na wanapolima zaidi maana yake uchumi wao utakukua. Ninawaambia wakulima wangu wa Tarafa ya Kipembawe Wilaya ya Chunya wajiandae sasa kampuni hii inakuja, makisio yataongezeka hivyo uchumi wa eneo husika utaenda kukuwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo bado kuna changamoto kwenye mbegu na miche ya tumbaku. Tumeona kwenye hii bajeti upande wa utafiti, maeneo mengine wamewekewa fedha lakini upande wa mbegu za tumbaku na miche ya tumbaku hawajawekewa fedha, hii kampuni ya utafiti ya *TORITA* haijawekewa fedha. Ninaiomba Serikali kama ina dhamira ya dhati kabisa ya kuhakikisha kwamba zao hili linaenda kumkomboa mkulima mwaka ujao

waweke fedha ili ziweze kuwasaidia kupata mbegu ambayo ni bora na tunaweza kupata tumbaku ambayo ni nzuri zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu watu wa Malawi pamoja na Zimbabwe wamewekeza kwenye utafiti, wamewekeza kwenye mbegu bora za tumbaku. Wao wanapata tumbaku yenye daraja la juu zaidi. Sisi tumbaku yetu iko chini na ndiyo maana hata bei ya tumbaku Tanzania iko chini. Tuna wastani wa dola 1.4 mpaka wastani wa dola 2.2 ambayo iko chini, wakati wenzetu wananunua kuanzia dola mbili na kitu na bei ya juu ni dola nane. Kwa hiyo, tukiwekeza huko tutaweza kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nizungumze habari ya pembejeo. Serikali imeongeza ruzuku kwenye bajeti hii kwa ajili ya pembejeo, ni jambo zuri sana, nasi tunapongeza kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya. Tunampongeza sana Waziri kwa ubunifu wake huo. Tuna imani wakipata fedha ambazo wameziomba, bei ya pembejeo inaenda kushuka. Sisi sote tumekuwa mashahidi huu musimu wa kilimo uliopita hapa, bei za pembejeo zilikuwa hazishikiki. Kila Mbunge hapa alikuwa analalamika kwamba pembejeo ziko juu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nicodemas Maganga, jiandae Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na fursa hii

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mdogo naomba nijikite kushauri tu kwa maneno machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia katika hotuba hii ya Waziri yote, na ninaomba nishauri mambo machache. Waziri aangalie kumlenga mwananchi mnyonge wa hali ya chini katika bajeti hii ya Shilingi milioni 751. Nakuomba rafiki yangu pamoja na Naibu Waziri Mavunde, msipoangalia hizi fedha zinaenda kuishia kwenye mikono ya watu wachache, hazitamsaidia mwananchi yule wa kawaida anayelima kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, hisia za Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wote, pamoja na hotuba zote tukiwa kwenye kampeni mwaka 2020 tuliahidi kwamba tutawasaidia wanyonge. Nakuomba Waziri kupitia ubunifu uliouunda kutengeneza kombati pamoja na mavazi *special* kwa ajili ya mkulima, ufuate mfumo huo huo, tengeneza programu nyingine, acha kutegemea mabenki. Wakulima huwa hawana akaunti benki, lazima ulijue hilo. Wazazi wetu hawana akaunti benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia mkulima, lazima umfikirie mkulima yule wa hali ya chini. Unaenda kumwezeshaje aliye na jembe la sheli ya ng'ombe? Unaenda kumwezasheje yule anayelima kwa jembe la mkono? Mheshimiwa Waziri fikiria mambo kama yale, tutaonekana watu wa maana, washauri wazuri, ukifuata ushauri wangu huu wa mwishoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kule Mbogwe ninazo sehemu nyingi sana, sioni hata sababu ya kufanya utafiti. Kitu kikubwa sana sana huwa ni mvua tu. Mheshimiwa Waziri sijui unanisikia! Sijui umeangalia pembeni! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa, naomba aje na Mpango, Wilaya ya Mbogwe ananisaidiaje? Ninazo Mbuga kubwa ambazo zinahitaji *scheme,* ukinisaidia skimu hata 20 hutasikia njaa katika Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nikupongeze tu Mheshimiwa Waziri, mwaka 2021 ukiwa Naibu Waziri nilikuja kwako nikalia kuhusu kiwanda changu cha Kagiri kile ulichokuja kukiangalia na kukifungua. Ulinipatia Shilingi bilioni sita na mwenyewe umeyaona matokeo, tumeingiza faida pamoja na wanakulima wanapewa ruzuku. Mwaka huu tumeandika andiko, tunataka Shilingi bilioni 13, tunataka tuzalishe mafuta wenyewe ya pamba pale Mazumbwe Kagiri na tunataka tuzalishe mafuta ya alizeti. Usisite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara na wakulima tunajuana, ukisema unahitaji kusaidia wakulima kupitia Jeshi lile ulilolígawia pikipiki, sasa hivi wanawajua wakulima. Usiangalie watu wanaokimbia sasa hivi kusajili makampuni, wanakuja kukuangusha hao Waziri, waepuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiria mwaka 1992 katika utawala wa Rais Mwinyi, tulikuwa tukiletewa mbegu za pamba mpaka Kijijini. Sasa hivi mnashindwaje kutuletea moja kwa moja mbegu za pamba, tukalima pamba na tukafaidika? Kwa nini mnapitia Mawakala? Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kulifikiria hilo. Wewe uzuri umezaliwa kwetu huko, unajua maisha ya Kijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha naomba zisiishie mjini, zisiende kwa watu wenye makampuni ya mjini. Wakulima walio wengi huwa hawana akaunti. Utaweka akaunti vipi wakati wewe ni Mkulima! Kwa hiyo, kupitia watu wako wale uliowapa pikipiki Mheshimiwa Waziri, wewe kaa nao, waulize huko una wakulima wangapi; ili uweze kuwasaidia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. Mchango mwingine nitaandika kwa maandishi,

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, jiandae Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie. Mheshimiwa Waziri anajua kwamba Bunda tunalima pamba na kuna *ginnery* za pamba Bunda zimekufa. Wananchi wa Bunda wana *stress* kwenye mbegu, *stress* kwenye masoko, *stress* kwenye *ginnery* ambazo zilikuwa zinatengeneza ajira kwa vijana wengi wa Bunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Waziri maghala 24 ya kuuzia pamba na kuhifadhia yako kwenye hali mbaya. Mheshimiwa Waziri Misisi, Sazila, Mlimani Ligamba, Mheme, Taramanka, Balili, Kunzugu, Bukole, Mihale, Nyamatoke, Changuge, Jembemali, Mchalo, Jitume, Kisangwa, Tairo, Guta, Ibiti, Kunanga, Rwagu, Nyamilila, Kabasa, Kamkenga, Kalisumu, Bitaraguro, Kagetutya, Lindala, Kiwasi na *Bunda Store;* hizi zote zina hali mbaya. Pamba itaenda kuuziwa wapi? Itaenda kuhifadhiwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Mheshimiwa Bashe najua ni mchapakazi, ametoka kwenye maeneo yanalima pamba. Wananchi wa Bunda baada ya kuona hivi, wanataka kujua Serikali mtakarabati lini haya maghala

wanusuru kilimo hiki cha pamba ambacho ni kilimo ambacho kinachowasaidia wananchi wa Kanda ya Ziwa? Wananchi wa Mkoa wa Mara, wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona kuna tatizo hili, wananchi wa Bunda wamejiongeza, wanaanza kulima alizeti. Hivi ninavyozungumza, Mheshimiwa Waziri wametenga hekta 10,000 kwa ajili ya kilimo cha alizeti, lakini hamjawapelekea mbegu. Sisi pale Bunda tunahitaji tani 30 tu za kuanzia na wamepanga kuvuna kilo 4,000,000 za alizeti ambazo watakuwa na uwezo wa kuzalisha mafuta lita 1,080,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huku wameshindwa kujikamua, wamejiongeza kwenda kwenye alizeti, tena kwenye Kata ya Guta, Kabasa, Sazila, Waliku, Mcharo na Kunzugu. Naomba sana tupelekee mbegu. Kule Maafisa Ugani wako tayari, hata kama wengine wa pale Mji wa Bunda mnawachelewesha kuwapandisha madaraja. Sijui tumeelewana kaka yangu Mheshimiwa Bashe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku mtukarabatie maghala, lakini huku kwenye alizeti tunaomba mbegu. Tuna *target* ya kuvuna lita 1,080,000 za mafuta.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Bashe…. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Chikota. Jiandae Mheshimiwa Kapinga na Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko Mezani. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa dhati wa kuongeza Bajeti ya Kilimo kutoka Shilingi bilioni 294 mpaka Shilingi bilioni 751. Haya ni mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwapongeze viongozi wa Wizara hii; Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Mavunde pamoja na Katibu Mkuu na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unajikita kwenye zao la korosho na nianze na soko la korosho na bei ya korosho. Naomba Wizara iimarishe Kitengo cha Masoko katika Wizara hii lakini pili, na Bodi ya Korosho ili korosho yetu ipate bei nzuri sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoendelea sasa hivi kwenye Mnada wa Korosho, tunapata bei nzuri kwenye mnada wa kwanza na minada yote inayofuata korosho bei inashuka. Hatujui kushuka huku ni kwa kupanga au ni kwa sababu soko limeshuka. Tukiwa na taarifa za kutosha kwenye soko, basi itasaidia kupata taarifa za uhakika na kuimarisha bei yetu ya korosho na kudhibiti uuzaji wa korosho katika minada.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kuhusu ubanguaji wa zao la korosho. Tuna mkakati wa kubangua zao la korosho. Tulikuwa na viwanda vyetu 12 hapo nyuma mpaka sasa hivi havifanyi kazi na vingine vimegeuzwa kuwa magodauni. Mheshimiwa Bashe wewe ni bingwa wa kuthubutu, chukua angalau viwanda vitatu vianze kubangua

korosho na hilo unaliweza ili tuanze kubangua korosho badala ya kupeleka korosho ghafi huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni kuhusu pembejeo. Naipongeza sana Wizara kwa kutoa pembejeo bure kwa wakulima na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa mwaka wa pili kutoa pembejeo bure kwa wakulima wa korosho. Naomba udhibiti ufanywe ili pembejeo hizi zifike kwa wakulima husika na siyo mikononi mwa walanguzi. Pili, pembejeo hizi sasa wasambazaji watoe mafunzo kwa wakulima kama ilivyofanya Kampuni moja ya BEZ naipongesa sana. Imetoa mafunzo kwa wakulima ili kupunguza dosari za utumiaji wa dawa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu lingine ni kuhusu *Export Levy*. Mheshimiwa Waziri utakuja na Muswada hapo wa *Export Levy* ili fedha isiwe chanzo cha mapato kwa Serikali. *Export Levy* irudi kwa mkulima ili iongeze uzalishaji, ili tufufue viwanda vyetu vya korosho, ili iimarishe utafiti, ili ile fedha ambayo anachangia mkulima sasa hivi Shilingi 25/= kwa ajili ya TARI Naliendele asikatwe mkulima, ichukuliwe kwenye *Export Levy*. *Export Levy* itasaidia kutoa uhamasishaji kwa wabanguaji wa korosho. Kwa hiyo, naomba kwenye Muswada wa Fedha ujao, basi utuletee ili *Export Levy* irudi na asilimia 65 iende kwenye zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, jiandae Mheshimiwa Joseph Tadayo na Mheshimiwa Emmanuel Ole-Shangai.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara naona wamejipanga vizuri, na tumeona mwanzo umekuwa mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitaongelea hoja moja ya Kahawa. Nampongeza sana Waziri, kwa muda mfupi ametoa taarifa, ameanza kusambaza miche ya kahawa katika maeneo yale yanayolima kahawa. Kwa bahati mbaya, sisi wana Mbinga tunalima kahawa na kwa bahati mbaya hatukupata miche. Nina uhakika kwa sababu ulikuwa mwanzo, sasa hivi ataenda kutoa miche Wilayani Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mbinga wamenipigia simu hapa, wana imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri. Wanaomba kwamba akimaliza bajeti hii, basi apange muda akawatembelee. Wako tayari kumpokea na wana mashamba wameandaa, wanachosubiri sasa hivi ni miche ya kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, suala la Bodi ya Kahawa. Mimi sifahamu, Bodi nyingine unasikia zimechangamka zinafanya hivi, lakini Bodi ya Kahawa sisikii chochote. Kwani wao siyo Bodi kama Bodi ya Pamba? Kwani wao siyo Bodi kama Bodi ya Korosho? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ongea na huyu Bwana wa Bodi ya Kahawa, kwa sababu tunataka tuone nchi inachangamka. Kama Korosho Bodi inafanya hivi, Pamba inafanya hivi tunataka kuona na Kahawa pia mtu wa Bodi anafanya kitu fulani. Mpaka saa hizi sijaona Bodi inafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliweka malengo ya kuongeza uzalishaji kwenye kahawa, lakini sijaona mikakati hasa ya nini kinaenda kufanyika. Kama Bodi, wao wanafanya nini? Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, najua umejipanga vizuri kwenye hili na ulininong'oneza pembeni kwamba Mbinga watapata miche mingi kwa sababu Kahawa ya Mbinga ni nzuri zaidi halafu tamu na inapendwa zaidi duniani huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la mbolea. Sisi wana-Mbinga bila mbolea hatujavuna. Tunamshukuru Mungu safari hii tulitumia miujiza. Maana yake mfuko mmoja tumetumia zaidi ya ekari mbili mpaka tatu. Kwa hiyo, tunashukuru mazao yamekua lakini uzalishaji hautakuwa kama ule tuliouzoea miaka yote. Kwa hiyo, uzalishaji kidogo utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa lile wazo la ruzuku ya mbolea. Nami nikuomba suala hili kama ulivyosema jana, uko tayari ukose vingine vyote lakini tupate ruzuku ya mbolea. Mbinga ni wazalishaji wakubwa wa mahindi, lakini hatuwezi kuzalisha bila mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huu mfupi, nashukuru sana. Nilikuwa na mambo hayo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Tadayo, jiandae Mheshimiwa Emmanuel Ole-Shangai na Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niungane na wenzangu wote kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya kwa ajili ya nchi yetu. Tanzania inaona na dunia inaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, kazi yao ni nzuri na wametuletea bajeti yenye matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko mdau mmoja wa mambo ya uchumi alikuwa akizungumza juzi juzi kwamba utajiri uliyoko juu ya ardhi ni mkubwa kuliko ulioko chini ya ardhi. Utajiri ulioko juu ya ardhi ni katika maana ya kilimo na ulioko chini ya ardhi katika maana ya madini. Kinachokosekana tu ni uwekezaji. Kwa uchumi kama wa kwetu ambao unategemea wakulima wadogo, kilichokuwa kinakosekama ni kile ambacho kipo kwenye ukurasa wa 14 wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri kuongeza nguvu kwenye utafiti, kuongeza nguvu kwenye ugani, umwagiliaji na ubora wa mbegu. Yakitekelezwa haya kama Mheshimiwa Waziri alivyotuletea, basi nadhani maneno haya ya mdau huyu yatatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mwanga maeneo yote ya milimani yalikuwa yakitegemea zaidi uchumi wa kahawa ambao hapo katika ulidorora kidogo kutokana na matatizo haya ya ugani pengine na masoko, lakini sasa hivi ari kubwa ya kahawa imerudi. Tunachoiomba Serikali ni kupatiwa mbegu tu, yaani miche ambayo inahimili hali ya kule milimani ambayo pia haihitaji dawa nyingi kwa ajili ya kukua na kustawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo skimu tatu kubwa za umwagiliaji. Kwanza ni Skimu ya Kirya ambayo nashukuru sana kwamba tulipata fedha inaendelea. *Potential* ya ile skimu ni hekta 1,600, lakini Mkandarasi aliyeko *site* akikamilisha tutaweza kutumia hekta 950. Tunashukuru na tunaamini tutaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu ya pili ni ya Kivulini Kileo ambayo ina *potential* ya hekta 1,550, lakini zinazotumika ni hekta 712. Tunaomba tupatiwe fedha ya kumalizia ili skimu hii ifanye kazi kwa asilimia 100. Pia tupatiwe maghala na mashine za kukaushia mpunga. Kwa sasa hivi wanaanika nje, hali ambayo haileti ubora mzuri wa mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu yetu ya tatu ni Skimu ya Kigonigoni. Mheshimiwa Waziri nakushukuru, ulipokuwa Naibu Waziri ulikuja Kilimanjaro ukanipa *breakfast* pale *Kili Wanders,* nami sikulipa, ni wewe ulilipa, nakushukuru sana. Ukanishauri juu ya Skimu hii ya Kigonigoni kwamba tutafute fedha tufanye upembuzi yakinifu. Tulifanya hivyo na hiyo kazi imefanyika, sasa hivi wako kwenye *designing.* Ile skimu ina *potential* kubwa sana ya hekta 2,300.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba Mheshimiwa Waziri ni kwamba tutakapokamilisha upembuzi yakinifu hivi karibuni, basi tusaidiwe fedha kupitia kwa wadau wa maendeleo kama *IDF* na *JICA* tusije tukasubiri tena bajeti ijayo. Naamini kabisa tutakamilisha upembuzi yakinifu ndani ya muda kwa sababu umetupa kijana mzuri sana, *Eng.* Said pale Mkoa wa Kilimanjaro. Tunachoomba tu ni kwamba aongezewe nguvu hasa *manpower* kwa sababu wataalam pale ni wachache na wanakimbiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda, naomba nimalizie mchango wangu hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Emmanuel Ole-Shangai, jiandae Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Waziri Ndaki.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa upendo wake kwa Watanzania kwa kukubali kutenga fedha nyingi kwa ajili ya

Wizara hii ya Kilimo. Kama tunavyojua, kilimo kimewaajiri Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote kwenye Wizara hii. Ni wasikivu sana. Jana tu nilikuwa na tatizo kwenye Jimbo langu lakini nimemplekea Mheshimiwa Waziri na watendaji wake, wameshafanyia kazi. Hawa ni watendaji, ni watumishi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana bajeti hii, kutoka Shilingi bilioni 294 mpaka Shilingi bilioni 751 ni ishara kwamba tumeamua sasa kuwakwamua wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kitu kimoja. Kwenye Wilaya ya Ngorongoro kuna maeneo mengine ambayo sasa hivi tunatafuta namna ya kupata maji, lakini sisi kwenye Kata za Pinyinyi, Oldonyosambu, Digodigo na maeneo mengine kama Engaresero, Enguserosambu kuna maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa ni kuweka miundombinu kwa ajili ya wananchi wetu kuanza kunufaika na mfumo wa umwagiliaji. Tukijaribu kuangalia kwa mfumo wa sasa hivi wa dunia, watu wengi wamekwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kwa nini, na nchi nyingi, kwa nini wameamua kwenda? Ni kwa sababu kilimo cha umwagiliaji ndicho kilimo cha uhakika kuliko kilimo cha kutegemea mvua. Tukichukulia mfano mwaka huu, watu gani wana uhakika wa kuvuna ni watu wanaotegemea kilimo cha umwagiliaji. Kwa sababu kwa wale wanaotegemea kilimo cha mvua wengi wamepata hasara hakuna mvua za kutosha. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuamua sasa kuangalia katika mfumo huu wa *irrigation system* ambao utakwenda kuwakwamua Watanzania wengi

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri, kwenye Wilaya yetu ya Ngorongoro wananchi wanapata hasara sana kwa sababu hawana hata ghala moja kwa ajili ya kuhifadhi chakula kipindi cha mavuno. Inawabidi wauze mazao yao kwa bei ya hasara; kwa sababu hawana namna ya kuhifadhi. Kwa hiyo, nikuombe kwenye Wilaya yetu ya Ngorongoro kaangalie kwenye mifuko yako yote, chonde chonde utupe angalau ghala moja kwa ajili ya wananchi kuhifadhi chakula chao. Kila mwaka sisi tumekuwa tukiuza chakula, mahindi kwa Wakenya kwa sababu hatuna maeneo ya kuhifadhi, na wao wanatumia *opportunity* hiyo kuja kununua chakula mpaka mashambani; ni lazima tuwalinde wakulima wetu namna ya kunufaika na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine niombe tupeleke mbolea pia. Ukienda leo Kata ya Pinyinyi, ni eneo ambalo tukiamua kuwekeza tutazalisha mbegu nyingi sana. Sasa hivi Kampuni ya Kibo *Seeds* wanawapa wakulima mbegu za alizeti na bamia wanazalisha halafu wanawapa bei wanayotaka wao. Lakini Serikali pia tunaweza kuzalisha mbegu katika eneo lile, ukienda kwenye Kata ya Oldonyosambu tunaweza tukatumia maji yaliyopo kwaajili ya wananchi kunufaika. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri tuwasaidie wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niomba kitu kingine, kuna tatizo la *emergence services* kwenye Wizara ya Kilimo pia. Mwaka huu mwanzoni mwezi wa tatu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ole-Shangai,,

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI…**, wananchi walipata shida sana. Nashukuru sana niunge mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Wizara ya Kilimo. Kwanza niishukuru Wizara kwa kupitia Waziri wake Mheshimiwa Bashe na wenzake wote na Mavunde wanafanyakazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni moja tu, jana nimesikiliza Ufaransa, wanasema Waziri Mkuu waliyopewa Ufaransa baada ya Emmanuel Macron kushinda ni mwanamke. Kwa hiyo, wenzetu nao wanaanza kuiga nchi za kiafrika kama Tanzania, kwamba akina mama wanafaa kushika uongozi wa ngazi ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini dhana yangu hapa nataka kuzunguza ni kitu kimoja tu kwamba, kilichompa uongozi wa uwaziri mkuu ni kwamba alipokuwa Waziri wa Kazi aliongeza ajira za kutosha Ufaransa. Sasa kwa nini, kwa sababu nchi za wenzetu ukimpa Waziri kazi unamuamini na unampa *full mandate* ya kufanya kazi hiyo. Mama Samia amekuja kwenye nchi yetu amewapa mawaziri wetu madaraka yote wafanye. Leo nchi yetu ikifeli kwenye kilimo; na ni wazo tu, kuna Waziri mmoja alikuwa anazungumza hapa juzi, akasema "*akili ya afya*"; alikuwa anazungumza Mbunge mmoja, sahani siyo Waziri; Mbunge mmoja, Balozi, anasema akili ya afya Watanzania inafanya tunakuwa masikini. Waheshimiwa Wabunge tumuachie Mheshimiwa Bashe na watu wake na Mheshimiwa Mavunde na watu wake. Kwa sababu wana uwezo wa kuonesha wana uwezo wa kufanya kazi tuwaachie madaraka yote wafanye tuone. Tumuulize Bashe wizara kwenye bajeti ijayo kitu gani kitafanyika?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, taarifa yangu ni fupi tu, kaka yangu Mwita pale anachangia anasema "akili ya afya" ni "afya ya akili" siyo "akili ya afya". *(Makofi/ Vicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dada yangu ni Kiswahili na mimi Kiswahili sikijui, namshukuru tuendelee. Kwa hiyo, niombe tuwape mandate ya kutosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuzungumza jambo moja kubwa sana. Waziri Bashe atuambie atakapokuja hapa, ni mikakati gani ataweka ili kuokoa ushirika nchini? Ushirika wetu umeyumba kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kuwepo kwa ushirika nchini ni nzuri sana, lakini ushirika wenyewe umekuwa na uwezo wa kutosha. Ni kitu gani anafanya, ni sheria gani atatumia, ni kanuni gani atatumia, kama ni kanuni ndogo au kanuni kubwa, ni utaratibu gani atatumia kupunguza wezi wa mali za ushirika nchini? Atuambie mikakati yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru Mheshimiwa Bashe Mheshimiwa Rais wameleta Pikipiki 7,000. Niwaombe sasa, hizo pikipiki 7,000 basi akazifungie *GPS*. Pikipiki ukipeleka huko mtu anaishi Bunda, pikipiki inakaa Bariadi; mtu anaishi Tanga pikipiki inakaa Pwani. Pikipiki zetu zimekuwa za kutembeza kama bodaboda zifungieni *GPS* ili watu wajulikane wapo wapi, wanafanya kazi gani, wanafuatilia nini nadhani hili litakuwa jambo zuri sana kuwadhibiti wale

maafisa ugani ambao umewapa nafasi ya kuhudumia wakulima…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, aidha nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo kuelekea uchumi wa wakulima wetu. Serikali yetu inaendelea kutilia mkazo wananchi kujishughulisha na kilimo. Lakini kilimo chenye tija ni lazima kiandaliwe kwa kuwapatia wakulima wetu pembejeo za kilimo kwa wakati. Mpaka sasa kuna baadhi ya maeneo katika nchi yetu huwa wanasumbuka,

aidha kutopata pembejeo kwa wakati au kukosa kabisa kwa baadhi ya miongo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali katika jambo hili la pembejeo ni kuhakikisha wakulima wetu wanapata pembejeo hizi kwa wakati na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, pili kuwawezesha wakulima wadogo wadogo; wakulima wetu wengi katika nchi yetu ni wanyonge sana. Uwezo wao wa kujiendesha kiuchumi ni mdogo sana. Wakulima wetu wanashindwa hata kuanza kilimo kwa sababu ya unyonge. Hivyo basi ni lazima Serikali yetu iwaunge mkono katika kilimo chao. Wengi huwa wanakimbilia kwenye mikopo ambayo baadae huwa wanashindwa hata kurejesha mikopo hiyo kutokana na masharti magumu. Riba kwenye mikopo ni miongoni mwa vihatarishi vikubwa kwa wakulima wetu.

Ushauri wangu katika suala hili la riba kwa mikopo ya wakulima ni Serikali kudhibiti kabisa viwango vya riba kwenye mabenki yetu ili kuondoa kabisa vihatarishi vinavyopelekea kufilisiwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji; mabadiko ya hali ya hewa ulimwenguni yanaathiri mwenendo wa kilimo kwa kutegemea mvua. Nchi nyingi pamoja na Tanzania hivi sasa zinapata mazao hafifu kwa kutegemea mvua. Wengi wanaelekea kwenye matumizi ya kilimo cha umwagiliaji.

Ushauri wangu kwenye jambo hili ni Serikali iendeleze mikakati ya mpango wa kilimo cha umwagiliaji kwa kueneza *scheme* za kilimo kwenye maeneo yote nchini. Pia Serikali iendeleze zoezi la kuwa elimisha wakulima wetu faida za kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Kilimo, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya Wizara ya Kilimo, Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo cha mazao, kwa wastani hekta milioni 10.8 tu sawa na asilimia 24 ndizo zinazolimwa kila mwaka. Sekta hii kwa mwaka 2020 imechangia asilimia 26.9 kwenye Pato la Taifa, imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 61.1 na imechangia asilimia 65 ya upatikanaji wa malighafi za viwanda. Sekta ya kilimo ni mhimili wa uchumi wa nchi na inachangia pato la mkulima mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla. Sekta ya kilimo na hususani sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 15.4 katika Pato la Taifa na zaidi ya asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula kinachozalishwa nchini na kupelekea kupunguza mfumuko wa bei kwa takribani asilimia 59.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujitosheleza kwa chakula na kuchangia katika uchumi wa Taifa, takribani mazao yote yanazalishwa kwa tija ndogo katika eneo husika. Uzalishaji wa mahindi wa tani 1.76 kwa hekta moja ni asilimia 29 tu ya uzalishaji unaotegemewa wa tani sita kwa hekta moja. Uzalishaji huu wa chini kwa mazao yote unatokana na ukosefu wa ushauri wa watalaam wa kilimo ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na pembejeo zingine. Katika hali hii, kilimo hakijamsaidia mkulima kwa kiasi kikubwa kunajinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea nchini hadi Februari, 2022 ulikuwa tani 436,452 sawa na asilimia 63 ya mahitaji ya tani 698,260, lakini kutokana na bei kubwa ya mbolea mauzo yalikuwa tani 173,957 tu sawa na asilimia 25. Wakulima wengi walishindwa kumudu kununua mbolea kutokana na mfumuko wa bei wa asilimia 100 na ikichangiwa na hali isiyoridhisha ya mvua inaweza kupelekea upungufu wa uzalishaji hasa mazao ya nafaka. Napendekeza Serikali ichukue hatua za kurudisha ruzuku ya pembejeo pamoja na kuanzisha *Price Stabilization Fund* kwa pembejeo hasa mbolea ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iendelee kuimarisha usalama wa chakula nchini kwa kununua na kuhifadhi nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Kutokana na vita ya Urusi na Ukraine kunaashiria upungufu mkubwa wa nafaka na kwa kuzingatia gharama kubwa za uzalishaji wa karibu asilimia 100, Serikali ichukue hatua za makusudi kusaidia wakulima wapate bei nzuri ya *NFRA* badala ya kuuza kwa walanguzi na kutorosha chakula nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie fursa za kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuanza uzalishaji wa viatilifu

inayotokana na pareto ambayo inazalishwa hapa nchini na imekuwa inauzwa nchi za nje kama *semi-finished product* kwa bei ndogo ya kutupa. Viatilifu kutokana na pareto ni suluhisho la soko la pareto na pia suluhisho kwa upotevu wa mazao kushambuliwa na wadudu *(post-harvest losses)*. Pia Serikali ianze mchakato wa kutumia madini *(calcium carbonate, agricultural lime, phosphates, natural gas etc.)* yanayopatikana kwa wingi hapa Tanzania, kuanza uzalishalishaji wa mbolea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2021/2022, Serikali ilitenga shilingi 164,748,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi 82,180,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 82,568,000,000 ni fedha za nje. Utekelezaji wa miradi hadi kufikia Februari, 2022 hasa utekelezaji kwa fedha za nje uko chini sana. Kutokana na hali hii sekta ya kilimo imeendelea kudorora katika kuchangia Pato la Taifa. Matumaini pekee ni hatua zilizooneshwa kwenye bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na Serikali iweke mikakati madhubuti kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa bajeti hii ya umwagiliaji. Pia mikakati hii iweke nyongeza za ujenzi wa mabwawa hasa maeneo yenye mafuriko makubwa ikiwa ni pamoja na kuzuia mafuriko.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye mradi wa Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Programme - SRBDP)*, wenye ofisi zake Kyela, Tanzania. Mradi huu unaotekelezwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi, ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za haraka kuleta Bungeni mapendekezo ya Sheria ya Kilimo ambayo pamoja na mambo mengine itawezesha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi. Pia kutokana na changamoto za tabia nchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Napendekeza Serikali iongeze msukumo kwa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchango na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**INSERT NO 03**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaki.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa nchi yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa uthubutu wake kuweza kuongeza bajeti kwenye Wizara hii ya Kilimo ambayo ni uti wa mgongo wa Watanzania wote. Lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Mavunde kwa namna ambavyo wamepangilia na kujitayarisha

kufanya kazi kwa ajili ya Watanzania wote wanaoshughulika na kilimo kitaalam kabisa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja tu ambalo mimi nataka kutoa ufafanuzi nalo ni suala la wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima, mashamba ya mahindi ama mazao mengine. Suala hili limezungumzwa kwa uchungu, sauti, inayoeleweka na Mheshimiwa Alexia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, Morogoro. Nipende kusema tu, hakuna sheria ya nchi yetu inayoruhusu wafugaji waende kuchunga kwenye mashamba ya wakulima ambao wamelima mazao yao. Hakuna sheria ya namna hiyo. Hata sheria zinazotuongoza kutenga maeneo ya kufugia hazisemi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia nimewahi kuchunga mifugo, ilikuwa marufuku kwenda kupeleka ng'ombe kwenye shamba la mtu la mahindi au mazao mengine na kulisha; ukifanya hivyo ukirudi nyumbani utapata adhabu kali; na familia yenye ng'ombe iliyokuwa inafanya hivyo, inachukua ng'ombe wake inakwenda kulisha mashamba ya watu wengine ilikuwa inajulikana kama familia ya watu wenye dharau, wasio na heshima na hivyo ilitengwa kwa namna fulani, hata ikiwa na mabinti wazuri kiasi gani, mabinti wale walikuwa hawaolewi kwa sababu wanatoka katika familia yenye dharau. Hata ikiwa na vijana wa kiume wazuri jinsi gani, vijana wale hawawezi kuoa kwenye kile kijiji, wataoa kijiji cha mbali ambako hawajulikana kwamba wanadharau na familia yao inadharau kwa sababu inatabia ya kupeleka mifugo yake kwenye mashamba ya watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, vitendo hivi havikubaliki. Niombe tena wafugaji popote mlipo, nchi yetu inaruhusu tuishi mahali popote ili mradi tusivunje sheria za nchi. Sasa wafugaji acheni kupeleka mifugo yenu kwenye mashamba ya wakulima, hairuhusiwi kwa sheria zetu; sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi miongozo yetu inakataa. Tuna miongozo ya malisho

na rasilimali za vyakula vya mifugo. Hakuna mahali tumetaja mifugo ikale mazao ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana sana sana, tunaendelea kutoa elimu kama Wizara ili kuwaelimisha wafugaji waelewe na wasipeleke mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana viongozi, ngazi za Serikali za vijiji, Kata, ngazi za wilaya waangalie jambo hili. Jambo hili linatokea na wenyewe wapo pale. Wakulima wanapigwa, wanadhulumiwa mazao yao, kusema kweli ni kama kitendo cha kuhujumu uchumi; kwa sababu tunafahamu, mkulima ametegemea amelima hekali zake tatu, amefikia mahali pa kuvuna, halafu mifugo inaachiwa inakula mazao yote. Maana yake huyo mkulima kwa mwaka mzima atakuwa hana kipato, chakula, kwa hiyo hana namna ya kuishi mpaka mwaka mwingine utakapokuja. Kusema kweli tabia hii siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba, wafugaji tufuge kileo, tufuge kwa kuelewana na wenzetu wanatumia ardhi ileile. Tufuge na wenzetu anaofanya shughuli za kiuchumi, tuziheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru sana, sisi kama Wizara tutaendelea kutoa elimu kwa wafugaji ili waweze kuelewa kwamba jambo hili ni baya. Nitakwenda Mkoa wa Morogoro, nitatembelea mahali ambapo wafugaji wapo wengi tuelimishane, tuelezane ni namna gani tunaweza kushi na Watanzania wengine vizuri kuliko kuendeleza migogoro ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaki kwa maelezo sahihi, na atakuwa na bahati mbaya hana kipato,

mazao yake yatakuwa yameliwa hana kipato; na atakuwa hana warembo kwa sababu wameshahamia mji mwingine. *(Makofi/Kicheko)*

Kuna wageni leo jioni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni sita Mheshimiwa Condester Sichalwe ambao ni wapiga kura wake kutoka Momba Mkoani Songwe wakiongozwa na Afisa Kilimo Wilaya, Ndugu Oscar Mwilongo, karibuni. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambaye ni kada wa CCM kutoka Mkoani Arusha Ndugu Litwiku January, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza ni shukurani kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetuwezesha kufika siku ya leo. Pili ni kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonipa ya kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii ya Kilimo; na pia kuwashukuru wananchi wangu wa Dodoma Mjini kwa heshima kubwa waliyonipa kuwa Mbunge wao; na la tatu, ni kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Hussein Mohamed Bashe ambaye amekuwa kaka, rafiki, mwalimu, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Andrew Masawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ambalo nilikuwa nataka nizungumzie ni suala la *program* ya vijana kushiriki kwenye kilimo. Tunatambua kwamba vijana wetu wa nchini Tanzania si kwamba hawapendi kilimo lakini mazingira ya kuwafanya wafanye kilimo hayakuwa rafiki sana. Walikuwa na changamoto ya maeneo, mbiundombinu, pembejeo, masoko na mitaji. Tumekuja na *program* maalum ambayo inaitwa, jenga kesho bora ya vijana, ambayo lengo lake

kubwa ni kuhakikisha kwamba tunawapatia vijana maeneo, ambayo tutapima afya ya udongo. Pia tutawapatia pembejeo, tutawatafutia masoko na hatimaye lengo letu ni kuwa na kitu kinaitwa Kijiji cha Vijana cha Kilimo. Tunaamini kabisa hii itakuwa sehemu nzuri ya kuweza kuwavutia vijana wengi kufanya kilimo. Kwa kuanzia tutaanzia hapa Dodoma ndiyo itakuwa sehemu ya *pilot* zaidi ya ekari 20,000 zitatengwa kwa ajili ya *block farms* ambazo vijana wengi watahusishwa kushiriki katika kilimo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni la zabibu. Tumejipanga kuendelea kuhamasisha wakulima wa zabibu kulima kwa tija ili hatimaye zao hili liwaletee mafanikio. Mwezi ujao tutakamilisha uanzishwaji wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Zabibu ili wawe na sauti moja. Lakini vilevile tumekwenda mbali zaidi, tunakwenda kuanzisha viwanda vitatu vikubwa vya uchakataji na uhifadhi wa mchuzi wa zabibu ili wakulima wetu waache kuuza zabibu wauze mchuzi wa zabibu na uwaletee tija kwenye kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeongeza utafiti kwenye eneo hilo la zabibu na hivi sana ndugu zetu wa pale *TARI* Makutupora wametuongezea mbegu zingine. Tunataka wakulima wetu pia waanze kuuza zabibu za mezani; na hivi sasa tumeshagundua mbegu ya *ruby seedless* ambayo itakuwa ni zabibu za mezani. Lakini vile vile na zabibu za viungo *(raisins),* hizi zote zitafanyika katika kukuza zao letu hili zabibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeingia makubaliano na wenzetu wa *TBL* kwa ajili ya kilimo cha mkataba cha wakulima wa zabibu ili wapate uhakika wa masoko yao ya zabibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni masuala la mboga mboga na matunda. Tumeingia makubaliano na wenzetu wa

*TAHA* chini ya Dkt. Jacquline Mkindi ambaye ametenga muda wake mwingi kuikuza tasnia hii ya mboga mboga na matunda. Makubaliano hayo ambayo tumeingia yatakuwa ni katika mfumo mzima wa usafirishaji wa mazao ya mboga mboga na matunda *(cold chain management)* ambayo itasaidia katika kulinda ubora wa mazao yetu. Hapa pia tunakuja na kitu kinaitwa *green channel* ambacho kitasaidia katika kusafirisha matunda hayo pasipo kikwazo chochote mpaka kufikia katika *destination* yake, kwa maana ya *Airport* au Bandarini. Tunafanya haya kwa ajili ya kulinda ubora wa mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na vilevile ndugu zetu wa *TARI* tumekubaliana nao katika eneo lingine kubwa kabisa ambalo ni la kusaidiana kuanzisha miongozo maalum kwa ajili ya kuratibu zoezi la mazao ya mboga mboga na matunda ili tupate mwelekeo mmoja ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Pia tunakwenda kujenga *common use facility* tatu ambazo zitajengwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Iringa na Dar es Salaam. Lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa tuna *collection center* moja yakupokea parachichi au na matunda mengine kuya-*grade* na kuya-*sort* na mwisho wa siku ni kuhakikisha tunafikia lengo tulilojiwekea, la kwamba ifikapo mwaka 2030 tuwe tunauza mazao yetu ya matunda yenye thamani ya kufikia Dola bilioni mbili kutoka Dola milioni 750 ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la mkonge tunajua kuna changamoto kubwa, na mimi nilikwenda mwenyewe nimetembelea kule Korogwe. Changamoto kubwa ya mkonge ni kwamba wakulima wa mkonge wanashindwa kuvuna mara mbili mkonge wao na unaoza shambani kwa sababu ya ukosefu ya korona. Nilitangazie Bunge lako, tumeshamuelekeza Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge kuhakikisha anatangaza zabuni ya kununua korona tatu kwa ajili ya wakulima wa mkonge kule Korogwe. Korona hizi zitasaidia pia kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava

juu ya ubora, tunatambua ya kwamba hivi sasa daraja la ubora wa Mkonge wetu wakulima wengi wanapata ile inayoitwa UG; lakini lengo letu ni wakulima waende katika 3L na 3S, watoke kwenye UG. Ukipata *desiccator* ambayo ni ya kisasa na bora itamsaidia pia mkulima kupata mkonge ambao unakidhi matakwa ya soko na ambao mkonge wa 3L and 3S una soko kubwa na bei yake ni kubwa zaidi kuliko ile ya UG na ile nyingine ya UF. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine pia ambalo tunalifanyia kazi ni la kuhakikisha kwamba tuna-*diversify* matumizi ya mkonge wetu, badala ya kujielekeza tu katika kutengeneza nyuzi na magunia, tumekaa na wenzetu Chama cha *SAT* na tumekubaliana waongeze pia wigo mpana wa matumizi haya ili kutafuta soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkonge una uwezo wa kutengeneza *dashboard* za magari, *cabin* za ndege, milango na mkonge ukiuchakata vizuri una uwezo wa kutengeneza pombe kali ile aina ya *Tequila*. Kwa hiyo, tumezungumza nao kwa ajili ya *ku-diversify* kwenda katika eneo hilo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa maelekezo kama Wizara ya kwamba mazao yote ambayo yako chini ya Bodi zinazoshughulikia mazao, waanze kutumia magunia yatokanayo na mkonge. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunaongeza soko kwa ajili ya mkonge wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine katika mkonge hapa ambalo nataka niligusie kwa haraka haraka ni eneo la nyuzi za nailoni za kufungia magunia ya mkonge. Tumekubaliana na wenzetu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwamba sisi tumetoa maelekezo mazao yote ya kilimo, yatafungwa kwa kamba zitokanazo na mkonge na sio nailoni ili tuongeze soko la mkonge wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejipanga pia kuja na Sheria ya Kilimo na Sheria ya Ushirika tunataka tuwalinde wakulima wetu tulinde maeneo yetu, tupate maeneo ya kilimo ambayo pia tutayapima na tutaya-*gazette* ili mwisho wa siku tuondoe migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeboresha eneo la maabara yetu iliyopo Arusha ambayo inatusaidia kwa ajili ya mazao yanayokwenda nje ya nchi. Maabara yetu imetambulika, imepata ithibati na tumefunga mitambo ya kisasa. Hivi sasa mazao yanayotoka Tanzania yakitua pale Arusha hakuna mtu yeyote atayatilia mashaka. Kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya na *investment* kubwa ya mashine za kisasa na hivi sasa mazao yetu yanatoka pasipo changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kazi kubwa ambayo imefanyika na tunaamini Waheshimiwa Wabunge mtatuunga mkono kwenye safari hii. Safari hii ndio tunaianza, tunaomba twende pamoja, mtuunge mkono, tunajua matokeo yatakuja baadaye, lakini kazi ndio tumeianza, mtuunge mkono, tuko tayari kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania, kuifikisha Tanzania katika nchi ya ahadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana, Mwenyezi Mungu awabariki, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa majumuisho mazuri, sasa namwita mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge. Pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge, kwa kusimamia mjadala wa hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 ambao tunauhitimisha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii vile vile kushukuru mchango mkubwa uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Kwa dhati kabisa nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwani wametoa hoja nzuri sana, zenye malengo ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara yangu na kuharakisha mapinduzi ya kilimo. Hii inaonesha umuhimu wa kilimo katika usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, kwa kuchangia hoja hii na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza. Niwashukuru pia Katibu Mkuu, Bwana Andrew Massawe; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Profesa Siza Tumbo na Ndugu Gerald Mweli; pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa ushirikiano na ushauri wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuwasilisha maboresho katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha, 2022/2023. Aya ya 61 ukurasa wa 35 jedwali Na. 4 mchanganuo wa matumizi ya fedha zilizotolewa kwa Mafungu yote matatu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla kuu ni shilingi bilioni 151,863 badala ya shilingi bilioni 272,931. Aidha, matumizi ya shilingi bilioni 151,863 ni asilimia 51.63 ya fedha zilizoidhinishwa na sio asilimia 92 kama zilivyooneshwa katika jedwali. Aya ya 366, ukurasa wa 194 inaonesha kuwa katika kuongeza thamani kipato cha mkulima na kupunguza upotevu wa zao la zabibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kujibu hoja za Wabunge ambao wametoa mawazo yao. Hoja yetu imechangiwa na Wabunge 92 kwa kuchangia na vile vile imechangiwa kwa maandishi na Wabunge 10. Naomba nianze kuongelea eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge

wametoa maoni ya muda mrefu. Naomba nianze na Mheshimiwa mama Anne Kilango Malecela, kwanza nikiri mimi nikiwa Naibu Waziri wakati huo Waziri wangu Profesa Adolf Mkenda, alinituma na nimekwenda Jimboni kwake na nimefanya *survey,* nimetembelea wakulima wote wa tangawizi. Vilevile nimeitembelea *scheme* yake ambayo ilijengwa na Baba wa Taifa ya Ndungu na nikaenda mwenyewe kufika pale na kutatua changamoto zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie hana sababu ya kuondoka na shilingi ya kijana wake. Nataka nimhakikishie mbele ya Bunge lako na kuwahakikishia wakulima wa tangawizi sio wa Same tu, lakini vile vile wakulima wa tangawizi wa Buhigwe, Wizara ya Kilimo baada ya miaka 38 tumelichukua zao la tangawizi tumelikabidhi Taasisi yetu ya Utafiti ya *TARI* Mlingano kuanza kufanya utafiti na kufanya *multiplication* ya mbegu, ili maradhi yanayowakabili wakulima wa eneo lile wanaolima tangawizi tuweze kuliondoa tatizo hili kwa kudumu na mazao yote ya viungo. Kuanzia mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya utafiti wa tangawizi na mazao mengine ya viungo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, nataka tu nimhakikishie Mama Anne Kilango, wataalam wa Wizara ya Kilimo wako Wilaya ya Same, wanafanya kazi kubwa mbili. Ya kwanza, watafiti wa *TARI* wamekwenda kuchukua *sample* za udongo na mazao ya tangawizi kwa ajili ya kuyapeleka maabara, tuweze kutambua maradhi halisi yanayowakabili wale wakulima wa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, watu wetu wa Tume ya Umwagiliaji wanafanya kazi ya kufanya stadi kuitambua mifereji, kujua tufanye *design* ya namna gani kuweza kuweka mifumo ya umwagiliaji. Ndugu zetu wa Hai walituvumilia na

mwaka huu tumeshatatua tatizo lao tumewapelekea fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwombe mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango asiwe na hofu wakulima wa tangawizi wa Wilaya ya Same wanakwenda kutatuliwa tatizo lao. Watu wa Tume ya Umwagiliaji wako kule, wanafanya *design* ili tuweze kujua tunatumia *solution* gani kuweza kuvuna maji yale na kuwaondolea matatizo ya muda mrefu ya wao kujiunganishia mipira kienyeji kwa ajili ya kupeleka mashambani kwao. Kwa hiyo, Serikali inalifahamu tatizo, lakini vile vile tunalifanyia kazi hatujawaacha na hatutawatupa mkono. Mwaka kesho kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu aje aniulize ndani ya Bunge hapa na anisute mbele ya Wabunge hawa na Watanzania kwamba, Hussein uliniahidi unakwenda kushughulikia tatizo la wananchi wa Same la tangawizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalowakabili wakulima wa tangawizi kule Buhigwe, wanavuna hawana sehemu ya kuhifadhi, mwaka huu tumewawekea fedha tunakwenda kuwajengea maghala. Nataka niwaambie wakulima wa tangawizi, Serikali inachukulia mazao yote ya viungo kwa u-*serious* mkubwa na hatutoyapa nafasi ndogo kama ambavyo miaka 30 iliyopita ilichukuliwa kwa *style* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge wapo waliochangia na kusema kwamba, bajeti ya Wizara ya Kilimo ni ndogo haitoshi, ni kweli lakini kuna hatua ambayo tumepiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na bajeti kwa zaidi ya miaka sita isiyozidi Shilingi bilioni 200, leo tunatenga bajeti ya Shilingi bilioni 751, asilimia 88 ya bajeti hii, inakwenda kwenye maendeleo, haiendi kwenye vikao, haiendi kwenye matumizi ya ofisi. Nataka tu nitaje maeneo ambayo tunapeleka. La kwanza tunapeleka kwenye suala la mbegu. Nataka niseme

mbele ya Mungu na mbele ya Bunge hili, kama kweli nchi hii tunataka kuondoka kwenye matatizo, kwenye sekta ya kilimo, tusifanye maamuzi ya sekta ya kilimo kisiasa. Kilimo ni biashara, kilimo ni sayansi, kilimo ni teknolojia na kilimo kina *basics*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwape hizi takwimu na ni vizuri kwa kuwa sisi ndio wawakilishi wa wananchi tufahamu. Nimechukua mazao 13 na ili *food security* ya nchi hii iweze kupatikana, tuna mazao mawili makubwa, mahindi na mpunga ndio mazao tunayokula Watanzania wengi. Swali la kujiuliza sisi, toka tumepata uhuru kati yetu tumewahi kukaa kujiuliza swali, tunahitaji mbegu bora tani ngapi ili tumpelekee huyu mkulima mdogo maskini kwa msaada wa Serikali ili aweze kwenda shambani? Nataka niwape hizi takwimu tunahitaji tani 652,000 kwa mwaka ili tuwagawie wakulima, sasa tujiulize swali tunazalisha tani ngapi? Tunazalisha tani 15,000 sisi na sekta binafsi, halafu tunaamini kwamba *we are safe*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mahitaji ya tani 652,000 uwezo wetu wa sekta binafsi na Serikali tunazalisha tani 15,000, ndicho tunachozalisha. Sisi kama Wizara na nawaomba mtuunge mkono. Tumekwenda kuongea na Mheshimiwa Rais, tumemwambia mama, cha kwanza kwenye sekta ya kilimo ni tija. Tija haiji kwa jina la Roho Mtakatifu wala haiji kwa kumwomba Mwenyezi Mungu kwa kupitia Mtume Muhammad, ina *equation*. *Equation* ya kwanza ni *input* na *input* namba moja ni mbegu, ni lazima kama nchi tujitosheleze kwa mbegu na tuwe na uwezo wa kuzalisha mbegu zetu. Sisi kama Wizara ndio tumekipa kipaumbele namba moja. Tunafanya nini? Bajeti ya utafiti imeongezwa kutoka shilingi bilioni 5.0 kwenda shilingi bilioni 43. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya uzalishaji wa mbegu tumeongeza kutoka shilingi bilioni 5.0 ya mwaka 2020 kwenda

Shilingi bilioni 40.7. Zinakwenda kufanya nini? Cha kwanza, tunakwenda kufanya kazi kubwa moja; kwanza kwenda kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu. Haiwezekani mkulima anakwenda shambani na sisi Serikali ndio tunakwenda kuzalisha kwa kudra ya Mungu. Tunawaomba mtuunge mkono ili tupate tani 600,000 tunahitaji kuzalisha *pre-basic seed.* Kwanza tunatakiwa kufanya *breeding* tufanye *pre-basic seed* tuzalishe *basic seeds* halafu tuwape sekta binafsi na Serikali kwa ajili ya *multiplication* tuweze kuzipeleka kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni safari, tunaomba watuunge mkono Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kufungua mashamba ya Serikali. Nitumie Bunge lako Tukufu niiombe sekta binafsi ya Watanzania, waje Wizara ya Kilimo, tutawapa ardhi kwa mikataba ya muda mrefu, tutawagawia wazalishe mbegu, tutanunua kama Serikali na tutawagawia wakulima kwa ruzuku**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ambayo tumejiamulia kama nchi ni lazima tuwekeze kwenye umwagiliaji. Nataka nimkwambie hiki kipindi mimi ni Muislam, sio *hamsa swalawat* lakini naswali swali. Mvua zilivyokuwa zinachelewa, wewe tunaswali wote Gaddafi, kila Ijumaa Imamu anatuongoza kuomba dua na kufanya *kunuti* Msikitini Mungu alete mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya yote, Mwenyezi Mungu katupa akili, Mwenyezi Mungu katupa nafasi, Mwenyezi Mungu katupa ikolojia nzuri, ni suala la kuamua tunawekeza fedha zetu wapi? Tumekwenda kwa Mheshimiwa Rais, tukamwambia mama, naomba tuongezee bajeti ya umwagiliaji. Mheshimiwa Rais tumepata fedha tumeongeza bajeti ya umwagiliaji kutoka Shilingi bilioni 46 kwenda shilingi bilioni 361. Hata hivyo, tumesema nini? Tumeamua na nawaambieni kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutayafanya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niliombe Bunge hili hata kama Bashe hayuko Wizara ya Kilimo Mungu kamchukua, au kwa jambo lolote, Bunge hili lisimamie *vision* hii ya *irrigation* kwenye nchi. Cha kwanza, tulichoamua kwenye umwagiliaji tumesema hivi lazima tufanye *comprehensive feasibility study and design* kwa mabonde yote ambayo ni ya uhakika na tuanze kujenga mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua kufanya nini? Tunakwenda kufanya *feasibility study* na *design* ya Bonde lote la Rufiji, hekta 64,000 tumeweka Shilingi milioni 835. Tumeamua kwenda kuweka *feasibility study* bonde lote la Mto Manonga na Wembele hekta 57,000. Tumeamua kuchukua bonde lote la Kilombero hekta 53,000. Tumeamua kuchukua eneo lote la Usangule, Malinyi hekta 2,500 na tumeamua kuchukua Mkoa wa Ruvuma Bonde la Mto Ruvuma hekta 26,000. Katika hili nimewaambia wenzangu Wizarani mambo ya *joint effort* na *neighbour's country,* tukikutana nao kwenda pamoja hewala, hawapo sisi tunaanza safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa tunakutana mikutano ya pamoja ya *joint effort,* vikao vya kuitwa Waziri tunakwenda, safari hii nimealikwa kwenye Ruvuma *Basin* sijakwenda kwa sababu *I don't see a reason, we can do our own design,* tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya hekta 306,000 zinazohusu eneo la Ziwa Victoria kuanzia Mara mpaka Kagera; eneo la *Lake* Tanganyika; na eneo la *Lake* Rukwa, tunakwenda kufanya *design* mwaka huu na tunalifanyia *design* lote, tutaanza kujenga kuanzia mwaka ujao wa fedha. Tumeamua kujenga mabwawa na nataka kusema ndani ya Bunge hili na iingie *on record,* nadhani katika Mawaziri ambao, wamekwenda kukaa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha mara nyingi, mimi ni mmojawao

na namshukuru sana yuko hapa, anaelewa, *ana-sympathize* na anaunga mkono juhudi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunaweka *effort* kwenye *irrigation?* Nimewaambia watu wa Tume ya Umwagiliaji, ni hivi, haiwezekani tunajenga mradi tuna shilingi bilioni 2.0 unampelekea Hussein shilingi milioni 100, John shilingi milioni 2.0 nani shilingi milioni 3.0, mwisho wa siku mmegawana umasikini na hakuna kilichokamilika. Tukijenga scheme ya umwagiliaji tunajenga *total package* kuanzia *water catchment* na mifereji, ni heri tujenge *scheme* mbili kuliko kukaa tunagawana umaskini mdogo mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *priority* yetu ya kwanza tunafanya *feasibility study* na kufanya *design* ya maeneo yote ambayo ni *potential* katika nchi, ili tunaposema kwamba mwaka kesho tunajenga nini tunajua tunakwenda kujenga sehemu ambayo hata nchi isipopata mvua mwaka mzima tunayo *food basket* ambayo inaweza kutulisha na kutuweka salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi tunazopeleka asilimia 90 zinakwenda kwenye *development za irrigation,* hakuna fedha inayokwenda kwenye matumizi ya kawaida. Mbali na hapo *scheme* nyingi zinajengwa katika nchi yetu, baada ya miaka miwili zimekufa. Nataka niwape mfano, Sheria ya Umwagiliaji inatutaka tukusanye *Irrigation Development Fund, five percent* katika kila *scheme* ambayo Serikali imewekeza. Niwape mfano Serikali imewekeza 21 *billion shillings* kwenye *scheme* ya Dakawa yenye hekta 2,000, *turn over* ambayo tunatakiwa tukusanye iingie kwenye *Irrigation Development Fund* ni 600,000,000 *million shillings*. Tumeamua ku-*unlock* hili tatizo kwa kufanya nini? Tunafungua Ofisi za Umwagiliaji kila Wilaya na kila *scheme* itakuwa na Meneja wa Skimu, ili tuweze kuzisimamia na wakulima wasimamiwe, wazalishe mara mbili kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapeleka *manpower,* tunapeleka vitendea kazi, tunanunua magari kwa ajili ya *Irrigation Development* iweze kufanyika katika nchi hii. Tunakwenda kufanya Luiche imekuwepo kwa muda mrefu lazima tufanye hivi vitu. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, *always* na naomba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, Bunge hili lii-*guide* Serikali kwenye kilimo kwa kuhakikisha tunawekeza kwenye mambo ya msingi. Moja ni *seed multiplication,* kama hatuna mbegu zetu, kama hatuna umwagiliaji, kama hatua uwezo wa kum-*subsidizing* mkulima kwenye *input,* hatuko salama. Huu ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee *issue* ya mbolea, nitumie Bunge lako hili Tukufu, *it is very danger* kwenye *capacity* zetu tunaposimama mbele ya Bunge Tukufu na sisi ndiyo tunaowakilisha wananchi, tunapata *air time and then we send a negative message and misleading information*. *Trend* ya bei ya *fertilizer* duniani na mimi nimeamua niongee hapa. Kuna hoja inasemwa kwa nini Rwanda, kwa nini Malawi, kwa nini Zambia bei ya mbolea iko chini? Nataka niwapeni *statistics* za bajeti ya Rwanda mwaka huu. Rwanda *for the last ten years* amekuwa aki-*subsidize input* yake, hasa mbolea kwa *support* ya *World Bank, WFP, FAO* na wengine. Mwaka huu wa fedha Rwanda inatumia Dola Milioni 15 kutoa ruzuku ya mbolea. Ni sawasawa na asilimia 11.7 ya bajeti nzima ya kilimo ya Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Malawi anatumia Dola Milioni 131 ku-*subsidize* mbolea. Ni sawasawa na asilimia 44 ya bajeti nzima ya Malawi. Zambia ana-*subsidize* mbolea *by 30 percent*. Tena Zambia *package* yake ya *subsidy* ni mbolea na mbegu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tanzania?

**WAZIRI WA KILIMO:** Tumeanza kuchukua hatua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatumia Bilioni 150 kuanzia Tarehe Mosi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe kidogo subiri. Waheshimiwa Wabunge hapa tunazungumza vitu *very serious* na kurukiarukia maneno ni nje ya utaratibu wa Kibunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme haya mambo kwa uwazi na *with respect* nijibu hoja *categorically* ya Mheshimiwa Mpina. *He has been a Minister* katika Serikali, *it is very danger* kwenye *capacity* ya mtu ambaye ni Mbunge wa muda mrefu, amekuwa Naibu Waziri, amekuwa Waziri, kusimama Bungeni ku-*present issue* ambayo *totally he is misleading the public. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mbolea duniani siyo jambo la kuficha ni jambo liko kwenye *public domain, it is a commodity like any other commodity.* Hata uki-*google* unazipata taarifa za bei ya mbolea duniani. Nimechukua *source* yangu hiyo ni taarifa ya *World Bank, a reputable organization.* Bei ya mbolea Machi, 2018 *DAP* ilikuwa Dola 549, *FOB rate an average price, today* ni Dola 948. Urea Dola 134 leo ni Dola 723.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili siyo jambo la siri, liko wazi halifichwi. Nipitie mbele ya Bunge lako nimuombe Mheshimiwa Mpina kama anayo *source* yoyote ya kunipatia mbolea ya bei rahisi aje nampa mkataba wa tani Laki Nne zote aniletee. Duniani kote wana-*subsidize* na mimi nataka niwaambie tusipotoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa nchi hii tutakuwa tunawaonea, tunawaumiza na hatuwatendei haki na hatulitakii Taifa letu uhai. Tusifanye siasa kwenye mambo hatari. Hii siasa ndiyo imeua kitalu cha mbegu ya pamba katika Jimbo lake. Ninawaomba, mimi ni *very open* na *I am ready to bear any cost, this is what I*

*believe,* lazima tutoe ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaishia hapo kwenye ku-*design* ruzuku, tumeamua kufufua Kampuni yetu ya *TFC. No where in the world,* hii dhana ya kwamba, Serikali *can not trade* ni dhana iliyopitwa na wakati. Serikali ita-*trade* kwa sababu mbili, moja ku-*make profit when it is necessary,* lakini mbili ku-*subsidize* na ku-*stabilize* ndiyo maana tunanunua na kuuza. Sasa tumeamua kuifufua *TFC* tumeipa mtaji wa Bilioni Sita na tutaipa *guarantee* iende ikanunue mbolea kwenye soko la dunia ije hapa iweze kushindana na *private companies.* Kama tuta-*subsidize* lazima tuwe na mkono wetu ndiyo maana kwenye hotuba nimesema *subsidy mechanism* ya Wizara ya Kilimo safari hii tutawapa *priority* wazalishaji wa ndani *and we will do this. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku zote hofu watu wataiba, halafu kuna dhana moja hatari sana, kuwaita wafanyabiashara wezi. Kwani hakuna *Civil Servants* wezi nchi hii? *Big scandals* zilizofanywa humu ndani hazijahusisha *Civil Servants? Why we call our private sector everyday* wezi kwenye nchi hii? Mtu wa sekta binafsi haibi peke yake lazima awe na mtu wa Serikali waibe nae. Kwa hiyo, mimi nataka niiambie *private sector* iliyoko kwenye kilimo, *I will protect you* kama ninavyom-*protect* mkulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majadiliano hapa yamesemwa kuhusu ushirika, nataka niwaambie na nimwambie Ndugu yangu Mheshimiwa Sanga, mazao yote yanayopitia mfumo wa ushirika hayana lumbesa. Ili kumlinda mkulima, wakulima hawa wadogowadogo ni lazima tuujenge ushirika. Wanaushirika wapo wanaoiba lakini hatutaufuta ushirika kwa sababu kuna wezi, tutashughulika na wezi wakati tunaendelea kuujenga ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo *success stories* za ushirika, zipo. Ushirika ulikufa *because the country decided* kwenda kwenye *role approach* ya *privatization,* ndiyo ukweli huo na mimi hiyo ndiyo naamini. Leo tumefufua *ginneries,* tunafanya Chato, *they are making profit,* tunayo Mbogwe ya Mheshimiwa Maganga mwaka huu imepata *profit* na tumeifufua mwaka jana. Nikuhakikishie tunawapa *13 Bilioni* ya kwenda kununua pamba. Tumefufua *CACU,* tunaenda kufufua *SHIRECU* Sola, tunaenda kufufua Nyanza, tunaenda kufufua Manawa, tunaenda kufufua Sola, tunaenda kufufua Lugulu, tunaenda kufufua *ginnery* ya Sengerema kwa Mheshimiwa Tabasamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hivi, tutazifufua. Tuliziua kwa sababu tuliogopa kukabiliana na changamoto, tutakabiliana nazo, tutazifufua *without any problem* na huo ndiyo mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Tanzania *Agricultural Development Bank.* Kisera *TADB is a development bank* siyo *commercial bank.* Kazi ya *TADB* ni ku-*de-risk* sekta ya kilimo na ku-*invest* kwenye miradi ya muda mrefu, ndiyo kazi yao. Bahati mbaya kwa sababu ya sera zetu na mifumo yetu ya ukopeshaji ambayo tunayo katika uchumi wetu, ambayo tume-*copy* na ku-*paste* huko kwingine tumeileta hapa ambayo hai-*acknowledge rural economies* ndiyo maana tunampeleka *TADB* kwenda kumkopesha mkulima ili akapande nyanya auze kesho, badala ya kumpeleka kwenye *development projects. TADB* anafanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekusikia Dada yangu Mheshimiwa Jacqueline, nimewasikia Wabunge wote wanaotaka wamuone *TADB* karibu, tutakaa na *commercial banks* zote ambazo zimesaini makubaliano na Tanzania *Agricultural Development Bank* ziwe na madirisha ya *TADB* kwa ajili ya kutoa *guarantees* kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, benki zote ambazo zina asili ya Kitanzania zimeanza kuelewa sekta ya kilimo, zipo benki *NMB, CRDB* na mimi wala sioni aibu kuzitaja, *TADB, Equity,* benki hizi zimeanza kutoa fedha kwa ajili ya kilimo, zimeanza, Wizara tutazisaidia na kuzi-*support*. Benki yoyote, nilisema mbele ya Rais, nasema mbele ya Bunge, benki yoyote ambayo haitakwenda kutoa mikopo ya kilimo kwa *single digit* kama tulivyokubaliana haitafanya biashara na Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misimu inakuja, unakuja msimu wa korosho wa *turn over* ya zaidi ya Bilioni 500, wanunuzi wote tutawapeleka kwenye benki zinazofanya biashara na sekta ya kilimo. Unakuja msimu wa pamba, unakuja msimu wa kahawa, unakuja msimu wa chai, unakuja msimu wa kakao, nataka niziambie *commercial banks, they must play our music*. Kwa muda mrefu *turn over* zao zinabebwa na kilimo, lakini kinachoenda kwenye kilimo hakionekani, tutafanya nao biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu kuwaambia *commercial banks* pelekeni fedha kwenye ushirika wa korosho. Wakopesheni *AMCOS,* tumeshakubaliana mimi na ninyi na mmetaka barua kwangu nimewaandikia, sasa ambae hatopeleka tutakaa naye mezani. Ninasema *categorically* tunaenda kwenye msimu atakaye-*enjoy* fedha ya msimu wa korosho ni yule aliyeenda kwenye korosho kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja hapa kwamba, kwanini tunaanzisha Benki ya Ushirika, nashauri tuende tukasome mifumo ya ukopeshaji na ya uendeshaji wa *Cooperative Society* na *Cooperative Society Financing Modals.* Vyama vya Ushirika haviwezi kukopesheka katika mifumo hii ya *commercial approach* tuliyonayo kwenye mabenki, ndiyo maana duniani kote watu walioendelea wanazo benki za *cooperatives.* Niwahakikishie benki ya

ushirika haitaenda kuchukua hela ya umma. Tumefanya *modal* Benki ya Kilimanjaro. Tumeingia benki wameweka mkono wao, wameweka *management,* tumeanza kupata faida. Tunai-*reform* Benki ya Tandahimba, tunazi-*merge* benki hizi mbili tuna-*form Cooperative Bank. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na *negotiating tool.* Lazima taasisi za fedha zijue kwamba wakulima wa nchi hii wana benki yao wasiposikilizwa *there is somewhere they can go. TADB* ni mali ya Serikali, tuiache *TADB* ifanye kazi yake ya msingi ya ku-*invest* kwenye *long term project,* tuziache *commercial banks* na *cooperative bank* zitaenda kwenye *short term,* hii *cooperative bank* tunashirikiana na *commercial bank* kuianzisha. Kama zilikufa benki nyingine, zilikufa *because* tuliamua kuziua kwa kufanya *political decisions* kwenye mifumo ya ukopeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kuanzisha *insurance* ya wakulima, inakuwa *total package.* Tumeanza kazi na *TIRA* na inakuwaje, kwenye *production,* kwenye *storage* na kwenye *market,* mkulima anapata *risk* kote, tumeamua. Kwa nini tunaenda kwenye eneo hili? Tunaenda ili kumlinda mkulima na siku ya mwisho aweze kukopesheka kirahisi. Tunashirikiana na Wizara ya Fedha, tunashirikiana na *TIRA* na tutaanzisha na ku-*launch scheme* ya *insurance* ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mafuta ya kula. Siku zote toka nimeingia Bungeni tumekuwa tukijisifia mchikichi ulianzia Tanzania, nataka niseme hivi kama tutaendelea na *modal* tunayoendelea nayo sasa hivi ya mchikichi tusahau kuwa na utoshelevu wa mafuta, tusahau! Hauwezi kuzalisha miche, unai-*breed* halafu unampelekea Hussein anaenda kupanda kwenye robo eka. Ninamuomba Mbunge wa Kalenga usiwagawie wakulima eka moja-moja kilimo siyo kugawana umasikini, *that is wrong approach. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachukua hatua gani kwenye mchikichi? Hatua ya kwanza tunayoichukua kama Serikali, tumejiwekea lengo la kuzalisha *metric tons* Laki Tano ya mafuta ya mchikichi. *The first approach* tunayotaka tunahitaji hekta 154,000. Nimemuandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Pwani, nimemuandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Tabora, nimemuandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, nimemuandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Katavi, tunaenda kuchukua maeneo makubwa kama yatahitaji fidia Serikali italipa fidia. Tunaenda ku-*clean,* kuyasafisha, tunagawa *blocks* kubwa kubwa na kuwagawia wakulima tumewakabidhi eneo, kama ni eka 20 unampa eka 20, umempandia, mnasimama. *Then automatically* kitakachotokea *processors* ndiyo watakuja pale wataanza ku-*process. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii wanayofanya Kaka yangu Mheshimiwa Kirumbe kule Kigoma ni kutengeneza michikichi nusu eka, wanaichemsha kwenye pipa na mti, haiwezi kutuondoa, ndiyo ukweli. Tumeamua kuchukua *modal* ya ku-*subsidize* kwenye alizeti na ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kuanzisha *Tanzania Agricultural Growth Corridors,* lazima tufanye hivi. Wazee wetu hawa akina Mheshimiwa Mkuchika na wenzake hawakuwa wajinga kutoa muongozo wa *TANU* wa maeneo ya kilimo. Leo unalima korosho kutoka kule kwa kina Mheshimiwa Katani unaipeleka mpaka Ngara. *Economically does not pay, logically it has no sound. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie inawezekana ikawa *unpopular decision,* lakini lazima tuwe na *growth corridors* za kilimo katika nchi hii, lazima na ndiyo mwelekeo tunaoenda nao kama Wizara. Ninaliomba hili Bunge yeyote atakayekuja Wizara ya Kilimo mumhoji juu ya *Agricultural Growth Corridor,* lazima! tusipofanya hivi hatuitendei haki hii nchi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunagawa mbegu za alizeti, tuna-*subsidize, it is a painful decision* na Serikali itaweka Bilioni 11. Nitumie Bunge hili kuwambia Mkurugenzi wa *ASA,* Dada yangu Sofia mmoja wa *Civil Servant* wanaofanya kazi nzuri sana katika nchi hii, tulivyoamua kugawa tani 2,000 hakulala yule Dada. Ninawaomba Wakurugenzi wa Halmashauri, *targets* za kukusanya mapato mtazipata kwenye kilimo, m-*support* kilimo, tutazalisha, tutagawa tani 5,000 msimu unaokuja kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na tutagawa *certified seeds,* msimu uliopita tuligawa *standard seeds,* safari hii tunaenda kugawa *certified seeds* kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipogawa mbegu na kuwapa ruzuku wakulima wa nchi hii, Marekani anatoa ruzuku, *European Union* wanatoa ruzuku, sisi ni akina nani kudhani kwamba eti mkulima atajinunulia kila kitu? *We should not be misled. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea sana kuhusu suala la mbegu na ninataka niseme kwamba mwelekeo wa Serikali ni kufanya *research and development,* kuzalisha mbegu bora za kisasa, tuwe na mbegu zetu ambazo tunazalisha wenyewe. Tukijizalishia wenyewe hizi mbegu bora *whether* ni *hybrid* au ni *OPV* na kwa kuwa tunataka *growth rate* ya *10 percent by 2030* haya tunayoyaanza leo matokeo yake siyo ya kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watu waliwekeza huko nyuma, leo tuna-*enjoy* sisi. *Let us sacrifice now.* Tujitoe, tuwekeze kwenye uzalishaji wa mbegu, tujitosheleze. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mazao 13 ambayo ni mahindi, mpunga, mtama, alizeti, soya, ufuta na maharage; mazao haya tukiwekeza kwa muda mrefu kwa kipindi cha miaka mitatu tu kwenye eneo la mbegu nchi hii itajitosheleza. Tutakuwa na mbegu zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuiambia sekta binafsi ya Tanzania, iache tabia ya kuwa *traders,* wawe *investors.* Njooni tutawapa maeneo, tutawapa mikataba ya muda mrefu mzalishe mbegu, tutazinunua sisi, tutawapa wakulima wa nchi hii kwa ruzuku. *This is the best model,* kote duniani wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameniambia ndugu yangu Mheshimiwa Katani kwamba nawapendelea watu wa tumbaku kwa sababu natoka Tabora kwenye tumbaku. Kwanza sikani, natoka Tabora. Pili,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme hivi, wakulima wanasajiliwa wote wala msiwe na hofu. Kupitia Bunge lako nimwambie Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho, usipoanza kusajili wakulima, kuanzia mwaka huu tunaanza kugawa pembejeo, mimi na wewe hatutaelewana. Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba ni lazima usajili wakulima. Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa ni lazima usajili wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Katani anasema tumewapendelea watu wa tumbaku; niseme, kwa mwaka huu mmoja…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe toa hoja. Ahsante kwa michango mizuri na majibu mazuri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie. Karatasi ya hela imepotea nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Tukae.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management*...........Sh. 6,539,591,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, nilishapewa majina ya wahusika kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri. Tunaanza na Mheshimiwa Esther Maleko, dakika tano.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuzingatia uzito wa zao la kahawa kwamba zao hili ni la kimkakati, lakini zao hili linaingizia nchi hii fedha za kigeni. Pamoja na hayo zao hili linalimwa takribani mikoa 15 nchini Tanzania, ni sawa na nusu ya Tanzania; lakini tunaona kwenye korosho wanapewa ruzuku ya mbolea; kwenye alizeti wanapewa ruzuku ya mbegu, lakini cha kusikitisha kwenye kahawa hakuna ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate *commitment* ya Serikali juu ya suala hili, vinginevyo nitaendelea kushikilia Shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimwombe dada yangu Mheshimiwa Esther, hana sababu ya kushika shilingi katika eneo hili. Kwanza kahawa tunawapa ruzuku ya miche, na mwaka huu tutawapa ruzuku ya miche milioni 20 ambayo tutawagawia wakulima wa kahawa. Ruzuku nyingine ambayo anaiona kama ilivyo kwenye korosho, kwenye pamba, ndiyo maana tumeleta *package* ya kuomba kutoa *subsidy* kwenye mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa kahawa wanaotumia mbolea, tutakapoanza kutoa ruzuku hii kwenye mbolea zote, maana yake wakulima hawa na wenyewe watapata ruzuku hiyo na wala watakuwa hawana sababu ya kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili tunayoifanya kwenye eneo la kahawa, sasa hivi Bodi yetu ya Kahawa tumeipa jukumu la kufanya *comprehensive study* ya kujua mahitaji halisi kwa *product* yao ni yapi? Je, ni mbolea peke yake? Je, wanahitaji aina gani ya gunia? Wanahitaji aina gani ya vifungashio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu katika *package* ya ruzuku ya kusaidia ujenzi wa maghala, zao la kahawa kupitia vyama vyao vya ushirika ni maeneo ambayo tutaenda ku-*rehabilitate* maghala yao. Hiyo ni *support* ya Serikali na ni *subsidy* ya Serikali ambayo siku ya mwisho hawairudishi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa hiyo, naomba aiachie tu Shilingi yetu ili twende kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini sijaridhika na ninaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kama nilivyoeleza mwanzo, zao la kahawa ni muhimu sana katika uchumi wa Tanzania lakini limepewa nafasi ya kuwa ni zao la kimkakati. Pia tunaona mazao yote ya kimkakati kama korosho, tumbaku, pamba zinapewa ruzuku, lakini bado kwenye suala la kahawa kunasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate *commitment* ya Serikali, ruzuku zote zinazotolewa kwenye korosho, kwenye tumbaku na kwenye pamba zitolewe vivyo hivyo kwenye kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba kahawa inapata ruzuku, na inapata ruzuku kwenye miche. Mwaka huu kwenye *plan* ya Wizara tunapozungumzia ruzuku ya

mbolea watapata wakulima wote; na wakulima wa kahawa ni sehemu ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatuna sababu ya kuwa na *a specific* kwenye haya mazao ya pamba. Ruzuku yao ya *input* siyo ya mbolea ya kupandia wala ya kukuzia. Ruzuku yao ya *input* ni vifungashio na viuatilifu. Ukienda kwenye korosho, ruzuku yao wenyewe hawaweki *DAP*, hawaweki *UREA;* wenyewe wanaweka *sulphur.* Wana aina fulani ya pembejeo wanazotumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mbele ya Bunge lako kwamba yapo maeneo yanayotumia viuatilifu, ndiyo maana tumemwagiza Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa afanye *a comprehensive study* kuwa na *specific needs* za zao la kahawa ambazo Serikali itaenda kuweka mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba siyo kwamba zao la kahawa tumeliacha. Nataka niseme mbele ya Bunge lako Tukufu kahawa inaenda kupata ruzuku ya maghala katika Mkoa wa Kagera. Maghala yao yote ya ushirika yaliyokufa ambayo ni zaidi ya 300 tunaenda kuyafufua kama Serikali. Hii ni ruzuku ya Serikali kwa ajili ya kulisaidia zao hili *specific*. Tunapeleka kwenye korosho maghala ya *subsidy* kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba tupeni nafasi, tutaendelea kufanya tathmini, aina gani ya *intervention* inatakiwa kwenye zao husika na Serikali itaweka mkono na Mheshimiwa Rais ameonyesha *political will* ya ku-*support* sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge, hamna sababu ya kuendelea kuishika hii Shilingi, tuendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Esther Malleko. Kama ulivyoona, pamoja na kazi nzuri ambayo Waziri ameifanya na amesema mambo mengi, lakini hata wakati wa ku-*wind-up* hajazungumza chochote kuhusu zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachozungumza sisi ni kwamba, ni kweli Bodi ya Kahawa wanatoa ruzuku ya mbegu, lakini uwezo wao ni mdogo sana. Kwa mfano, mwaka ambao tunao sasa tunakaribia kuumaliza June 30, katika Halmashauri nzima ya Lushoto tumepata miche 68,000 peke yake wakati mahitaji yetu yalikuwa zaidi ya miche 1,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua pia kwamba wapo wazalishaji binafsi ambao wanapenda sana kufanya kazi pamoja na Bodi ya Kahawa, bado Bodi haijapewa uwezo wa kifedha wa kuweza kusaidia kupata miche ili tuweze kupata miche bora na tuondoe ile miche ya zamani. Kwa hiyo, *commitment* ambayo tunaitaka sasa hapa ni kuona kwamba angalau kwa mwakani Serikali inaahidi kutoa miche mingapi ili kuongeza uzalishaji katika zao hili la korosho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Samahani, katika zao la kahawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na niombe Bunge lako Tukufu kwa kutambua hoja za msingi kabisa Waheshimiwa Wabunge walizosema, nimemsikia Mheshimiwa Esther pamoja na

Mheshimiwa Shangazi, na kwa kweli ndiyo maana wapigakura wao waliwaleta hapa. Hoja zao ni za msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kuwaambia ni kipi? Moja, tumeongeza bajeti ya kwenye hizi *inputs.* Awali zilikuwa tu *around five billion,* sasa hivi tumepeleka mpaka 40. Ni ongezeko kubwa sana kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hicho tu, Mheshimiwa Waziri amekuja na mpango ambao ni *comprehensive*. Tulikotoka tulikuwa tunagusa tu kimoja kimoja hivi; sasa hivi maadamu amekuja na mpango ambao uko *comprehensive* na hii siyo bajeti ya mwisho, ndiyo kwanza tunaendelea, nawaomba Waheshimiwa Wabunge mridhie, Serikali tumepokea hili. Kwa kweli kama alivyosema, tumekaa vikao vingi sana mpaka tumefika hapa. Mheshimiwa Rais ametupa rungu la kuendelea kuitengeneza hii mipango na nia yake ni kuona mazao yote yanafanya vizuri. Sisi kama watu wa Wizara ya Fedha mazao haya yakifanya vizuri, yanatusaidia kwenye *export earnings.* Ni jambo kubwa mno na ni jambo ambalo linaisaidia nchi kwenye *ranking* za pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, hatupingani na maoni ya Wabunge ya mazao yote haya ya kuweza kupata hizo ruzuku isipokuwa watoe fursa waachie Shilingi ya Mheshimiwa Waziri, anapomaliza tu hapa, tunaendelea tena na vikao vingine vya kuendelea kuboresha sekta ya kilimo kwenye haya mazao mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Malleko funga hoja yako.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa maelezo hayo, ninarudisha Shilingi ya Waziri na nimwombe 2023 ni keshokutwa, tutakutana tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu umekwenda, tunaenda kwenye *guillotine.*

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management*............Sh. 6,539,591,000
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*..........Sh. 1,992,871,000
Kifungu 1003 – *Policy & Planning Unit*................Sh. 3,417,435,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*....Sh. 29,954,566,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 529,912,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*.................................................Sh. 739,071,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.............................................Sh. 469,354,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*........................Sh. 665,909,000
Kifungu 1009 – *Management Inform. System*......Sh. 748,546,000
Kifungu 1010 – *Environmental Management Unit*..................................................Sh. 438,289,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*.................Sh. 38,012,025,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*......Sh. 2,334,484,000
Kifungu 2003 – *Agricultural Land Use Planning & Management*..........Sh. 1,133,528,000
Kifungu 2004 – *Plant Breeders Unit*........................Sh. 261,683,000
Kifungu 5001 – *National Food* Security............Sh. 12,418,283,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 5 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...............................Sh.1,021,781,830
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*.............Sh. 356,883,030

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*....................................Sh.1,650,093,931
Kifungu 1004 – *Government Communication*....Sh. 106,460,431
Kifungu 1005 – *Procurement Management*........Sh. 257,940,831
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 176,728,933
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*................................................ Sh. 114,230,230
Kifungu 1008 - *Legal Services* Unit.........................Sh. 111,133,531
Kifungu 1009 – *Enveronment and Social Management*................................Sh. 101,628,531
Kifungu 2001 - *Design & Research* Division.....Sh. 50,634,382,831
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*............................Sh. 11,554,461,830
Kifungu 2004 – *Operations Division*.......................Sh. 551,997,831
Kifungu 2005 – *Compliance & Quality Assurance*......................................Sh. 136,405,230

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 1001 – *Admininistration Human Resources Management*..............................Sh. 1,832,457,160
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*.............Sh. 247,757,840
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*.....................................Sh. 385,853,000
Kifungu 1004 – *Government Communication*....Sh. 226,508,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*........................Sh. 173,670,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management*..........Sh. 91,856,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology*...................................Sh. 737,092,000
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 183,140,000
Kifungu 1009 – *Research & Training* Unit.............Sh. 218,856,000
Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion & Coordination Section*....................Sh. 279,336,000

Kifungu 4002 – *Cooperative Microfinance Section*..........................................Sh. 229,716,000
Kifungu 4003 – *Regional Cooperative Offices*......................................Sh. 5,506,635,000
Kifungu 4004 – *Cooperative Marketing & Investment*....................................Sh. 135,202,620
Kifungu 4005 – *Registration Services*.....................Sh. 219,144,000
Kifungu 4006 – *Inspection & Supervision*...........Sh. 4,226,043,380

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 5 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*..................................Sh. 3,917,000,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*..........................Sh. 84,820,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology*.................................Sh. 1,718,530,880
Kifungu 1009 – *Environmental & Social Management Unit*......................Sh. 1,238,120,000
Kifungu 2001 – *Design & Research Management*..........................Sh. 36,203,310,294
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*..........................Sh.133,574,176,826
Kifungu 2004 – *Operations Division*.......................Sh. 383,650,000
Kifungu 2005 – *Compliance & Quality Assurance*....... ..............................Sh. 242,900,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion & Coordination*..............................Sh. 550,000,000
Kifungu 4006 – *Inspection & Supervision*............Sh. 550,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiko yoyote)*

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*................................Sh. 700,000,000
Kifungu 1003 – *Policy & Planning Unit*..............Sh. 24,432,150,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*....Sh. 56,397,180,000
Kifungu 1009 – *Management Information System*..........................................Sh. 200,000,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*.................Sh. 80,781,658,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*......Sh. 5,050,000,000
Kifungu 2003 – *Agricultural, Land Use Planning & Management*............................Sh. 3,000,000,000
Kifungu 5001 – *National Food Security*............Sh. 83,947,255,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Fungu 5 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naomba Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Sasa bajeti ya Wizara ya Kilimo imepita rasmi kwa asilimia mia moja. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara ya Kilimo wakishirikiana na Wizara ya Fedha. Kwa kweli mnaonesha na mnaongeza uhai

wa Taifa hili. Kwa sasa huko tunakokwenda, tunakwenda kujitegemea kwa kuongeza uzalishaji mwingi ili Taifa liweze kujitegemea. Hongereni sana. *(Makofi)*

Kulikuwa na hoja hapa za *starch* ya ndani ya Tanzania, haina sababu ya kuagiza *starch* nje. Kulikuwa na hoja ya hawa Maafisa Ugani wako TAMISEMI, kama hawana cha kufanya warudisheni kwenu. Kulikuwa na hoja ya mbegu feki na kulikuwa na hoja ya madawa feki ambayo yanakwenda kwa wakulima. Cha kushangaza, tuna *TBS* ambao ndiyo mamlaka ya kudhibiti ubora wa hizi dawa, lakini mpaka leo wanaoumia ni wakulima.

Sasa Waziri wa Viwanda na Biashara uko hapa, watembelee uwaulize wanapimaje hizi dawa kiasi cha mpaka wakulima wanapata hasara kwa dawa feki kuingia nchini? Nakujua wewe ni mchapakazi mzuri sana, hata ikiwezekana kesho uende uwakague na uwahoji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, nawashukuru sana kwa michango mizuri. Naendelea tena kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Bashe na Naibu wako kwa kazi nzuri ambazo mnazifanya. *(Makofi)*

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 19 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*